

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Pili- Tarehe 5 Septemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Maelezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018 [*The Teacher's Professional Board, Bill 2018*]

MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMI YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Maoni ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018, (*The Teacher's Professional Board, Bill, 2018*)

MHE. CECILIA D. PARESSO – (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):

Maoni ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018, (*The Teacher's Professional Board, Bill, 2018*)]

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali, swali letu la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na linaulizwa na Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Jerome Dismasi Bwanausi, kwa niaba yake Mheshimiwa Chikota.

Na.15

Kujenga Madaraja Jimbo la Lulindi

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA - (K.n.y. MHE. JEROME D. BWANAUSI) aliuliza:-

Madaraja ya Mwitika – Maparawe, Mipande – Mtengula na Mbangara – Mbuyuni yalisombwa na maji wakati wa mafuriko miaka mitano iliyopita na kusababisha matatizo makubwa ya usafiri:-

Je, ni lini Serikali itajenga madaraja hayo ili kuondoa adha ya usafiri inayowakabili wananchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,

naomba kujibu swal i Mheshimiwa Jerome Dismasi Bwanausi Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba madaraja ya Mwitika, Maparawe, Mputeni, Mtengula na Mbangala, Mbuyuni yalisombwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa zilizonyesha mwaka 2015/2016. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii Serikali illifanya tathmini juu ya gharama za ujenzi wa madaraja hayo, ilibainika kuwa kiasi cha shilingi bilioni 3.5 zinahitajika kukamilisha ujenzi wa madaraja hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kiasi hicho cha fedha ni kikubwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeweka kwenye maombi maalumu, hivyo ujenzi wake utategemea kuanza pindi fedha hilo iliyoombwa itakapopatikana. Madaraja hayo yatahudumiwa na Wakala wa Huduma za Barabara Vijiji yaani *TARURA*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza naishukuru Serikali kwa kufanya tathimini ya ujenzi wa madaraja haya. Eneo hili ni muhimu sana kwa uzalishaji wa zao la korosho na wananchi wanapata shida kweli wakati wa kusafirisha korosho kupeleka mnadani. Sasa je, Serikali leo inatoa tamko gani kwamba ni lini ujenzi huu unaanza hata kama ni kwa awamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kikwazo kikubwa cha ujenzi huu ni bajeti ndogo ambayo wamepewa *TARURA*. Sasa je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha ambazo zinaenda *TARURA* ili ujenzi wa madaraja nchini uweze kwenda kwa kasi inayotakiwa?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavo nimekiri kwene majibu yangu ya msingi, kwamba umuhimu wa madaraja haya haina ubishani; lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba ili kujenga madaraja haya kwa kiasi cha pesa kama tulivyotaja kwene tathmini, bilioni 3.5 ni kiasi kingi cha fedha. Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge aiamini Serikali kwamba ina nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba changamoto hii inatatuliwa ipo kinachogomba ni bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anauliza uwezekano wa *TARURA* kuongezewa fedha ili iweze kufanya kazi kubwa. Jana nilijibu swali la nyongeza, kwamba ni vizuri pia tukazingatia kazi kubwa ambayo inafanywa na *TANROADS* na *TARURA* ndiyo tumeanza kuijenga, tuipe muda tuone namna ambavyo inatenda kazi kwa sababu pia itakuwa si busara kusema kiasi kingi cha fedha kitoke *TANROADS* kiende *TARURA* kwa sababu nao wana kazi kubwa ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ukweli utabaki pale pale kwamba *TARURA* inahitaji nyongeza ya fedha. Pamoja na ubovu wa daraja liko tatizo la barabara ambazo zina mawe hazipitiki, kwa mfano katika Jimbo la Rombo, Kata za Handeni, Shimbi, na Makiidi ni Kata ambazo zilikumbwa na volkano na kwa hiyo mawe ni mengi barabara hazitengenezeki. Sasa, je, ni mkakati gani Serikali itakayofanya ili barabara kama hizi ziweze kuitika kwa sababu Vijiji ndiko kwene uzalishaji?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa

Mwenyekiti, nakubaliana na yeye kwamba kuna baadhi ya ameneo ambayo uhitaji wa pesa ni mkubwa. Kwa hiyo iko *case by case*, naomba Mheshimiwa nimhakikishie kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekuwa ikichukua *case by case*, pale ambapo kuna uhitaji maalum kuna fedha ambazo zimekuwa zikitengwa ili kutatua changamoto ambazo zinakuwa zinawakabili wananchi wa maeneo husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa daraja la Gwedegwede lilisombwa na maji wakati wa masika; na kwa kuwa wananchi wa Kata wa Zagaligali, Mbuga, Lumuma, Pwaga na Godegode wanazunguka mpaka Kibakwe, zaidi ya kilomita 75 ndipo wafike Mpwapwa Mjini. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja la Godegode ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wa maeneo hayo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Kandege Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ufupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja ambalo Mheshimiwa analitaja ana uelewa mzuri na daraja hilo. Naomba baada ya kumaliza kipindi hiki cha Bunge tuwasiliane ili tujue; kabla ya kuanza kujenga daraja hilo lazima tufanye tathimini tujue gharama kiasi gani cha fedha inahitajika ili tuhakikishe kwamba daraja hilo linajengwa ili kuondoa adha kwa wananchi ambao wanalazimika kuzunguka umbali mrefu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na pia nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa suala la madaraja yanayounganisha Wilaya kwa Wilaya au hata Kata kwa Kata

ni ya muhimu sana; lleje tulijiongeza kuhusiana na suala hilo kuwa fedha inayohitajika ni kubwa, lakini mahitaji yaliyopo ni madogo. Kwa hiyo tumeomba kwa ombi maalum kuomba fedha ya kimkakati kwa ajili ya daraja linalopita mto Mwalwisi ambalo ndiyo linalotumika na mgodi wa makaa ya mawe Kiwira na Kabulo. Kwa hiyo nilitaka kujuu hatima yake ni nini? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, tafadhalii Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyeekiti, nilipata fursa ya kutembelea lleje, na nimefika Jimboni kwake naomba nimpongeze sana jinsi ambavyo wananchi wa lleje; hakika lleje ambayo ilikuwa inatazamwa miaka hiyo siyo lleje ya sasa hivi, lleje inafunguka.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni ukweli usiopingika kwamba katika maeneo ambayo yana uwekezaji wa kimkakati ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba yanatatuliwa changamoto ili tunapoongelea kwenda kufuata makaa ya mawe kule isiwe ni adha. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mipango ya Serikali ya kuhakikisha kwamba makaa yale tunaanza kuyatumia lazima tufike daraja likiwa limekamilika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Vulu.

Na. 16

Ujenzi wa Barabara za Nzasa – Kilungule

MHE. ZAYNABU M. VULU (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI) aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Nzasa – Kilungule – Buza – Temeke:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hiyo muhimu kwa wakazi wa Mbagala, Mwanagati na Temeke?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nzasa – Kilungule – Buza – Temeke ina urefu wa kilomita 7.6. Barabara hii imeongezwa kwenye mpango wa maboresho ya Jiji ya Dar es Salam kupitia mradi wa *DMDP* na katika awamu inayofuata itajengwa kwa kiwango cha lami. Serikali imekwishalipa fidia ya jumla ya shilingi bilioni 3.25 kwa wananchi 310 ambao wanatakiwa kupisha mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya usanifu imeshakamilika na kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa barabara ya lami kilomita 7.6, ujenzi, wa madaraja mawili yenye urefu wa mita 60 na makalvati makubwa matano kwenye bonde la Mto Mzinga, uwekaji wa taa barabarani jumla ya taa 324 ambazo zinatumia mwanga wa juu; pia kujenga vituo tisa vya mabasi ya daladala. Gharama ya kutengeneza shughuli hii inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 22.6.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Vulu.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Nzasa – Kilungule – Kwa Mwanagati na Buza ni muhimu sana kwa wakazi wa Mbagala, kwa maana ya Jimbo la Temeke na vile vile kwa wakazi wa Jimbo la Ukonga. Je Serikali, ina mpango gani wa muda mfupi wa kuweza kuboresha barabara hiyo ili wakazi hao waweze kupita kwa ufasaha na wepesi kusafirisha mazao na huduma za kijamii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Wilaya Kisarawe, imepakana na Mkoa wa Dar es Salam na Jimbo la Ukonga; na kwa kuwa barabara inayopita Msimbu inaanzia Chanika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha au kujenga lami ya muda mrefu barabara inayoanza Chanika – Msimbu hadi Masaki ambapo itaungana na barabara ya Mwanaromango ili kusaidia ujenzi wa taifa na kuendana na *speed* ya Mheshimiwa Rais kwa sababu tuko kwenye awamu ya viwanda na biashara? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi utaona jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Serikali kwa kupitia mradi wa *DMDP* kuhakikisha kwamba Dar es Salam inajengeka, kwa maana ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ambayo ameisema Mheshimiwa Mbunge kuna jumla ya shilingi bilioni 260 kati ya shilingi bilioni 660 imetengwa kwa ajili ya mradi huu. Naomba nimwondoe hofu, katika mipango ambayo inafanywa na taratibu karibu zote zimekamilika; tukishakamilisha ujenzi wa barabara hiyo ambayo na mimi nimeenda kuitembelea tutaenda mpaka Kisarawe.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya barabara ambazo zina changamoto ya muda mrefu, lakini ni muhimu sana ni barabara ya Makongo kwa mantiki ya kwamba *UCLAS*, Makongo Juu kwenda Goba, hii barabara nimeuliza kwenye swali la TAMISEMI kwa sababu ni barabara ya halmashauri, lakini ina hudumiwa na *TANROADS* kwa mantiki ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba zoezi la tathimini ya kulipa fidia wananchi limeshakamilika, lakini lime *stuck* kwa muda mrefu. Sasa kwa sababu ya umuhimu wa hii barabara na ni barabara ya kimkakati kwa sababu inasadia kupunguza foleni wakati wa ujenzi wa madaraja pale njia ya Ubungo...

MWENYEKITI: Uliza basi swali.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka sasa Waziri aniambie; ni lini ujenzi wa barabara hii utakamilika kumalizia kipande ambacho kimeshaanzwa?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege, ni lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba katika ujenzi wa barabara kuna hatua mbalimbali na katika huu mradi wa *DMDP* lazima ipatikane *no objection* kwa kila hatua. Pale ambapo fidia inatolewa nafasi ili kama kuna malalamiko mengine ambayo yatakuwa *yame-raise*, baada ya kuwa *sorted out* ndipo tunaendelea na hatua ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Halima, na bahati nzuri swala hili tumekuwa tukiwasiliana hata na Mheshimiwa Susan Lymo naamini na ye ye labla anaishi maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongea na Meneja wa *TARURA* kwanza kufanya marekebisho kwa muda wakati wa ujenzi mwingine unasubiriwa. Naomba avute subira, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa; lakini pia kusiwe na malalamiko kutoka kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joyce Sokombi.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuiuliza Serikali; ni lini itajenga barabara itokayo Bunda kwenda Musoma Vijiji ili wananchi wa Kangetuya, Saragana, Bugoji na Kandelema wafaidike kwa sababu wakulima wanapolima mazao yao wanapata shida sana kusafiri kutoka Musoma Vijiji kwenda Bunda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege, kwa kifupi tu.

M NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara zote kubwa zinajengwa; na nimepata fursa ya kwenda Mkoa wa Mara kuna kipande tumeanza kwa ajili ya kujenga daraja pale na ye ye mwenyewe ni shuhuda kama atakuwa amepata nafasi ya kwenda hivi karibuni. Naomba nimhakikishie, Serikali ya Awamu ya Tano, suala la miundombinu ni kipaumbele chetu. Avute subira, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara zote zinajengwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mussa Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Barabara za Jimbo la Ilala zote za Mjini ni mbaya, na tukamuita Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo akaja akashuhudia, wakaitwa watu wa TARURA wote wakashuhudia, lakini mpaka leo barabara za Kalenga, Mindu, Mchikichi, Pemba, Aggrey, Likoma, Bonde, Mali, Utete, Morogoro, Kikuyu, Mafuriko, pamoja na barabara ya Pemba; barabara hizi zote; na barabara zote hizi ndiyo sehemu ya uchumi wa Dar es Salaam na huchangia asilimia 70 ya mapato ya Taifa katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ione umuhimu wa kuboresha kiundombinu hii ili wananchi waendelee kulipa kodi vizuri.

MWENYEKITI: Umepewa ombi, changamoto; Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyeekiti, nawe ni shuhuda jinsi ambavyo Mheshimiwa Zungu anazifahamu barabara, amezitaja nyingi kweli kweli. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Zungu ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara ndani ya Jiji la Dar es Salaam zinajengwa na kuboreshwa kwa kiwango kikubwa. Ndiyo maana kwa kupitia mradi wa DMDP imetengwa jumla ya shilingi bilioni 660 na zitajengwa kilomita 210.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, naamini kabisa barabara ambazo Mheshimiwa Zungu amezitaja zitakuwa ni miongoni mwa barabara ambazo zitajengwa. Tuko kwenye hatua nzuri, baada ya muda si mrefu tutakuwa tumeshaweka Mkandarasi kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hizo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Rashid Akbar Ajali, Mbunge wa Newala Vijijini; linaulizwa kwa Waziri wa Madini.

Na.17

Kugundulika Kwa Madini ya *Coltan*

MHE. MHE. AJALI R. AKBAR aliuliza:-

Madini aina ya *Coltan* yamegundulika katika Wilaya za Ruangwa, Masasi na Newala, lakini Wizara ya Madini imeweeka *beacon* katika Kijiji cha Nandimba, Kata ya Chilagala.

(a) Je, ni utaratibu gani umetumika kuweka *beacon* katika Wilaya nyingine?

(b) Je, Serikali haioni kupora rasilimali ya wilaya nyingine kunaweza kusababisha migogoro?

(c) Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro huo?

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Akbar Ajali, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijiini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Ruangwa, Masasi na Newala hakuna uthibitisho wa uwepo wa madini aina ya *Coltan* yaliyogunduliwa. Madini yaliyogunduliwa katika Wilaya hizo ni aina ya *Graphite* yaani madini ya Kinywe ambapo baadhi ya Kampuni zimepewa leseni za utafiti na uchimbaji wa madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 na Kanuni zake, mmiliki wa leseni anatakiwa kuweka alama (*beacon*) zinazoonesha mipaka ya leseni yake ili jamii inayozunguka maeneo hayo iue mwisho wa leseni husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *beacon* zilizopo katika Kijiji cha Namlimba ziliwekwa na Kamuni ya *Natural Resources Limited* wakati wa ukusanyaji wa taarifa muhimu. Kampuni hii ya *Natural Resources Limited* ina umiliki wa leseni ya utafiti wa madini ya *Graphite* yenye nambari *PL 10644/2015* ambayo mipaka yake inaingia kwenye Wilaya za Masasi na Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina lengo la kupora rasilimali ya Wilaya nyingine bali lengo lake ni kuhakikisha kuwa rasilimali madini zinazopatikana katika eneo husika, zinanufaisha wananchi wake na taifa kwa ujumla. Hadi sasa kampuni hiyo inaendelea na shughuli za utafiti wa madini ya *graphite* (kinywe). Pindi itakapogundulika uwepo

wa mashapo ya kutosha, taratibu za kuvuna rasilimali hiyo kwa manufaa ya Watanzania wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Newala zitafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Kampuni ya *Natural Resources Limited* haina mgogoro wowote na wananchi wa maeneo hayo. Namwomba Mheshimiwa Rashid Akbar Ajali kama kuna tatizo la mipaka ya kiutawala katika Wilaya za Masasi na Newala suala hilo liwasilishwe kwenye Wizara husika kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ajali.

MHE. MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri; lakini naomba nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Wilaya ya Newala na Masasi hatuna mgogoro wa kimpaka ila migogoro ya mipaka watasababaisha watu wa madini. Kitendo cha viongozi wa Wilaya nyingine kwenda kufanya tathmini na kusema wao watalipa fidia kwenye wilaya nyingine wakati viongozi wapo kinavunja heshima kwa viongozi wa wilaya nyingine. Kwa hiyo inaonekana kabisda kwamba viongozi wa wilaya nyingine hawafanyi kazi. Je, Serikali ipo tayari kuacha kuwadhalilisha viongozi wa Wilaya ya Newala kuonekana hawafanyakazi na wanaofanyakazi ni Wilaya ya Masasi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, itakapotokea mrabaha, kama hawa wananchi wa Newala wanakwenda kufanyiwa tathmini Masasi italipwaje na Wilaya ya Newala itapataje haki zake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Nyongo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO): Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro kati ya wilaya moja hadi nyingine, kwa maana ya mgogoro wa viongozi, nadhani ni kwamba ni vizuri tu viongozi hao wakakaa chini wakaelewana kwa sababu hakuna haja ya kugombana katika hatua hii wakati Kampuni ya *Natural Resources* inafanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu mrabaha; hatua za utafiti ni hatua za mwanzo za uchimbaji. Pale madini yatakapogundulika kwamba Kampuni hii imefanya utafiti ikagundua madini yaani katika wilaya zote mbili kwa maana ya Newala na Masasi, basi sisi kama Wizara tutakaa chini na tutaangalia namna ya halmashauri hizi mbili kuweza kuneemeka katika kupata *service levy* na wala si mrabaha kwa sababu mrabaha wenyewe unakusanya na Wizara moja kwa moja, kwa hiyo hakutakuwa na ugomvi, lakini katika *service levy* kwa sababu ni ushuru ambao unakwenda katika halmashauri, tutaangalia na tutakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo siyo suala jipya, kuna maeneo mengine unakuta halmashauri mbili zinaweza zikaneemeka katika *service levy* kwa maana katika mradi mmoja. Kwa hiyo tutaangalia namna ya *service levy* zitakavyogawanya kwenda katika wilaya hizo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, utafiti utakapokwisha tutajua kwa sababu inawezekana ile leseni ya utafiti iko wilaya mbili lakini baadaye utafiti ukaonesha kwamba madini haya yapo wilaya moja, kwa hiyo wilaya hiyo ndiyo itakayoneemeka na ushuru wa *service levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa sababu ya muda, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua na linalekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na.18

Hitaji la Kiwanda cha Kuchakata Tumbaku-Tabora

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA aliuliza:-

Katika kuelekea uchumi wa viwanda Tanzania, Serikali imedhamiria kuwepo kwa viwanda vya kimkakati.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha Kiwanda cha Kuchakata ao la Tumbaku kinajengwa katika Mkoa wa Tabora?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mbunge wa Kaliua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina viwanda viwili vya kuchakata Tumbaku vilivyopo Mkoani Morogoro. Viwanda hivyo ni *Tanzania Tobacco Processing Company Limited* na *Alliance One Tobacco Processing Limited*. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kusindika tani 120,000 za tumbaku kwa mwaka lakini vinatumia wastani wa asilimia 50 tu ya uwezo huo kwa sasa. Uwezo unaotumika ni mdogo kutokana na mahitaji ya tumbaku kuendelea kupungua katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usindikaji wa tumbaku una uhusiano wa moja kwa moja na tumbaku inayolimwa ambayo kwa sasa ni wastani wa tani 60,000 kwa mwaka. Uzalishaji umepungua kutoka tani 126,000 mwaka 2010/2011 hadi tani 54,000 mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya tumbaku yamepungua kutokana na kampeni zinazoendelea duniani za kuzuia kutumia tumbaku na bidhaa zake kutokana na

athari za afya na mazingira. Kwa upande mwingine, kampeni hizo zimeathiri uwekezaji katika viwanda vya tumbaku na ajira ikiwemo Mkoani Tabora, takribani wafanyakazi 7,000 wamepunguza kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zao la tumbaku bado lina mcahngo mkubwa katika uchumi wa Taifa, Serikali inaendelea kuwahamasisha wawekezaji kutafuta teknolojia bora zaidi ya kuwekeza katika Mkoa wa Tabora.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora na Kanda ambazo tunalima tumbaku kwa miaka zaidi ya 10 tumekuwa tunaomba kiwanda cha tumbaku kijengwe Mkoa wa Tabora na ikithibitika kabisa kwamba asilimia 60 ya tumbaku ya Tanzania inalimwa Mkoa wa Tabora, lakini mwaka jana tu Serikali imeruhusu kiwanda cha pili kujengwa Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa kiwanda cha Tumbaku Mkoa wa Tabora kwanza kumewanyima ajira vijana wetu wa Tabora, lakini kubwa zaidi ni kwamba wakulima wa tumbaku wanachajiwani gharama za kusafirisha tumbaku kutoka Tabora kupeleka Morogoro, kwa hiyo wanaongezewa maumivu. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali iliruhusu sasa mwaka jana kiwanda kipyaa kujengwa Mkoa wa Morogoro ambako hakulimwi tumbaku, iko tayari sasa kushawishi kile kiwanda kimoja kihamishiwe Mkoa wa Tabora ili wakulima wa Tabora nao pia waweze kunufaika na zao lao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwenye jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kawumba uzalishaji umepungua, ni kweli umepungua lakini umepungua

kutokana na wakulima hawapewi makisio na kampuni. Wana lengo la kulima, wanakopa hata msimu huu wenyewe tu Kaliua peke yake zaidi ya Vyama vya Msingi sita vimekosa makisio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zao hili ni zao la uchumi wa Taifa na Mkoa wa Tabora, je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kwamba Vyama vya Msingi ambavyo vimekosa makisio mwaka huu vinapatiwa makisio? Kwa sababu uchumi wa Tabora unategemea tumbaku na uchumi wa familia unategemea tumbaku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, *Engineer Manyanya* kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na dhamira nzuri ya Serikali na wananchi wa Tabora kupenda kujenga Kiwanda cha Kuchakata Tumbaku Tabora lakini pia Muwekezaji huwa anaangalia mazingira ya yanayoweza kumuwezesha kupata faida zaidi na kufanya shughuli zake vizuri zaidi. Kwa hiyo kama tulivyosema awali tutaendelea kuhamasisha lakini pia kuwakatisha tamaa wale ambao wameamua kuwekeza Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kuhusu kutoa makisio; kwa kweli kama kuna zao ambalo linapambana na changamoto ni pamoja na hili la tumbaku. Fikiria mteja anaanza kwanza kuhamasishwa "uvutaji wa sigara ni hatari kwa maisha yako" lakini pia uweze kufanya biashara. Kwa hiyo kwa misingi hii unakuta hata kampuni wakati mwingine zinashindwa kufikia malengo kutokana na mazingira kama hayo. Hata hivyo, nizidi kuwaomba wananchi wa Tabora, wote kwa pamoja tutaendelea kufuatilia na kuona kwamba hali ya bei yanzuri kwa upande wa wakulima inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali ya Awamu ya Tano imejinasibu kwamba ni Serikali ya viwanda na tunataka kuhakikisha tutakapofikia mwaka 2025 tuwe kwenye nchi ya kipato cha kat. Sasa nataka kufahamu kutoka kwa Waziri; tulipofanya vikao vya Kamati alikuwa anatueleza kwamba maghala ya korosho yaliyopo Masasi yamegeuzwa, tunafahamu, kufanywa maghala badala ya viwanda na kwamba kuna kesi zilizoko mahakamani kwa sababu ya kutanzua migogoro iliyoko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, mpaka sasa hivi wamefikia hatua gani ya kesi hizi zilizoko mahakamani ili kuhakikisha viwanda vile vinafuliwa badala ya kuendelea kutumika kama maghala na wale watu waliovinunua wakati huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, *Engineer Manyanya*.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza katika majibu yangu ya hapo awali niliahidi kutembelea eneo hilo, nasikitika kuliarifu Bunge kwamba sikuweza kutembelea. Hata hivyo, kama ambavyo nimekuwa nikizungumza siku zote, Wizara kwa kushirikiana pia na Kamati yetu ya Viwanda, Biashara na Mazingira tupo katika kuendelea kuhakikisha kuona kwamba wawekezaji wanatimiza wajibu wao, lakini pia kuhakikisha maeneo yote ambayo yanalima korosho basi korosho hiyo iweze kubanguliwa au kuongezwa thamani kabla ya kusafirishwa. Kwa hiyo tupo katika mchakato na mchakato wa kisheria kawaida huwa hatuuingilii.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa SimwanzaSitta

MHE. MAGRET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swalii la nyongeza. Kwa kuwa tumbaku nyingi inayolimwa Mkoo wa Tabora inatoka Wilaya ya Urambo, Kaliua, Uyui na kwingineko. Je, Serikali iko tayari kuja kuona eneo ambalo lilishatengwa kwa ajili ya kiwanda Wilayani Urambo? Kwa kuwa wakulima wanapoteza kilo nyingi sana kusafirisha tumbaku kutoka Tabora kupeleka Morogoro.

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa *Engineer Manyanya*.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutakapopata nafasi tutaweza kuja kuona na kushauri kadri itakavyowezekana japo kama ambavyo hapo awali nimeeleza changamoto zinazojitokeza.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mbunge wa Viti Maalum.

Na.19

Hitaji la Gari la Zimamoto Mkoo wa Singida

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE aliuliza:-

Mkoo wa Singida unakua kwa kasi sana na ujenzi wa majengo makubwa ya kisasa umeongezeka, lakini kwa muda mrefu sasa hakuna gari la zimamoto linaloweza kuhudumia mkoo; gari lililopo kwa sasa ni bovu na lina ujazo wa lita 1,500 tu na lenye ujazo wa lita 7,000 lilipata ajali miaka iliyopita na Serikali iliahidi kulifanyia matengenezo lakini mpaka sasa haijafanya hivyo:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la kisasa la zimamoto Mkoani Singida ili kukabiliiana na majanga ya moto yanayoweza kutokea?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Mkoa wa Singida unakua kwa kasi ingawa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina gari moja lenye ujazo wa lita 1,500 ambalo linafanya kazi zake na gari la pili ni bovu. Hata hivyo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kulifanyia matengenezo gari la pili ambalo ujazo wake ni lita 7,000 na pindi fedha zitakapopatikana gari zote mbili zitaweza kufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha shughuli za zimamoto na uokoaji, Serikali kwa kupitia bajeti ya mwaka 2018/2019, imepanga kununua gari tano za zimamoto ambazo zitagawiwa katika maeneo mbalimbali nchini yenye uhitaji mkubwa. Aidha, Wizara inaandaa marekebisho ya Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Namba 14 ya Mwaka 2017 ili kuzitaka halmashauri za manispaa, miji na wilaya kununua magari ya kuzimia moto ili kuondokana na upungufu mkubwa wa magari uliopo hivi sasa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Matembe.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swalii la kwanza, kwa kuwa Mkoa wa Singida unakua kwa kasi na majanga ya moto yamekuwa yakitokea mara kwa mara, yakihusisha makazi na pia vile vile kwenye barabara kuu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuupatia Mkoa wa Singida gari la kisasa la zimamoto ili kuokoa maisha na mali za wananchi wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa kuwa gari la zimamoto lililopo ni bovu na halikidhi mahitaji; na ili kutoka

Singida Mjini hadi kufika Wilayani Iramba, Manyoni, Mkalama na Ikungi kuna umbali mrefu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipa kipaumbele Wilaya hizi kwa kuzipatia magari ya kisasa ya zimamoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni mpango gani wa Serikali wa kupeleka magari Singida pamoja na wilaya nyingine ambazo inazunguka; ni kama ambavyo nimejibu kwenye swalii msingi, kwamba, kwanza tutahakikisha tunafanya ukarabati wa lile gari bovu haraka iwezekanavyo pale tu fedha itakapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika bajeti yetu mwaka huu tumepanga kununua gari tano, kwa hiyo tutaangalia Singida kama ni mmoja wa Mkoa wa vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kama ambavyo nimesema, ule mchakato wa kurekebisha sheria utakapokuwa tayari nadhani itasaldia sasa Halmashauri za Wilaya zilizopo katika Mkoa wa Singida kuweza kuchangia katika kununua magari haya yaweze kusaidia katika wilaya za nchi nzima.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Semuguruka.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swalii la nyongeza. Swalii namba 19 lilitoulizwa linafanana kabisa na changamoto iliyopo Jimbo la Ngara. Hivi juzi tulishuhudia gari zikiungua border ya Rusumo na ikapelekea kifo cha dereva, hakukuwa na gari la zimamoto. Je, ni lini Serikali itatuletea gari la zimamoto Wilaya ya Ngara?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ni lini utawapelekea gari ya zimamoto.

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Oliver kutokana na kuumwa kwake na maendeleo ya vyombo ama taasisi zetu zilizopo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mkoa wa Kagera ikiwemo Jeshi la Zimamoto. Kuhusiana na Wilaya ya Ngara, ukiachilia mbali mikakati ambayo nimeizungumzia nikijibu swali la msingi la Mheshimiwa Aisharose Matembe ambalo linagusa Wilaya zote nchini, mikakati ni ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna pia tuna mipango mingine mbalimbali ambayo tunaendelea nayo, ambayo tunaamini kabisa ikikaa sawa basi changamoto hii ya upungufu wa magari ya zimamoto itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango wa kuweza kupata mkopo kuitia nchi za Belgium na Australia ambayo itatuwezesha kupata vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari mapya kabisa. Michakato ya kupata mikopo hiyo nayo inakwenda vizuri na iko katika hatua nzuri pale ambapo itakapokuwa imekamilika naamini kabisa tukichanganya na mikakati niliyozungumza katika swali la msingi basi matatizo ya magari ya zimamoto na vitendea kazi nchini ikiwemo Ngara yatakuwa yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gashaza, Mheshimiwa Kapufi.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa, Mwenyekiti, pamoja na kwamba....

MWENYEKITI: Tuwatendee haki watu wa nyuma huko.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Oliver Semuguruka ameuliza swalii hilo lakini nataka kusema kwamba Ngara ni sehemu ambayo ni *special zone*, ni mpakani. Tuna vituo viwili vya forodha vya pamoja, *one stop border post* kwenye mpaka wa Burundi na Tanzania na mpaka wa Rwanda na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali iliyo tokeea ya moto ya tarehe 19 mwezi wa jana ni ajali kubwa, gari sita zikaungua, dereva akafa, kwa hiyo tunaombwa Serikali iweze kuchukua nafasi na iweze kuchukua hatua ili tuweze kupata gari kwenye vituo hivi ambavyo sasa kumekuweko na msongamano mkubwa. Tayari Kamati ya Ulinzi na Usalama ilikwisha andika barua tangu tarehe 18 Mei, kwa hiyo tunaombwa ichukue hatua ya dharura kwa ajili ya maeneo haya (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa kifupi tu, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, *EngineerMasauni*.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi na tunaichukulia kwa uzito unaostahili. Tunatambua changamoto na *location* ya ile wilaya yake, Wilaya ya Ngara ama jimbo lake liliivyo, kuna umuhimu wa kuwepo kwa gari la polisi pale kwa sababu Mkoa wa Kagera tuna gari nadhani hazizidi nne ambazo zinasaidia kutoa huduma ikiwemo maeneo ya Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua umuhimu wa hilo jambo na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalichukulia uzito unaostahili.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa kwa sababu ya muda tunaendelea. Swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na.20

Mgogoro Kati ya Hifadhi na Wananchi – Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopakana na hifadhi za misitu katika Wilaya ya Urambo wamepitia migogoro mingi ya mipaka na hata kuchomewa nyumba na mali:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya mipaka katika Kata za Nsenda, Uyumbu na Ukondamayo ili wananchi waendelee na kilimo pamoja na shughuli nyingine za kuwaletea maendeleo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Nsenda na Ukondamoyo ni mojawapo ya kata zinazopakana na Msitu wa Hifadhi wa North Ugalla. Msitu wa Hifadhi wa North Ugalla ulitengwa mwaka 1956 ukiwa na hekta 278,423.3 na kusajiliwa kwa ramani namba 307 chini ya Wilaya ya Tabora. Mwaka 2008 eneo la mpaka wa kaskazini mwa msitu ulipunguzwa kwa zaidi ya umbali wa kilomita tano, sawa na eneo la hekta 114,940.91 kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Hivyo, mwaka 2008 eneo la msitu wa North Ugalla lililobaki ni hekta 163,482.39 kwa ramani 2,567 iliyosajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msitu huu umehifadhiwa kwa madhumuni ya kutunza ardhi na udongo eneo la lindimaji (*catchment area*), kuhifadhi bioanuai, kurekebisha hali ya hewa, kuzalisha mazao ya timbao na yasiyo ya timbao kwa ajili ya kutumiwa kwa utaratibu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014, wananchi waliovamia msitu huo waliondolewa kwa mujibu wa Sheria

ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002. Hatua zilizochukuliwa za kuondoa migogoro ya mipaka kati ya Vijiji vya Kata za Nsenda na Ukondamoyo ilikuwa; kwanza kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji husika. Mpango huo uliandaliwa mwaka 2017 na Serikali za Vijiji kwa kushirikiana na Mradi wa Miombo chini ya usimamizi wa Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ya kutayarisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ilifanyika bila ya kuwa mgogoro wowote. Aidha, hati miliki za kimila zinaendelea kutolewa na elimu kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu katika vijiji husika. Hatua hii ya utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya kutambua, kubaini mipaka halali ya vijiji na mpaka wa hifadhi ya msitu wa North Ugalla zinafanyika kwa ushirikishaji wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Uyumbu kuna Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya *UWIMA* ambayo inaundwa na Vijiji vitatu vya Izimbili, Nsogoro na Izegabatogilwe. Vijiji hivyo vilisaidiwa kutengeneza Mpango wa matumizi bora ya ardhi mwaka 2004. Mwaka 2006 mpaka 2007, baadhi ya wananchi walivamia eneo la ukanda wa malisho linalotumika kama ushoroba. Mwaka 2007 wananchi hao waliondolewa kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kijiji cha Tebhela ambao awali kilikuwa Kitongoji cha kijiji cha Nsogoro walivamia eneo hilo kwa kuweka makazi, kuendesha kilimo na malisho ya mifugo. Hivyo, tatizo lillipo ni uanzishwaji wa eneo jipya la utawala (Kijiji cha Tebhela) bila kuzingatia eneo lillipo. Hata hivyo *UWIMA* na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo wamefanya mikutano kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuheshimu mipaka ya Hifadhi ya Jamii na matumizi bora ya ardhi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Margareth Sitta.

MHE. MARGARETH S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Awali

ya yote namshukuru Naibu Waziri alifika mwenyewe na kujionea utata uliopo, kati ya mipaka iliyowekwa. Kuna mipaka miwili, wa zamani na wa sasa, ambayo imesababisha wananchi kutolewa kwa nguvu na hata kupoteza mali zao. Swali la kwanza; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alifika ye ye mwenyewe na kujionea utata uliopo anasemaje kuhusu utata ambao aliuona?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana na mimi kwenda kukaa kumaliza kabisa utata uliopo pale ili wananchi waendelee na shughuli zao?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Hasunga.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi kumpongeza sana Mheshimiwa Margaret Sitta kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika kuhakikisha kwamba anasimamia uchangishaji wa fedha kwa ajili ya vyoo vya mfano katika shule zetu katika majimbo yote. Nakupongeza sana mama yangu kwa kazi nzuri ambayo umekuwa ukiifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumpongeza kwa jinsi ambavyo amekuwa akilifuatilia hili suala kwa muda mrefu. Nakumbuka mimi mwenyewe nilifika katika lile eneo kweli, tuliangalia utata wa mipaka iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia agizo la Bunge la mwezi wa Sita katika kipindi cha bajeti tulikubaliana kwamba mipaka yote lazima iwekwe kwa ushirikishwaji wa wananchi, viongozi, Wizara ya Ardhi pamoja na Maliasili. Kwa hiyo, nasema tu kwamba, tuko tayari tutashirikiana na Wizara zinazohusika na wadau mbalimbali kuhakikisha utata wa migogoro ya mipaka iliyopo unatatuliwa mara moja na wananchi wanaendelea kufanya kazi zao kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niko tayari kabisa kufuatana naye lakini wakati nitakapofuatana naye nitaomba kwamba twende pamoja na Waziri wa Ardhi ili tuweze kuhakikisha kwamba wote tunajionea uhalisia uliopo katika eneo hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamida.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, alifanya ziara Mkoa wetu wa Lindi kuja kumaliza mgogoro wa mpaka wa Kikulyungu Wilaya ya Liwale lakini na mpaka wa Selous na Wilaya ya Kilwa. Kwa bahati mbaya sana kwa dharura iliyojitokeza Mheshimiwa Naibu Waziri alishindwa kukamilisha ile kazi. Sasa ningependa kujua ni lini Serikali itakuja sasa kumaliza ule mgogoro ili wananchi wa Kikulyungu na wananchi wa Wilaya ya Kilwa waendelee kufanya shughuli zao? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu ya swali hilo kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kujibu naomba niseme kweli kwamba nilikuwa nimeenda kwenye lile eneo hasa katika Wilaya ya Liwale kwa ajili ya kushughulikia ule mgogoro ambaeo upo katika Kijiji cha Kikulyungu. Bahati mbaya siku ile wakati tunajipanga kuelekea kule ndiyo siku ambapo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alipata ajali kwa hiyo nikalazimika kuahirisha ile safari ndiyo maana sikuweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na Maafisa mbalimbali wa kutoka Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili walienda katika eneo husika walikaa na wananchi wakatoa elimu na wananchi wakawapoea na wakawa sasa kwamba wako tayari sasa kushirikiana kwa pamoja ili kuweza kubaini mpaka uliopo na kuondoa huo mgogoro ambaeo umedumu kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kusema kwamba, sasa tuko tayari wakati wowote tena tutarudi kuhakikisha kwamba sasa tunashirikiana na wananchi katika kuonesha mipaka ya eneo hilo husika na Mheshimiwa Mbunge utashirikishwa kikamilifu katika hilo suala.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata kwa Wizara hiyo hiyo, linaulizwa na Mheshimiwa Suzan Limbwene Kiwanga, Mbunge wa Mlimba.

Na. 21

**Kuweka Mipaka Kutenganisha Vijiji vya Jimbo la
Mlimba na Ramsar Site**

MHE. SUSAN L. KIWANGA aliuliza:-

Serikali iliahidi kuweka mipaka ya kutenganisha Vijiji vya Jimbo la Mlimba na *RAMSAR SITE* kwa kuwashirikisha wanavijiji wa maeneo husika lakini kazi hiyo haikufanyika badala yake wakulima waliambiwa mwisho wao kwenye maeneo hayo ni mwezi Agosti na wafugaji mwisho wao kwenye maeneo yao ni Julai:-

(a) Je, kwa nini Serikali haikutekeleza jukumu lake la kuweka mipaka badala yake wakulima na wafugaji wamepewa barua ya kusitisha kutumia maeneo hayo na kusababisha taharuki kubwa kwa wananchi?

(b) Kwa kuwa wananchi hao walifungua kesi kupinga maonevu hayo mwaka 2015 kesi Na. 161 kuhusu mgogoro huo na bado kesi hiyo haijawkisha, kwa nini Serikali imewasitisha wananchi hao kuendelea kutumia maeneo hayo kabla ya kesi haijakamilika?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga,

Mbunge wa Mlimba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekaji wa alama za mipaka kwenye maeneo yaliyohifadhiwa kisheria hufanyika kwa kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika. Katika Pori Tengefu la Kilombero, zoezi la uwekaji wa alama za mipaka (vizingi) limefanyika kwa kuwashirikisha wananchi ambapo hadi kufikia Agosti, 2018, jumla ya vizingi 143 vimesimikwa kwa upande wa Wilaya za Malinyi na Ulanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika Wilaya ya Kilombero zoezi la uelimishaji wananchi limefanyika katika vijiji saba vya Miwangani, Namwawala, Idandu, Mofu, Ikwambi, Miomboni na Kalenga. Baada ya hatua hiyo, uwekaji wa alama ya mipaka utaendelea na utashirikisha wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wananchi walifungua Kesi ya Ardhi Na.161 ya mwaka 2015 kupinga zoezi la Operesheni Okoa Bonde la Kilombero iliyofanyika mwaka 2012 kwa madai ya kuwa watu wanaofanya shughuli katika bonde hilo walipwe stahiki zao na kupewa muda muafaka wa kuondoka. Hoja ya wananchi hao ililenga kuiomba Mahakama izuie Serikali katika kuendesha operesheni tajwa kupitia Shauri Na.357 la Mwaka 2017 yaani *Miscellaneous Land Application No.357 of 2017*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mahakama kusikiliza ombi la wananchi hao ilionekana kutokuwa na tija hivyo ikaamua kutokukubaliana na shauri hilo na badala yake ikaelekeza kesi ya msingi Na. 161 ya mwaka 2015 iendelee kusikilizwa, kesi hiyo itatajwa tena tarehe 19/9/2018. Hata hivyo, kesi iliyopo mahakamani kwa sasa haizui Serikali kuendelea na operesheni itakayosaidia kuokoa Bonde la Kilombero ambalo ni muhimu sana katika kulinda ardhi oevu na ni chanzo kikubwa cha maji ya Mto Rufiji unaotegemewa kwa uzalishaji wa umeme kupitia mradi wa Rufiji.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kiwanga.

MHE.SUZAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Naibu Waziri. Mheshimiwa Waziri, amezungumzia suala la Malinyi na Ulanga, swali langu liliijklita zaidi Jimbo la Mlimba lenye kata 16 na kuna kata zisizopungua 14 ambazo zinatakiwa ziende zikafanyiwe marekebisho; na jibu lake limejikita kwenye kata tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na mpango huo wa Serikali kutaka kuhifadhi hilo eneo, wananchi hatukatai, lakini kuna barua zimeshasambazwa kwamba, wananchi wanatakiwa waondoke, wafugaji na wakulima mwisho tarehe 30 mwezi Agosti. Zoezi la uelimishaji kweli limefanyika katika vijiji hivyo saba na imeundwa timu ya watu 15, lakini kiangazi ndiyo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliahidi tangu mwezi Agosti watamaliza hilo zoezi kwenye hizo kata 14, ona, wamefikia kata tatu hata kata tatu wameunda tu timu lakini hawaenda kuweka vizingi. Je, lini sasa Serikali itaenda kuweka vizingi kwa kisababisho kwamba hamna hela? Kwa nini wanatufanya hivi jamani? Lini watakwenda, hilo swalila kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalilala pili, kwa kuwa wananchi hawana uhakika wa maeneo haya kama yataenda kwenye hifadhi ama watabaki nayo, katika kata zote 14 wananchi wanagoma kuchangia maendeleo ya kujenga shule na zahanati kwa sababu hawajui hatima yao katika maeneo hayo. Sasa Serikali kwa nini wanaleta kigugumizi hawapeleki hela? Wanatunyang'anya maeneo lakini wanasema hawana hela za kwenda kuweka mipaka na kiangazi ndio hiki je, ikifika wakati wa mvua watakwenda huko?

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE.SUZAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wako tayari kwenda lini waniahidi hapa jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara Maliasili na Utalii Mheshimiwa Hasunga.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza kwa kuamua kushirikiana vizuri kabisa na Serikali kwamba kuna haja ya kuweka hivyo vizingi ili mipaka ieleteke kwa wananchi kusudi waendelee kushughulika na shughuli zao na maeneo ambayo yamehifadhiwa yaendelee kuhifadhiwa, nampongeza sana kwa msimamo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuweka vizingi ni kweli kabisa kwamba tulisimamisha kwa sababu ya mgogoro uliokuwepo, lakini kuna hatua kadhaa ambazo tulikuwa tumezichukua. Hatua ya kwanza tuliunda Kamati ya watu 22 wa kupitia wilaya zote tatu illi waweze kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, namna bora ya kuhakikisha kwamba vile vizingi vinawekwa na kupunguza migogoro ambayo ilikuwepo. Kamati hiyo tunatarajia kwamba itamaliza kazi yake na italeta ripoti wiki mbili zijazo kuanzia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwenda kutenga fedha naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zimetengwa, fedha zipo; na nitumie nafasi hii kweli kuungana naye kwamba ni kipindi muafaka kwa sababu mvua zikianza itakuwa ni vigumu sana kwenda kuweka mipaka katika lile eneo hasa kipindi cha mvua, lakini kipindi hiki ndio kipindi muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutahakikisha kwamba ndani ya mwezi huu wa 10 mipaka hiyo inawekwa na nitaagiza taasisi zinazohusika zihakikishe kwamba hili zoezi linakamilika na wananchi wanashirikishwa na ye ye mwenyewe Mbunge anashiriki kikamilifu katika hilo zoezi ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawasawa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hussein Salim.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Suala la migogoro ya ardhii, misitu, maliasili na wananchi inazidi kuongezeka kila siku hapa nchini hali ambayo inaipatia Serikali hasara kubwa ya kuweka ulinzi katika maeneo hayo, halikadhalika wananchi wanaathirika sana kwa kuchomewa majumba yao na mali zao kuharibiwa kutokana na zoezi hilo. Sasa inaonekana hii dhana ya ushirikishi inayotumika hapa labda inatumika vibaya au hawajashirikishwa kwa dhati. Je, Mheshimiwa Waziri na Serikali yake wako tayari sasa kuja Zanzibar kujifunza mbinu walizotumia katika haya na wakafanikiwa?

MWENYEKITI: Ahsante. Mko tayari kwenda kujifunza Zanzibar ni hilo tu, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba niseme kwamba tuko tayari kabisa kwenda kujifunza mbinu bora za kuhakikisha migogoro hii haipo. Kama walivyofanya Zanzibar basi na sisi tungependa tutumie mbinu hizo hizo kuhakikisha kwamba huku migogoro yote inamalizika.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Almas Athuman Maige Mbunge wa Tabora Kaskazini na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Na. 22

Vijana Wanaojiunga na JKT Kutoka Shule na Vyuo

MHE. ALMAS A. MAIGE aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali kupitia JKT imeanzisha tena mafunzo ya vijana wa kujitolea na wale wa mujibu wa sheria waliomaliza kidato cha sita au kutoka vyuo hapa nchini.

(a) Je, ni kweli kuwa JKT wanachukua wanafunzi kwa mujibu wa sheria kutoka shule na vyuo vya Serikali tu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa vijana kutoka shule na vyuo binafsi wanahitaji pia mafunzo muhimu ya uzalendo na kuijendeleza kiuchumi?

(c) Je, ni vijana wangapi kwa mujibu wa sheria kwa mwaka 2017/2018 wamechukuliwa na JKT katika shule na vyuo binafsi nchini?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa mujibu wa sheria huchukuliwa moja moja kutoka shule za Serikali na binafsi bila kuhusisha vyuo. Vijana kutoka vyuo vya Serikali na binafsi hujunga na mafunzo ya JKT kwa utaratibu wa kujitolea ambapo utaratibu wa kuwapata hupitia katika usaili unaofanyika ngazi za Wilaya na Mikoa ambapo unahuisha pia vijana wengine wenye sifa bila kujali shule aliyoleta.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona umuhimu wa kuchukua vijana kutoka shule na vyuo binafsi kwa ajili ya mafunzo katika Jeshi la Kujenga Taifa, ndio maana uteuzi wa vijana unahuisha shule zote za Serikali na binafsi. Vijana ambao ni wahitimu wa vyuo vya Serikali au binafsi huingia JKT kwa utaratibu wa kujitolea kama nilivyosema awali.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana waliojunga na JKT kutoka shule binafsi idadi yao ni 7,076 ambapo kati yao wavulana ni 5,432 na wasichana ni 1,644. Idadi hiyo ni kati ya vijana 20,000 walioitwa kujunga na mafunzo kwa mujibu wa sheria kwa mwaka 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Almas Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana leo ya Waziri wa Ulinzi ndugu yangu Mheshimiwa Mwinyi nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa vile idadi inayochukuliwa kwa mwaka ni ndogo sana ukilinganisha na idadi ya wanafunzi wanaomaliza shule *form six* na vyuo. Je, Serikali haioni umuhimu wa kupanua kiasi idadi ya wanafunzi hawa ili wapate mafunzo ambayo tunafikiri kwamba ni ya maadili na uzalendo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa vile vijana wengi wanaotoka baada ya mafunzo kutoka JKT husahau au kuacha mafunzo mazuri na maadili waliyofundishwa kule JKT. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafuatilia vijana hawa illi wasisahau mafunzo na kuacha maadili mazuri ya wananchi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Almas Maige kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu idadi ndogo ya vijana tunaowachukua kwa mujibu wa sheria, ni kweli kwamba wahitimu sasa hivi wanazidi 60,000, lakini uwezo wetu wa kuchukua inakadirwa kuwa ni kama 20,000 peke yake. Kwa hiyo iko mikakati ya kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya vijana wanaochukuliwa kwenda JKT kwa kuboresha miundombinu katika kambi tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuziboresha ili ziweze kuchukua vijana wengi zaidi na ni matumaini yetu kwamba kila mwaka tutaendelea kuongeza idadi. Hata hivyo, hivi karibuni tu tumefungua kambi mpya tano katika Mikoa ya Rukwa kule Milimbikwa na Ruwa, Mpwapwa

Dodoma, Makuyuni Arusha, Itaka pamoja na Kibiti. Kwa hivyo ni mategemeo yetu kwamba, kwa kuongeza kambi hizi mpya idadi ya vijana tunaoendelea kuwachukua itaongezeka ili hatimaye wote wanaomaliza *form six* waweze kujunga kwanza na JKT kabla hawajaanza vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la kufuatilia vijana ili wasisahau maadili nadhani hili ni wazo zuri. Mpaka sasa hivi hakuna mkakati wa kuwarudisha tena lakini tunalipokea tutaangalia njia bora zaidi ya kulifuatilia.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. LYMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Majibu ya Mheshimiwa Waziri yamekuwa ni hayo hayo kwa muda mrefu, na maswali yalikuwa ni kwa nini sasa wanafunzi wote wanaomaliza kidato cha sita wasiende JKT kwa sababu lengo la JKT kama ulivyosema mwenyewe ni suala la uzalendo na maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila leo wanasesma wanaboresha, wanaongeza lakini sisi tunachotaka ni kwamba wote Watanzania vijana hawa tunataka wote wawe *in uniform* waweze kutekeleza suala zima la uzalendo na maadili ili nchi yetu maadili yasiendelee kuperomoka, sasa ni lini watahakikisha hilo linafanyika?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema jitihada zimefanyika na zimeonekana. Wakati tunarudisha tena utaratibu wa JKT baada ya kuwa tumeuacha kwa miaka mingi kuanzia mwaka 1994, idadi tuliyokuwa tunaweza kuchukua ilikuwa ndogo sana si zaidi ya vijana 5000; leo tunavyozungumza tayari tumefikia 20,000 na kambi mpya nimezitaja tunazozifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo si maneno tu ya kurudia hii ni mkakati uliopo. Kila mwaka tunaendelea kufungua kambi mpya tunaboresha za zamani na idadi imeendelea kuongezeka. Leo tunavyozungumza kama tunachukua vijana 20,000, bila shaka ndani ya miaka michache ijayo tutawenza kukidhi mahitaji ya vijana 60,000 au 80,000 ambao watakuwa wanahitimu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali moja dogo la nyongeza. Kuna malalamiko kadhaa kwa vijana wale ambao walioajiriwa kwenye Shirika la Uzalishaji Mali la SUMA JKT, kiwango chao cha fedha ni kidogo sana na vijana hawa wanalinda katika maeneo kadhaa na maeneo muhimu kama vile benki. Ni mara kadhaa wamekuwa wakisema kwamba mtapandisha kiwango cha posho cha vijana hawa wa SUMA JKT *Guard*, ni kwa nini basi Serikali imekuwa ikisuasua kwa muda mrefu hawapandishi pesa hizi na ni vijana hwa wanafanya kazi kubwa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud kuhusu vijana wanaofanya kazi kwenye Shirika la SUMA *Guard*. Ni kweli malalamiko hayo na sisi tumeyapata, tumezungumza na Uongozi wa SUMA *Guard* ili waweze kuongeza viwango ambavyo wanawapatia vijana hawa. Hivi sasa tunavyozungumza ukiacha mshahara ile *basic salary*, kuna posho wanazopata za usafiri, za chakula na kadhalika; lakini bado tunakiri kwamba viwango wanavyopewa havikidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kujitahidi kufanya kila linalowezekana ili maslahi kwa ujumla ya vijana

hawa yaweze kuboreka. Kwa ujumla ni kwamba viwango vinavyofuatwa vinaendana na mashirika mengine ya ulinzi. Kwa hivyo ni vyema sisi kama Serikali tuone umuhimu wa kuboresha haya. Jambo hilo limechukuliwa na Uongozi wa SUMA JKT na ni mategemeo yetu kwamba wataweza kuwaboreshea viwango hivyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea swalii linalofuata ni la Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Mjini, linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kiza Mayeye.

Na. 23

Mradi wa Kuboresha Bandari ya Kigoma

MHE. KIZA H. MAYEYE (k. n. y MHE. ZITTO KABWE)
aliuliza:-

Kigoma Ujiji ni Mji wa kibiashara kwa kuwa ni Lango la Magharibi la nchi yetu kuelekea nchi jirani za Maziwa Makuu. Kutokana na hali hiyo Serikali ya Japan kuitia JICA imekuwa ikiandaa mradi wa kuboresha Bandari ya Kigoma kwa miaka kadhaa sasa:-

- (a) Je, Mchakato wa mradi huo umefikia hatua gani hadi sasa?
- (b) Je, mradi huo utagharimu kiasi gani cha fedha na utaboresha maeneo gani ya Bandari ya Kigoma?
- (c) Je, mradi huo utaanza kutekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zitto Ruyagwa Kabwe, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa *JICA* imekuwa ikiandaa mradi wa kuboresha bandari ya Kigoma ambapo tarehe 29 Juni, 2018 Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara ya Fedha na Mipango na Serikali ya Japan kupitia *JICA* zilisaini makubaliano ya kitaalam ya utekelezaji ya ujenzi wa gati la abiria, jengo la kusubiria abiria, ghala la kutunzia mizigo na barabara itakayoelekea kwenye gati jipy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa *JICA* inasubiri kibali cha ufadhili huo kutoka Serikali ya Japan. Mchakato wa kumpata mkandarasi umepangwa kuanza Novemba, 2018 kulingana na makubaliano yaliyofikiwa katи ya Serikali yetu na *JICA*.

(b) Gharama halisi ya mradi zitajullikana baada ya kusaini makubaliano ya ufadhili na kumpata mkandarasi wa ujenzi.

(c) Mradi huo unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi Juni, 2019 kulingana na makubaliano yaliyofikiwa katи ya Serikali yetu na JICA.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kiza Mayeye.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini napenda kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza, upanuzi wa Bandari hii ya Kigoma unakwenda sambamba na Bandari Ndogo za Ujiji na Kibirizi ni lini sasa Serikali watakamilisha ujenzi wa Bandari ya Ujiji na Kibirizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, mwezi wa Nne Mheshimiwa Zitto aliuliza kuhusu Azimio la Mawaziri wa Maziwa haya Makuu ambapo walikubaliana Kigoma kuwa Bandari ya mwisho katika usafirishaji wa mizigo kwenda Mashariki ya Congo na Burundi. Je, Serikali wamefikia wapi katika utekelezaji wa azimio hili na lini watakamilisha ujenzi wa Bandari Kavu ya Katosho Kigoma? Ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano *Engineer Nditiye*.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Bandari Ndogo za Ujiji na Kibirizi ni moja kati ya Bandari za kipaumbele ambazo zinatafutiwa pesa ya ujenzi na Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi ninavyoongea Mheshimiwa Mbunge nikutaarifu tu kwamba Bandari ndogo ya Ujiji na Kibirizi ziko kwenye *lot* moja na zilishatangazwa tenda ya kutafuta mkandarasi wa kujenga na tenda hiyo ilifunguliwa tangu tarehe 28 Agosti na sasa hivi taratibu za kumpata mnunuzi wa kuendelea kuzijenga na kusanifu zinaendelea, na tutakapopata tutamtaarifu lini hizo Bandari zitaanza makandarasi na kuanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii lake la pili Mheshimiwa Mayeye, ni kweli kwamba kulikuwa na changamoto ya kulipa fidia kwa wananchi ambao wako eneo la pale Katoshio na wananchi walishalipwa na walishaachia sehemu kwa ajili ya kujenga Bandari kavu ya Katoshio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizofanyika mpaka sasa hivi ni kusafisha eneo lote kuona mipaka, lakini vilevile tumetangaza tenda kwa ajili ya kumpata mtu wa ku-*design* na kujenga majengo mbalimbali ndani ya eneo hilo na tenda inategemewa kufunguliwa katikati ya mwezi huu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hasna Mwilima na Mheshimiwa Dau.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa swalii la nyongeza. Kwa kuwa Bandari Ndogo za Kirando, Lukoma, Mgambo na Sibwesa hazijakamilika na kwa vile wafanyabiashara wa Jimbo langu la Kigoma Kusini kwenye kata zinazopakana na nchi za DRC,

Burundi na Zambia hufanya biashara zao na kupidishia mizigo kwenye Bandari hii ya Kigoma. Swali langu; kwa kuwa wafanyabiashara hawa hutumia magari makubwa na wanapitia kwenye kivuko cha llagala na kivuko hiki hakina uwezo wa kubeba magari makubwa, je, kwa nini sasa tenda ya kutangazwa ujenzi wa Daraja la llagala haijatangazwa mpaka leo ilhali tumepitisha pesa kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, *Engineer Nditiye.*

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli Serikali kupidia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) inayo mpango wa kujenga Bandari ndogo katika eneo la Kilando na Sibwesa. Mpaka sasa hivi Bandari ya Sibwesa imeshakamilika kwa asilimia 93, tunasubiri tu taratibu mbalimbali za kikandarasi na za kiufundi kwa ajili ya kwenda kuifungua hiyo Bandari ya Sibwesa ianze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Kilando utaratibu wa kumpata mkandarasi unaendelea, tayari watu wameshafanya *design*; tunasubiri tu taratibu zikikamilika tutangaza tenda kwa ajili ya kumpata mtu wa kufanya ukarabati na ujenzi wa Bandari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Daraja la llagala nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari taratibu za mwanzo zimeshaanza za upembuzi yakinifu. Baada ya hapo tutafanya usanifu wa kina ili kupata gharama tutangaze tenda kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kujenga daraja hilo. Ahsante. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge nimesitisha kidogo nina matangazo hapa ya wageni wa Mheshimiwa Spika; kwa sababu baadaye wataenda kuonana na Kiongozi wetu.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Spika na watu walioongozana nao kwenye *Gallery* yetu, Balozi wa Kenya nchini Tanzania Mheshimiwa Dan Kazungu, karibu sana Balozi, ameambatana na Bi. Rose Mugo, Afisa Ubalozi wa Kenya nchini Tanzania pamoja na ndugu Erick Ngilangwa, Afisa kutoka Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaendelea, Mheshimiwa Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Gati la Kilindoni lilipo Wilayani Mafia lipo katika hali mbaya sana. Mbao zake zimechakaa, ngazi imekatika na lile tishali ambalo abiria pale wanapandia limekaa vibaya kiasi kwamba wakati wowote inaweza ikatokea ajali. Sasa Mheshimiwa Waziri ningependa atufafanulie, kwamba imekuwaje, ni lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa wa gati la Kilindoni ukizingatia kwamba ile boti ya *DMY* itaanza kazi mwezi wa 10? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba gati la Kilindoni lipo katika hali isiyoridhisha kwa matumizi ya abira. Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania pamoja na wataalam kutoka *TEMESA* na *DMY* wameshatumwa maeneo yale kwa ajili ya kwenda kufanya ukaguzi na kuleta gharama ambazo zitatumika kutengeneza *BOQ* kwa ajili ya kufanya marekebisho makubwa ambayo tunakiri yanahitajika katika eneo hilo. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa kuteuliwa na linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 24

Ujenzi wa Barabara ya Mkomazi – Same

MHE.SHALLY J. RAYMOND (K.n.y. ANNE K. MALECELA)
aliuliza:

Tarafa ya Ndungu iliyoko Wilaya ya Same imesheheni uchumi mkubwa sana wa mazao ya chakula na biashara, Serikali ya Awamu ya Nne ya Chama cha Mapinduzi illionna hilo na ikakubali kujenga barabara ya lami kutoka Mkomazi kupita Ndungu, Kisiwani hadi Same; barabara hiyo iliwekwa lami vipara vipara kwa kilomita tatu Kihurio, tano Kisiwani, tano Ndungu na tano Maore.

Je, Serikalii haioni kuwa kuna umuhimu wa kuunganisha vipande hivi ili kukamilisha barabara hii ya Mkomazi, Kisiwani hadi Same kwa kiwango cha Lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi yenye urefu wa kilomita 100.5 ni barabara ya Mkoa inayojumuisha kilomita 96.46 zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Kilimanjaro na kilomita 4.04 Mkoa wa Tanga. Kama alivyoeleza vizuri Mheshimiwa Mbunge sehemu tano za barabara hii, zenye jumla ya kilomita 21 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami barabara hii Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilisaini Mkataba wenye thamani ya shilingi milioni 890.221 na Kampuni ya Kihadisi ya *Advanced Engineering Solutions Limited* ya hapa nchini, ikishirikiana na Kampuni ya

Advanced Construction Centre ya Misri ili kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kilomita zote 100.5 za barabara hii. Kazi hiyo ilianza tarehe 28 Juni, 2018 na inatarajiwa kukamilika tarehe 25 Machi, 2019. Kwa sasa taarifa ya awali ya mradi (*Inception Report*) imewasilishwa kwa ajili ya mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa utekelezaji wa Mkataba huu kutawezesha kujulikana kwa gharama za ujenzi hivyo kuweshesa Serikali kuanza hatua za kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo, kwa awamu kadri fedha zitakavyopatikana. Wakati usanifu unaendelea Serikali katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 imetenga jumla ya shilingi milioni 1,113.595 kwa ajili ya kuifanya matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shally Raymond.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena. Nianze kwa kumshukuru sana Naibu Waziri aliyeata muda wa kuitembelea barabara hiyo na Mheshimiwa Anne Kilango mnamo tarehe 8 Agosti. Mheshimiwa Anne Kilango anatumwa salamu na anasema ahsante sana na nadhani aliliona kazi kubwa hiyo. Pamoja na shukurani hizo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maji ni adui mkubwa sana wa barabara ya lami na baada ya mvua kila wakati vile vipande vya lami vilivyojengwa katika eneo husika zikiwemo zile kilomita tatu Kihurio, kilomita tano kisiwani, kilomita tano Ndungu zinaendelea kumomonyoka kila wakati. Je, Serikali haioni sasa kuna kila sababu ya kufanya haraka kuunganisha vipande hivyo ili lami ile iliyowahi isifagiliwe kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wote wa Kilimanjaro ilionekana wazi kwamba katika vikao vya RCC Same iko nyuma sana kwenye miundombinu ya barabara na barabara iliyotajwa hapa ni barabara muhimu ambayo

pia ina Mbuga za Wanyama. Je, ni lini sasa, baada ya upembuzi yakinifu Serikali iko tayari kupeleka hela hiyo mapema ili zoezi hili lifanyike kwa sababu hii ni ahadi ya Waheshimiwa wagombea Marais toka Awamu ya Nne na Awamu ya Tano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa muda wangu sio rafiki, sasa hivi sitakubali maswali ya nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa jinsi ambavyo anafanya kazi zake kutetea Mkoa wa Kilimanjaro na wananchi wake kwa ujumla. Swali lake la kwanza ni kweli kwamba mvua au maji ni adui mkubwa sana wa barabara zetu na hasa zile za lami na hata zile ambazo si za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyooleza katika majibu ya swali la awali, kwamba baada ya usanifu wa kina kukamilika na kujua gharama tutatangaza tena tutampata mkandarasi, tukishampata mkandarasi hatua za haraka za kutafuta pesa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hiyo zitaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, sisi tunasubiri taarifa za kitaalam, zitakapokuwa tayari na kujua gharama hatutachukua muda mrefu kama Serikali kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami na tutaendelea kuilinda hiyo barabara kwa pesa tulioitenga kwenye bajeti ya mwaka huu. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Faida Mohammed

Bakari, Mbunge wa Viti Maalum na linalekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Na. 25

Kiswahili Kutumika Kwenye Mahakama Nchini

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKARI aliuliza:-

Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa letu na kinapaswa kutumika katika nyanja zote ili kukipa hadhi yake:-

Je, kwa nini baadhi ya Mahakama nchini zinatumia lugha ya Kiingereza wakati zinapoendesha mijadala yake na katika kutoa hukumu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Bakari, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya lugha katika Mahakama zetu yamewekwa kwa mujibu wa sheria. Kwa mujibu wa kifungu cha 13(1) na (2) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 (*The Magistrates Courts Act, Cap 11*) lugha inayotumika kuendesha kesi katika mahakama za mwanzo ni Kiswahili. Vile vile lugha itakayotumika katika mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama ya Wilaya ni Kiswahili au Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, shauri linaweza kuendeshwa kwa lugha yoyote kwa maelekezo ya Hakimu anayeendesha kesi katika Mahakama hizo, japokuwa kumbukumbu za shauri na maamuzi zinapaswa kuandikwa katika lugha ya kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwa mujibu wa Kanuni ya Pili ya Kanuni za Lugha za Mahakama na

Kanuni ya Tano ya Kanuni za Mahakama ya Rufani ya Mwaka 2009, lugha itakayotumika kuendesha mashauri katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ni Kiswahili au Kiingereza kutegemea na maelekezo ya Jaji au Mwenyekiti wa Jopo la Majaji japokuwa kumbukumbu na maamuzi ya shauri vinapaswa kuandikwa katika lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kutumika kwa Kiswahili katika Mahakama zetu na hukumu kuandikwa kwa Kiingereza kunatokana na kwamba Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Madola na inafuata mfumo wa *Common Law*. Kwa kuandika hukumu kwa lugha ya Kiingereza imewezesha Mahakama za nchi nyingine za Jumuiya ya Madola kutumia hukumu zetu kama rejea na vivyo hivyo Tanzania kutumia hukumu za nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa mashauri katika Mahakama zetu unaruhusu kutumia lugha zote mbili, Kiswahili au Kiingereza na Mahakama zetu zimekuwa zikizingatia hilo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bakari.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri niko na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa hizi sheria naona kama zitakuwa zimepitwa na wakati; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wetu amekuwa mfano mzuri wa kuhamasisha utumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii langu ni je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba sasa umefika wakati muafaka wa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa matumizi ya Kiswahili katika Mahakama, katika kuandika maamuzi yake kwa lugha hii ya Kiswahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa hata hapa Bungeni unaletewa hii Miswada hii unaiona hii kwa lugha ya Kiingereza, hii ni Tanzania tunaletewa Miswada kwa lugha ya Kiingereza na humu Bungeni kuna watu tofauti na elimu zetu tofauti, watu wanaweza wakajadili wakawa hawapati muafaka mzuri kwa sababu hawaelewi hii lugha iliyomo katika Miswaada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami sasa kwamba ni wakati muafaka katika nchi yetu ya Tanzania tutumie lugha yetu ya Kiswahili, Lugha ya Taifa katika Mahakama na katika Mabunge na katika sehemu zote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Hayo makofi yanaashiria nini? Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameshayatoa. Kuhusiana na lile suala la kwanza la kuendesha mashitaka kwa Kiswahili halafu hukumu zinatolewa kwa lugha ya Kiingereza ametoa maelezo ya kutosha na nafasi ipo kwamba kama mashtaka yanaendeshwa Hakimu au Jaji anaweza kuruhusu yaendelee kwa Kiswahili au kwa Kiingereza; na sababu nadhani amezitoa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuhusu Miswada na pengine sheria kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili hilo lipi katika mpango wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanza na kutafsiri karibu sheria zote ziwe na zisomeke kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu ndiyo lugha inayozungumzwa na kueleweka na watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, suala hili linahitaji rasilimali na tuna changamoto kidogo za rasilimali lakini pia hata utaalam wa kutosha kwa sababu kuna hatari,

sheria ina lugha yake unapoitafsiri tu moja kwa moja kwenda Kiswahili kuna hatari kubwa pia ya kupoteza mantiki iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna changamoto pia ya kuwa na wataalam wanaoweza kutufanya kazi hii kwa usahihi. Hata hivyo, hilo ni kati ya mambo ambayo tumeyawekea mipango tuanze kuyafanya kazi sheria zote ziandikwe kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo liko pale pale kwenye Wizara hiyo hiyo ya Katiba na Sheria. Swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 26

Ukarabati wa Mahakama za Mwanzo

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO aliuliza:-

Baadhi ya Mahakama za Mwanzo kama vile Matemanga, Napakanya na nyingine nyingi ni chakavu na hazipati fedha kwa ajili ya ukarabati hali inayosababisha Mahakimu na watumishi wengine kufanya kazi katika mazingira magumu sana:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa Mahakama hizo?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa baadhi ya maeneo watumishi wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tunduru ina jumla ya Mahakama za Mwanzo tisa ambazo karibu zote majengo yake ni ya zamani sana na mengi yakiwa ni yale yaliyoachwa na mkoloni. Kati ya Mahakama za Mwanzo tisa zilizopo, majengo ambayo angalau yana hali nzuri ni matatu tu, ya Nandembo, Mlingoti na Ndesa. Mengine yaliyosalia yakiwemo ya Matemanga na Nakapanya ni chakavu sana, hayafai kukarabati na hivyo yamepangwa kujengwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa ujenzi wa mahakama, Mahakama ya Mwanzo Nakapanya na Mahakama ya Wilaya ya Tunduru zimepangwa kujengwa mwaka 2019/2020 kulingana na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sikudhani Yasin Chikambo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sisi sote tunafahamu kwamba mahakama ni chombo cha kisheria ambacho kimekuwa kikitoa haki na kuleta amani katika maeneo mbalimbali kwa mujibu wa sheria. Je, Serikali haloni kuchelewa kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa watumishi wa mahakama wakiwemo Mahakimu ni kudhoofisha hali ya utendaji kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, katika jibu la Mheshimiwa Waziri la msingi amekiri kama mahakama hizo ni chakavu na majengo mengi ni yale yaliyoachwa na Mkoloni, je, ni nini tamko la Serikali la kuharakisha ujenzi wa mahakama hizo sambamba na ujenzi wa nyumba za Mahakimu? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa maswali yako. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inatambua changamoto iliyokuwepo katika ujenzi wa mahakama na kwa muda wote tumeendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu kuhakikisha kwamba tunakabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa Wizara tumeamua kushirikiana na Baraza la Nyumba la Taifa na Chuo Kikuu cha Ardhi ili kupitia ujenzi wa nyumba za mahakama na ofisi za mahakama kwa kupitia teknolojia mpya ya moladi tuweze kuzifiki mahakama nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tunajenga mahakama nyingi kadri iwezekanavyo na hii itatokana na upatikanaji wa fedha. Uzuri tunayo teknolojia mpya ya moladi, naamini tutawafikia wananchi wa Tunduru na wao wapate huduma hii ya mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Halima Abdalla Bulembo, Mbunge Viti Maalum.

Na. 27

Uhaba wa Maji – Kagera

MHE. HALIMA ABDALLAH BULEMBO aliuliza:-

Mkoa wa Kagera upo karibu na Ziwa Victoria lakini una uhaba mkubwa wa Maji:-

Je, ni kwa nini Wizara isibuni mradi mkubwa wa kutoa Maji Ziwa Victoria kupeleka Kagera kama ule wa kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda Tabora?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mkoa wa Kagera ni mionganoni mwa mikoa inayopakana na Ziwa Victoria hapa nchini. Kwa Mkoa wa Kagera, Serikali inaendelea kutumia ziwa hilo, ambapo imekamilisha mradi wa maji Manispaa ya Bukoba na maeneo ya pembezoni yanayozunguka Manispaa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua tatizo la maji katika Mkoa wa Kagera hususan katika Miji ya Kayanga, Omurushaka, Kyaka, Bunazi, Ngara, Muleba na Biharamulo, Serikali inaendelea na taratibu za kumpata Mataalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni ambapo usanifu huo utabainisha jinsi ya kutatua matatizo ya maji kwa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa kutumia Ziwa Victoria kuwa chanzo cha maji katika Mkoa wa Kagera kama ulivyotolewa na Mheshimiwa Mbunge umepokelewa na Mataalam Mshauri anayetarajiwa kupatikana mwezi huu wa Septemba, 2018 ataangalia uwezekano kuzingatia ushauri uliotolewa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Halima Bulembo.

MHE. HALIMA ABDALLAH BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Moja ya changamoto mbalimbali za maji ni ukosefu wa vyanzo vya maji, lakini sisi Mkoa wa Kagera Mwenyezi Mungu ametujaalia tuna vyanzo vingi vya maji. Ukiachilia mbali Ziwa Victoria tuna mito mingi ukiwemo Mto Kagera, lakini shida ya maji imekuwa ni kubwa zaidi na kuna wakati Wilaya ya Ngara kuna wanafunzi walilipotiwa kukosa masomo kwa sababu ya kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo Serikali imekuwa ikitekeleza miradi mikubwa ya maji nchini lakini Mkoa wa Kagera umekuwa ukiwekwa pembeni. Waziri atakubaliana na mimi sasa umefika muda Mkoa wa Kagera uwe una mradi mkubwa mmoja wa maji ili uweze kusambaza maji katika vijiji vyote vya Mkoa wa Kagera na huyo Mkandarasi Mshauri atakubali suala hili la kimkakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu langu la pili, Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika la AFD lilikubali kufadhili Mradi wa Maji Bukoba Mjini. Je, Serikali ipo tayari kuwaomba Serikali ya Ufaransa iendelee kufadhili Mkoa wa Kagera ili waweze kutatua tatizo la maji kuwasaidia wananchi hasa hasa akinamama na watoto wa Mkoa wa Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILAI AJI: Mheshimiwa Mwenyekati, napenda kumpongeza mdogo wangu Mheshimiwa Halima Bulembo; ni mionganoni mwa Wabunge makini sana katika Bunge hili na amekuwa ni mtetezi mkubwa sana kwa akinamama na watoto katika suala zima la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie, jukumu la Wizara ya Maji ni kuhakikisha Wanakagera wanapata maji na si maji tu, ni kwa maana ya maji safi salama na yenye kuwatoshaleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu kwa kuona hali ya changamoto ya maji kwa Mkoa wa Kagera tumetekeleza Mradi mkubwa sana katika Mji wa Kagera zaidi ya bilioni thelathini na mbili katika kuhakikisha wananchi wa Bukoba wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; tuna mradi mwininge katika miji 17, tunaenda kujenga mradi mkubwa sana katika Mji wa Kayanga kwa kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa katika kuhakikisha wananchi wa Kagera wanaenda kupata maji hayo. Kingine, katika Bajeti ya mwaka 2018/2019 tumetenga zaidi ya Sh.13,520,000,000/= katika kuhakikisha wananchi wa Kagera wanapata maji. Niwaombe sana wataalam wetu wa maji wa Mkoa wa Kagera wasilale na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera wasimamie fedha hizi katika kuhakikisha zinaenda kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii lake la pili nataka nimitie moyo Mheshimiwa Mbunge; ukisoma Mathayo-7 inasema ombeni nanyi mtapewa, bisheni hodi nanyi mtafunguliwa. Tumeshawafungulia wananchi wa Kagera, sisi tuko tayari kuendelea kuwatafuta wafadhili katika kuhakikisha tunaenda kutatua tatizo la maji Kagera. Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea. Swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 28

Hitaji la Chuo cha VETA

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA aliuliza:-

Serikali iliweka Wilaya ya Mkinga kuwa miongoni mwa Wilaya za kipaumbele kujengewa Chuo cha *VETA*.

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi ya kujenga Chuo cha *VETA* Wilayani Mkinga?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Ole Nasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali naomba kama itakupendeza, kupitia Bunge lako tukufu niwapongeze na kuwatakia kila la kheri vijana wetu 960,202 wanaofanya mitihani ya darasa la saba leo kwenye shule tofauti 16,845. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi kwa ajili ya kuandaa rasilmalliwatu watakaotumika katika viwanda na shughuli nyingine za uzalishaji, hasa wakati huu ambapo Serikali imeazimia kufanya nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Vyuo hivi vitasaidia kuwaandaa vijana ili waweze kujipatia ajira kwa kujajiri au kuajiriwa ikizingatiwa kuwa kundi kubwa la vijana wetu halipati fursa ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wake wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundu Stadi vya Mikoa na Wilaya, ikiwemo Wilaya ya Mkinga, kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Lengo ni kila Mkoa na Wilaya kuwa na Chuo cha Ufundu Stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Stadi za Kazi (*Education and Skills for Productive Jobs – ESPJ*) ambapo kupitia Mradi huu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDC's*) vitakarabatiwa ili kuongeza fursa za mafunzo. Hivyo, katika kipindi hiki ambacho Serikali inaendelea na jitihada hizi, nashauri wananchi wa mikoa na wilaya zote ambazo hazijawa na Vyuo vya VETA kutumia Vyuo vya Ufundu vilivyopo nchini, hususan kwenye

mikoa na wilaya jirani ili vijana wetu waweze kupata ujuzi na stadi muhimu kwa maendeleo ya nchi kwa ujumla.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu haya hayaridhishi hasa ukizingatia kwamba ahadi hii ya Serikali ni ya muda mrefu takriban miaka saba sasa. Pale Mkinga tunategemea uwekezaji mkubwa sana wa kiwanda kikubwa cha *cement*, uwekezaji wa takriban dola bilioni tatu. Uwekezaji ambao utayutia takriban viwanda 11. Sasa kwa muktadha huo, nini mkakati wa Serikali wa kuleta Chuo cha Ufundı pale Mkinga ili vijana waweze kupata stadi zitakazowawezesha kuingia kwenye uchumi huu wa viwanda? (*Makofı*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı la pili, wenzetu wa Singapore kwa kutambua changamoto ya ajira katika nchi yao, wametumia mfumo ambao umewawezesha kuondoka kwenye tatizo, mfumo wa *ku-link* mafunzo ya *VETA* na maeneo ya kimkakati ya uzalishaji (*industrial park*) je, Serikali iko tayari kujifunza kutoka kwa wenzetu ili tuondokane na tatizo tulilonalo? (*Makofı*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa sana Mheshimiwa Kitandula anaposema jibu langu la msingi halijamridhisha kwa sababu kwa kweli kwa miaka mitatu sasa amekuwa kila wakati yupo Wizarani akifuatilia ujenzi wa *VETA* ya Wilayani kwake Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nimhakikishie Mheshimiwa Kitandula kwamba tayari mchakato wa kujenga Chuo cha *VETA* Mkinga umefikia katika hatua za mwisho. Serikali kwa kushirikiana na kampuni ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Dubai inayoitwa *Planet Core* iko katika hatua za mwisho za kuingia mkataba wa *PPPili* waweze kujenga vyuo kumi nchini kikiwepo Chuo cha *VETA* cha Mkinga. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba awe na subira kidogo tu kwa sababu kile ambacho amekuwa akitafuta kwa muda mrefu sasa kiko mbioni kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Swali letu linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum na linaulizwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 29

Ukosefu wa Vitabu nya Kiada

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Vitabu ni nyenzo muhimu sana ya kujifunzia lakini kwa muda mrefu sasa wanafunzi hawana vitabu nya kiada:-

Je, Serikali inawaambia nini Walimu na Wanafunzi wa Shule za Msingi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa vitabu nya kiada kama nyenzo muhimu katika utoaji wa elimu. Kwa umuhimuhuu, Serikali inafanya kila liwezekanalo kuhakikisha wanafunzi wa shule za msingi hawakosi vitabu hivyo. Katika kuhakikisha hilo, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (*TET*) kwa Mwaka wa Fedha 2017/

2018 imechapisha jumla ya nakala 10,232,812 za vitabu vya kiada vya darasa la I-III na kuvisambaza katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Jumla ya mahitaji ya vitabu vya darasa la nne nchini kote ni vitabu 6,700,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imechapa nakala zote za vitabu vya kiada kwa darasa la IV. Kati ya vitabu hivi jumla ya nakala 4 000,000 vimesambazwa. Vitabu hivi vinaenda kugawiwa kwa uwiano 1:1 yaani kitabu kimoja mwanafunzi mmoja. Serikali inakamilisha zoezi la usambazaji katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Mbeya, Iringa na Ruvuma ambayo ilibaki kupokea nakala za kitabu kimoja kukamilisha idadi ya vitabu sita vinavyohitajika. Zoezi hili litakamilika ifikapo tarehe 15 Septemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imezingatia mahitaji ya Wallimu kwa kuchapa na kusambaza vitabu vya kiongozi cha Mwalimu darasa la nne ambapo, jumla ya nakala 190,036 vimechapwa na kusambazwa shulenii. Kwa sasa Serikali inaendelea na uchapaji wa jumla ya nakala 9,000 za vitabu vyote darasa la I-IV kwa ajili ya wanafunzi wenyewe uono hafifu na nakala 14,000 ya vitabu vya nukta nundu kwa wanafunzi wasioona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mikakati ya kuboresha elimu, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa vitabu vyote vinapatikana ili watoto wote wa Kitanzania wapate elimu iliyo bora.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Ukiangalia kwenye majibu ya msingi ya swali langu Waziri anakiri kabisa kwamba bado mpaka sasa hivi wanásambaza vitabu vya darasa la nne na kimsingi darasa la nne wamefanya mitihani. Kwa hiyo ina maana kuna wanafunzi wamekosa vitabu na wamefanya mitihani na hawa watoto pia wanafanya mitihani ya kufanana. Je, Serikali haioni hili ni tatizo kubwa na kwamba ni lazima sasa

watoto wapate vitabu kwa wakati kwa sababu tunajua Walimu nao wana matatizo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; mwaka 2016 Taasisi ya Elimu ilitayarisha vitabu na vitabu hivyo vikaondolewa kwa sababu vilikuwa vibovu sana, lakini mwaka 2018 wametengeneza tena vitabu na baadhi ya vitabu vina matatizo. Je, Serikali haioni kwamba Taasisi ya Elimu imeshindwa kazi yake kwa sababu vile vitabu vilikuwa zaidi ya bilioni 100 tulivyoambiwa na kwamba sasa Serikali haioni kuna haja ya kuwa na ushindani na Sekta Binafsi ili vipatikane vitabu ambavyo vitakuwa bora ili watoto wetu waweze kupata elimu bora? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwepo na changamoto ya kuhakikisha kwamba vijana wetu wa darasa la nne wanapata vitabu kwa wakati. Hata hivyo, kama nilivyoeleza sasa tunaelekea kukamilisha zoezi la kusambaza vitabu hivyo nchi nzima. Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto hiyo sasa tuko mbioni kuachana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la vitabu anavyosema vina makosa tulishatoa rai kwamba kama kuna yeoyote mwenye kitabu kati ya vitabu hivi ambavyo tumechapisha ambaye ameona au anahisi vina makosa atuletee kwa sababu sisi ka Wizara na kama Serikali. Mchakato ambao tumeutumia kuja na vitabu vipyta umetuhakikishia kwamba kuna ubora mkubwa sana katika vitabu vipyta ambavyo vimetoka kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge na wengine wote ambao wao wana vitabu ambavyo wanafikiri vina makosa wavilete kwetu na tutaviangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tayari kulikuwa na vikaragosi vinazungushwa mtaani kumbe

vilikuwa ni vikaragosi nya vitabu nya Kenya. Kuna watu wengi ambao wanajaribu kuichafua Serikali na kuchafua mfumo wetu wa elimu. Kwa hiyo, naombeni mwenye chochote kile ambacho anafikiri ni makosa alete tuangalie kwa sababu sisi tunajiridhisha kuwa vitabu havina makosa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tumezidi sana kipindi chetu cha maswali na sababu zenyewe mnazifahamu. Tutaendelea hivyo hivyo kuhimizana. Majibu ya maswali yanakuwa marefu, tunarembaremba sana lakini muda hautusubiri.

Wageni ambao wako hapa Bungeni leo, tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambao ni wapiga kura wake kutoka Mkoa wa Ruvuma waklongozwa na ndugu George Kazumba. Wageni wetu kutoka Ruvuma, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, ambao ni ndugu Upendo Sanga na ndugu Radhia Sanga. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Kanal (Mst) Masoud Khamis, ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Tanga, ndugu Mohamed Ahmad na ndugu Mwanahamis Iddi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 20 kutoka Shule ya Sekondari ya Mvumi iliyopo Wilaya ya Chamwino Jijini Dodoma. Wanafunzi karibuni sana kwa mafunzo yenu ya leo hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore, anatangaza kwamba leo tarehe 5 Septemba, kutakuwa na ibada ya misa kwa wakristo wakatoliki mara baada ya kuahirishwa Bunge saa

saba katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote wa madhehebu ya Kikristo wanakaribishwa kwenye ibada hiyo.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama kuhusu Faraja *Fund*. Waheshimiwa Wabunge wa Mfuko huu wa Faraja, tunakumbushwa kuendelea kuchangia Mfuko huu kwa mwaka huu wa Fedha 2018/2019 na tunapaswa tuwasilishe michango yetu kwa Katibu, Mheshimiwa Joseph Mhagama.

Haya ndiyo matangazo, tangazo la kwanza nililimaliza, la Spika kwa hiyo tunaendelea. Katibu!

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018 (*The Teacher's Professional Board, Bill, 2018*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu wa mwaka 2018 (*The Tanzania Teacher's Professional Board, Bill, 2018*) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, naomba nianze kwa kumshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika kifungu 21(1)(b) kufuta maneno kuanzia “.....and atleast one year of full time teaching to the satisfaction of the board” ambacho kinaweka sharti la Mwalimu anayesajiliwa kwa mara ya kwanza awe amefanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja, wakati huohuo sheria inabainisha makosa kwa Mwalimu atakayefundisha bila kusajiliwa na bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kufuta sharti hilo kwa mtu anayesajiliwa kwa mara ya kwanza asiwekewe sharti la kuwa na mwaka mmoja wa kufanya kazi kama sharti la kusajiliwa. Kwa kufanya hivyo kutatoa fursa ya Walimu wote waliomaliza ualimu waweze kutambulika na bodi na nchi kufahamu ni kwa kiwango gani ina hazina ya watu wenye taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 21(1)(c) na (d) vifutwe kwa kuwa katika kifungu cha 21(1)(c) kinaweka masharti ya kuweka kiwango cha Mwalimu alichochangia katika kupata elimu yake. Pendekezo hili ni kutokana na utekelezaji wake kuwa ni mgumu na utawazuia Walimu wengi kupata stahiki ya kutambuliwa kama Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21(2),(3) na (4) vinavyoainisha vigezo vya usajili; ni ushauri wa Kamati kuwa, vigezo vitakavyotumika katika usajili viwe ni vile vinavyohusiana na taaluma ya ualimu (*Academic qualifications*) tu na siyo tabia ya mtu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inatoa ushauri kwamba, Waziri akishirikiana na Bodi ya Taaluma ya Walimu waandae miongozo mbalimbali ya kuweza kupata taarifa kuhusu mienendo ya Walimu pamoja na tathmini ya lazima katika maeneo ya kufanya usajili wa Walimu hasa wakati wa kuhuisha leseni kwa kuwa usajili utafanyika mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 23 kinachoainisha *"renewal of registration"*; Kamati inapendekeza kufuta kifungu cha 23(1) na 23(2) kwa kuwa sifa zilizowekwa ni kwa ajili ya kuhuishwa usajili. Ni maoni ya Kamati kwamba Mwalimu atasajiliwa mara moja tu na kinachopaswa kuhuishwa ni leseni ya ufundishaji na siyo usajili. Hivyo basi vifungu hivyo havina mantiki katika sheria hii na kwa kufanya hivyo kifungu hiki kitapangwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 24 kinachohusu *"payment of annual registration fee"*, kinachobainisha ada za usajili wa Mwalimu kuweza kulipa kila mwaka. Kamati inashauri ada hizo ziainishwe katika kanuni za sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 kinachohusu *"criteria for provisional registration"*, kinachotoa masharti ya usajili wa muda kwa Mwalimu; Kamati inashauri kifungu 27(4) kufutwa kwa kuwa hakipo wazi katika masharti ya sifa ya kupewa usajili wa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 29 kinachohusu *"prohibition of teaching by unauthorized teacher"* kinachobainisha katazo la kufundisha kwa Mwalimu ambaye hana usajili wa bodi; Kamati inashauri katika kifungu 29(1) kufuta neno *"be employed as"* na kuweka neno *"employ"* ili kujumuisha waajiri katika zuio la kuajiri Mwalimu ambaye hajapata usajili na kupata leseni. Kifungu 29(2) Kamati inashauri kiongezewe masharti ya adhabu ambayo itatolewa kwa mtu ambaye atakwenda kinyume na sharti hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 30 kinachohusu *"Practicing licence for teacher"* utoaji wa leseni za kufundishia; Kamati inashauri kiongezwe kifungu cha 30(3) kitakachoweka masharti ya muda wa leseni ya kufundishia ya awali kuwa ni miaka mitatu (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 31 kinachohusu *"Renewal of practicing licence for teachers"* kinachoweka sharti la uhuishaji wa leseni ya kufundishia kwa Mwalimu ambaye leseni imekwisha muda wake; Kamati inashauri

kifutwe kwa kuwa masharti yaliyowekwa yanafanana na masharti ya kifungu namba 23 cha sheria hii ambacho kinaainisha uhuishaji wa usajili ambapo Kamati inashauri masharti hayo yawe ya uhuishaji wa leseni na siyo usajili kwa kuwa usajili utafanyika mara moja na uhuishaji ni wa leseni za ufundishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kifungu cha kutoa masharti ya uhuishaji wa leseni kiongeze masharti ya kuwa Mwalimu awe amelipa ada zake, awe na cheti cha usajili pamoja na taarifa za kuwa amejiendeleza kitaaluma kwa kipindi cha matumizi ya leseni yake ya awali ya kufundishia ambayo inapendekezwa kuwa ya miaka mitano baada ya leseni ya awali ya miaka mitatu kwisha muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 35 kinachohusu *"removal of name from register"* kinachoelezea sababu zitakazopelekea bodi kufuta jina la Mwalimu katika rejista ya Walimu; Kamati inashauri kwamba katika kifungu cha 35(e) kufutwa kwa kuwa mtu akifariki amefariki haina mbadala wake. Kwa mantiki hiyo Kamati inashauri kufuta kifungu 35(f).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 45 kinachohusu *"disobedience of summons and refusal to give evidence"*; Kamati inashauri Serikali kwenda kukiangalia tena upya ili kuweka masharti ya sheria hii kuweza kufanyiwa kazi. Kwa kuwa masharti yake hayaendani na makosa yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha cha 50 kinachohusu *"Appeal"* Kifungu cha 50(2) kinachoelezea masharti ya Mwalimu ambaye hataridhishwa na uamuzi wa Waziri kupewa siku 30 za kukata rufaa Mahakama ya Rufaa. Ni maoni ya Kamati kwamba muda huo ni mchache ikizingatiwa miundombinu na maeneo mengi ya Walimu wanakofanya kazi inaweza kuleta changamoto kubwa ya Walimu hao kukosa haki yao ya msingi ya kuweza kukata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kwamba, kifungu hicho kiainishe muda wa kukata rufaa kuwa ni siku tisini yaani miezi mitatu badala ya siku thelathini. Kwa kufanya hivyo upande wa mlalamikaji atakuwa ametendewa haki ya kuweza kukata rufaa pale panapohitajika. Aidha, katika kifungu hicho kibainishe muda wa siku arobaini na tano kwa Waziri mwenye dhamana kuweza kutoa majibu ya Mwalimu aliyekata rufaa kwa kutoridhishwa na maamuzi ya bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 52 kinachohusu "*power to borrow*" kinachoainisha bodi kupewa mamlaka au uwezo wa kukopa fedha kama mkopo wa riba; ni maoni ya Kamati kwamba, bodi imepewa mamlaka makubwa ya kukopa fedha hizo kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kamati inashauri kwamba, ili kutoa nafasi ya uwajibikaji na kulinda dhamana ya bodi, basi mikopo hiyo lazima ipate idhini ya Waziri mwenye dhamana ya Elimu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 59 kinachohusu "*offence for illegal practice*" kimeainisha makosa ya Mwalimu anayefundisha bila kusajiliwa, kwamba atakuwa anatenda makosa na adhabu yake imetajwa katika kifungu hicho; ni maoni ya Kamati kuwa, lionezwe neno "*or licence*" baada ya neno "*registered*" ili kuweka masharti ya Mwalimu anayefundisha bila leseni kupata adhabu sawasawa na Mwalimu anayefundisha bila kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo bodi itakuwa inaendelea kusimamia vyema taaluma ya ualimu hapa nchini kwa kuhakikisha Walimu wote wanaofundisha wanafuata masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 60 kinachohusu "*prohibition for unauthorized teacher*" kinachotoa katazo la mwalimu kufundisha bila ya kibali cha bodi; ni maoni ya Kamati kuwa kifungu hiki kinakaribia kuwa na ufanano wa maudhui na kifungu 29 kinachohusu "*Prohibition of teaching by unauthorized teacher*". Kamati inashauri kwamba, Serikali

ikifanyie marekebisho kifungu hiki ili kiwe kifungu kimoja kinachotoa katazo pamoja na adhabu yake kwa mtu atakayekwenda kinyume na katazo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 63 kuhusu *offences for a teacher who fails to obey summons* kinachoainisha adhabu kwa Mwalimu aliyeshindwa kutii wito wa kufika mbele ya Bodi na kutoa ushahidi na makosa mengine anayoweza kutenda mbele ya Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 64 kinachohusu *general offence and penalty* kinaainisha adhabu itakayotolewa kwa mtu atakayekwenda kinyume na masharti ya sheria hii na adhabu ya kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tatu au kifungo cha miaka mitano au vyote kwa pamoja; ni maoni ya Kamati kwamba adhabu ya fedha haijaonesha ukomo kwa kuwa imetamka kiasi si chini ya shilingi milioni tatu imeacha mwanya wa kulipa faini ya fedha zaidi ya iliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba Kifungu hiki kirekebishwe na kuainisha ukomo wa faini hiyo ili kuondoa utata na wakosaji wengine watakaonekana wanapendeleta au kuonewa kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 68, *Codes of Ethics* ni maoni ya Kamati kuwa haiba ya Mwalimu inategemeana na mazingira ya Mwalimu anakofanya kazi au mwajiri wake ambapo kwa kuweka sharti hili Bodi itakuwa imejipa jukumu kubwa ambalo utekelezaji wake utakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 70 kinachohusu *"replacement certificates"* kinachoainisha utoaji wa cheti kingine cha usajili baada ya kubainika na kuthibitika kwamba cheti cha usajili wa awali kimepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 72 kinachohusu *"regulations"* kwa maana ya kanuni mbalimbali zitakazotungwa ili kusaidia utekelezaji wa sheria hii, ni maoni

ya Kamati kuwa lionezwe sharti la kuweka au kuipa Bodi jukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa mara nyingine tena napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada huu wa Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa William Tate Olenasha, Naibu Waziri; Katibu Mkuu, ndugu Leonard Akwilapo; Naibu Katibu Mkuu ndugu James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Ave Maria Semakafu, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati na kuwasilisha vyema Muswada huu mbele ya Kamati pamoja na kutoa ufanuzi wa kina pale palipohitaji kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutoa mwongozo wa kitaaluma wa kisheria wakati wote wa uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru tena wadau wote waliofika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Aidha, nawashukuru pia wadau ambao walioshindwa kufika mbele ya Kamati kutokana na sababu mbalimbali, lakini waliweza kutuma maoni kuhusu Muswada kwa maandishi. Napenda kuwaeleza kuwa maoni yao yamesaidia kuboresha Muswada huu wa sheria hii muhimu kwa maslahi mapana ya taaluma ya ualimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia na Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa kazi nzuri yenye umahiri katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, ndugu Athuman B. Hussein; na Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati, ndugu Dickson Bisile; pamoja na Makatibu wa Kamati hii ndugu Pamela Pallangyo na ndugu Agnes Nkwera na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Kaimu Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria wa Bunge ndugu Pius Mboya pamoja na wasaidizi wake, ndugu Leorcard Kapongwa na ndugu Rehema Kipera kwa uchambuzi wa kisheria walioufanya kuisadia Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasillisha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa taarifa nzuri kwa niaba ya Kamati na kwa maana hiyo mmelitendea Bunge haki.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU MUSWADA WA
SHERIA YA BODI YA TAALUMA YA WALIMU TANZANIA WA
MWAKA 2018 (THE TANZANIA TEACHERS PROFESSIONAL
BOARD BILL, 2018) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018 (The Tanzania Teachers' Professional Board Bill, 2018). Uwasilishaji huu wa maoni ya Kamati ni kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, uliipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Muswada unaoanzisha kuundwa kwa Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania. Ni kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu chombo hiki kinaundwa kwa ajili ya kusimamia vyema Taaluma ya Ualimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza shughuli hiyo muhimu ya uchambuzi wa Muswada, Kamati ilipata fursa ya kupokea Maelezo ya kina kuhusu Muswada huu wa Sheria inayopendekezwa yaliyowasilishwa mbele ya Kamati siku ya Jumanne **tarehe 21 Agosti, 2018** na Naibu Waziri Mheshimiwa William Tate Ole Nasha, (Mb) ambapo alieleza kuhusu Madhumuni, Sababu za kutungwa kwa Sheria hii na mpangilio mzima wa Muswada huu.

2.0 DHANA YA TAALUMA YA UALIMU

2.1 Historia ya Taaluma ya Ualimu Ulimwenguni

Mheshimiwa Spika, Taaluma ya Ualimu ni moja kati ya Taaluma muhimu duniani kote. Historia ya Taaluma ya Ualimu inaweza kuangaliwa kuanzia miaka ya 561 (Kabla ya Kristo) ambapo mwalimu aliyefahamika kwa jina la *Confucious* alikuwa ndiye mwalimu wa kwanza maarufu wa shule binafsi. Aidha, katika kipindi cha wakoloni watu wengi walajirji walimu binafsi kuwafundisha watoto wao majumbani kwa kuwa hapakuwepo na shule rasmi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Tangu kipindi hicho kuliendelea kuwa na mabadiliko mbalimbali katika sekta ya elimu na kufikia miaka ya 1900 kilitokea mabadiliko makubwa ya uboreshaji wa elimu katika maeneo mbalimbali ulimwenguni ambapo taaluma ya ualimu iliibuka kuwa ni taaluma iliyohitajika sana katika jamii kwa kuwa shule nydingi zilianzishwa na wanaume wengi walitokea kuipenda taaluma ya ualimu na kuamua kuwa walimu ikilinganishwa na wanawake.

2.2 HISTORIA YA UALIMU TANZANIA

Mheshimiwa Spika, Historia ya Elimu Tanzania Bara imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni kabla na

baada ya uhuru. Kabla ya Uhuru kulikuwa na elimu ya kijadi au ya kitamaduni ambayo wakoloni waliita siyo elimu rasmi (*Informal Education*) ambayo kila kabile lilikuwa na mfumo wake wa elimu ya kijadi. Elimu ya kijadi ilitokana na taratibu za kila siku za jamii za makabila mbalimbali ambayo ilipelekea kuwa na aina ya Walimu wa kijadi hasa wenyewe umri mkubwa kwa ajili ya kuwafundisha vijana namna ya kuishi katika jamii hasa wanapobadili rika kutoka utoto, ujana na hatimaye kuingia katika umri wa utu uzima. Elimu hiyo iliyojumuisha maarifa ya nyumbani, stadi za kazi, maadili, utamaduni, mbinu na taratibu nzuri za kufanya kazi na kujilinda kutokana na mabaa ya njaa, magonjwa na maadui wa usalama wa jamii pamoja na mali zao na elimu hii ilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Mheshimiwa Spika, Elimu iliyotolewa wakati wa Ukoloni iliyotambulika kama (*Formal Education*) ililetwa na wageni wa kwanza Tanzania Bara ambao walikuwa ni Waarabu, Wareno, Wajerumani na Waingereza kwa mantiki hiyo taaluma ya ualimu ilishikiliwa na wageni hao na watanganyika hawakuweza kupata fursa ya kufundisha kwa kuwa hawakuwa na taaluma ya ualimu.

Aidha, shule za mataifa mbalimbali zilizoanzishwa zilitofautiana katika malengo, mitaala, sifa na taaluma za walimu, lugha ya kufundishia na ubora wa majengo ya shule na nyumba za walimu. Kwa mfano Waarabu walipoingia walianzisha mafunzo ya Quran, Elimu hii ilitia mkazo uenezi wa dini ya Kiislamu na Utamaduni wa Kiarabu na walimu wake walikuwa ni wakiarabu kwa asilimia kubwa ili kuweza kufanikisha elimu ya kiislamu inasambaa nchini.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Utawala wa Wajerumani na Waingereza ambao ultanguliwa na ujo wa Wamisionari nao walitoa elimu kutokana na imani yao na historia ya nchi walizotoka ambapo elimu ya Wamisionari ilisisitiza uenezi wa dini ya Kikristo. Elimu iliyotolewa katika kipindi cha utawala wa kijerumani ilitilia mkazo stadi, maarifa, mafunzo ya kazi na uraia mwema.

Aidha, mfumo wa elimu ya Waingereza kwa upande wa Tanganyika ulikuwa na misingi ya ubaguzi wa rangi na ulitoa nafasi na nyenzo bora zaidi za elimu kwa watoto wa kizungu na kiasia ikilinganishwa na aina ya elimu iliyotolewa kwa waafrika ambao ni watanganyika. Lengo kubwa la elimu iliyotolewa kwa watanganyika (waafrika) lilikuwa ni kupata watumishi wakiwemo walimu ambao wangetumika katika kutetea matakwa ya wakoloni katika Nyanja mbalimbali zikiwemo za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupata uhuru mwaka 1961, nchi yetu ilirithi mfumo wa elimu uliokuwa wa kibaguzi. Shule zilikuwa katika makundi matatu kwa maana ya shule za Wazungu, Waasia hasa Wahindi na shule za Waafrika. Kila kundi lilikuwa na utaratibu wake wa kutoa elimu husika kama vile masharti ya ajira kwa walimu, mitaala ya kufundishia, mfumo wa mitihani, vitabu viliyotumika, lugha ya kufundishia, usimamizi na utawala.

Katika shule hizo walimu walifundisha walikuwa ni wale waliotokana na aina ya Taifa linalomiliki shule kwa maana ya kwamba walimu wazungu walifundisha katika shule za watoto wa kizungu, Waasia walifundisha watoto wa kiasia na waafrika walifundisha watoto wa kiafrika bila ya watoto wa taifa moja kuchangamana na watoto wa mataifa mengine.

Aidha, kwa upande wa lugha ya kufundishia, kwa shule za Waafrika (Tanzania), lugha ya kufundishia katika shule za msingi ilikuwa Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi la sita na lugha ya Kiingereza ilikuwa ikitumiwa kama lugha ya kufundishia darasa la saba na nane na kuendelea hadi shule za Sekondari. Waasia walikuwa wanatumia lugha zao za asili kama vile Gujarat, Urdu na Kipunjab na Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na shule kutengwa kulingana na utaifa kwa maana ya ubaguzi, walimu pia waligawanyika katika makundi mbalimbali kulingana na utaifa wa wanaowasimamia kwa maana ya wanaosimamiwa na misheni na wale wanaosimamiwa na Serikali.

Kutokana na tofauti hizo kulipelekeea hata utofauti katika upatikanaji wa maslahi yao, kwa mfano Walimu wa Misheni hawakupata haki sawa na walimu wa Serikali kama vile kodi ya pango, matibabu, pensheni na pia malipo ya likizo. Kwa upande wa Walimu wa Serikali, hawakuruhusiwa kujunga na Vyama vya Siasa. Pia walimu hawa walikuwa wanapata uhamisho wa mara kwa mara katika nchi nzima wakati walimu wa misheni walikuwa wakihamishwa kulingana na madhehebu husika.

2.3 HISTORIA YA URASIMISHAJI WA TAALUMA YA UALIMU

2.3.1 Historia ya Vyama vya Walimu Nchini

Mheshimiwa Spika, Historia ya Vyama vya Walimu inatokana na tofauti zilizokuwepo katika Makundi ya Walimu wakati huo. Walimu waliamu kuunda vyama vyao kwa lengo la kutetea maslahi yao. Walimu Waafrika walikuwa na chama chao kilichoJulikana kama Umoja wa Walimu Waafrika Tanganyika (*Tanganyika Union of African Teachers -TUAT*) Walimu waliokuwa wanafundisha shule za Kikatoliki walikuwa na chama chao kilichoJulikana kama Umoja wa walimu Wakatoliki (*Tanzania Catholic Teachers Union – TACTU*).

Mheshimiwa Spika, Vyama hivi viliungana na kuwa chama kimoja kilichoJulikana kama Umoja wa Walimu Tanganyika (*Tanganyika National Union of Teachers – TNUT*). Hatimaye Serikali ikaona umuhimu wa kuwa na chombo cha kushughulikia maslahi ya Walimu wote bila kubagua walimu wa Misheni na Serikali. Chombo hiki kiliitwa Umoja wa Huduma kwa walimu (*Unified Teaching Service- UTS*). Hivi sasa huduma za walimu walioko chini ya ajira ya Serikali zinashughulikiwa na Chama cha Walimu Tanzania – CWT kilichoanzishwa mwaka 1993.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Walimu Tanzania kinawasimamia walimu ambao wapo katika ajira ya Serikali na kuwaacha walimu ambao wapo katika shule binafsi kwakuwa kwa asili ya ajira zao haziwalazimishi kujunga na Chama hicho ili kuweza kutetea maslahi yao, kusimamiwa

weledi wao na hata nidhamu inayohitajika katika taaluma ya Ualimu. Kwa mantiki hiyo, taaluma ya ualimu ilikosa kuwa na usimamizi wa kuangalia ubora, Kamati ya kusimamia maadili, kuwachuja walimu wenye sifa na vigezo vya kufundisha watoto na kuweza kuwawayibisha walimu ambao wanakwenda kinyume na maadili na misingi ya taaluma ya ualimu.

2.3.2 Urasimishaji wa Taaluma ya Ualimu

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi wa Walimu nchini mnamo Mwaka 1989 kilitungwa Sheria ya Tume ya Walimu (*Teachers' Service Commission Act, 1989*) ikiwa na jukumu la kusajili walimu wote waliopo katika utumishi na kutunza kumbukumbu za kila mwalimu aliyeko kwenye utumishi wa Umma. Aidha, majukumu mengine ya Tume yalikuwa ni kumshauri Waziri juu ya usimamizi wa utumishi na kuhakikisha kunakuwepo mazingira mazuri na salama ya kufanya kazi walimu; na pia kuwa kiungo cha maridhiano kati ya mwalimu, mwajiri na Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania (JUWATA).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mnamo **mwaka 2002 kupitia Sheria Na. 8** ya Utumishi wa Umma (*Public Service Act, 2002*), kuliundwa Idara mbalimbali za Tume ya Utumishi ikiwemo Idara ya Utumishi wa Walimu (**Kifungu cha 15 (1) (b)** na majukumu ya kushughulikia masuala ya Walimu yallelezwa katika **Kifungu 6 (4)**, Sheria hii ilifuta Sheria ya Tume ya Walimu ya Mwaka, 1989 (*Teachers' Service Commission Act, 1989*)).

Aidha, mwaka 2015 Bunge lilitunga Sheria nyingine ya Tume ya Walimu (*The Teachers' Service Commission Act, 2015*) ikiwa na wajibu wa kushughulikia masuala ya Walimu wa shule za msingi na sekondari waliopo katika utumishi wa Umma. Sheria hii ilifuta vifungu vya Sheria ya Utumishi wa Umma (*Public Service Act, 2002*) Kifungu Na. 6(4), na 15 (1) (b) vilivyokuwa vinahusu Idara ya Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Tume hii iliyoundwa Mwaka 2015 ni pamoja na kutunza rejestra na kumbukumbu za

walimu wote waliopo kwenye utumishi, kuandaa kanuni za maadili ya Walimu, kusimamia Walimu katika Mafunzo, kuteua, kupandisha na kuwachukulia hatua za kinidhamu walimu hao wa shule za msingi na sekondari walio katika ajira ya Serikali.

3.0 DHUMUNI LA MUSWADA NA UANZISHWAJI WA BODI YA TAALUMA YA WALIMU TANZANIA

Mheshimiwa Spika, Sheria hii itasaidia kusimamia taaluma ya ualimu kwa weledi mkubwa na kuimarisha taaluma ya ualimu na kuipa heshima yake. Kabla ya mapendeleko haya ya Sheria Taaluma ya ualimu ilikuwa inasimamiwa na Tume ya Ualimu ambayo jukumu lake kubwa ilikuwa ni kusimamia walimu walioko katika mfumo wa Serikali na kuwaacha pembeni walimu wanaofundisha katika shule za binafsi ambazo zinamiliki wanafunzi zaldi ya millioni mbili na wanafanya kazi pasipo usimamizi wowote wa taaluma hiyo.

Aidha, Bodi hiyo itakapokuwa tayari itasaidia kusimamia maadili na weledi wa walimu wote nchini na hivyo kuongeza nidhamu na kuinua ubora wa elimu hapa nchini kwa ajili ya ujenzi wa taifa zima.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umeainisha adhabu si chini ya shillingi milioni 3, kifungo jela cha miaka mitano au vyote kwa pamoja endapo mwanataaluma atakiuka masharti yatakayowekwa kwa mujibu wa Sheria hii. Aidha, kwa mujibu wa muswada huu pamoja na majukumu mengine Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania itakuwa na jukumu la kuinua kiwango cha taaluma ya ualimu na kupata walimu mahiri, kuhakikisha inaanizisha na kutunza mfumo wa usajili wa walimu, utoaji wa leseni za kufundishia kwa walimu wote wenye vigezo na wanaohitaji kufundishia, kuweka vigezo na viwango vya mwalimu bora.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unaainisha masharti kuhusu usajili wa walimu, vigezo vya usajili, aina za usajili, ulipaji wa ada ya usajili, utoaji wa leseni kwa walimu na kuweka masharti ya namna ya kuweka na kutunza orodha

ya Walimu. Aidha, Muswada unapendekeza kuweka masharti kuhusu utaratibu wa kuondoa jina la mwanachama kwenye rejista, kufuta na kusimamisha usajili pamoja na adhabu kwa makosa yatokanayo na mwajiri kutoa ajira ya ualimu kwa mwalimu asiyesajiliwa na asiye na leseni ya kufundisha kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa na Muswada wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na malalamiko ya Walimu ya muda mrefu, Muswada wa Sheria umependekeza kuweka masharti kuhusu malalamiko mbalimbali ya Walimu, uchunguzi wa malalamiko, namna ya kushughulikia malalamiko dhidi ya mwalimu, kuunda Kamati ya uchunguzi, wito wa mashahidi, taratibu za uchunguzi, uamuvi wa Bodi dhidi ya malalamiko pamoja na muda wa kukata rufaa kwa mtu ambaye atakuwa hajaridhishwa na uamuvi wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unataja masuala ya fedha hasa vyanzo vya mapato ya Bodi, bajeti ya mwaka, utoaji wa taarifa za mwaka, hesabu za Bodi na ukaguzi wa hesabu hizo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umezingatia uainishaji wa Makosa mbalimbali na adhabu zake ambapo unataja makosa makuu kuwa ni pamoja na mwalimu kuanza kufundisha bila kusajiliwa na Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania au kusajiliwa kinyume cha masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria hii, utoaji wa nyaraka danganyifu na kwa upande wa mwajiri kuajiri mwalimu asiyesajiliwa. Aidha, Muswada unaainisha mamlaka ya Waziri mwenye dhamana kutengeneza kanuni, utengenezaji wa mwongozo wa maadili, taarifa ya uamuvi ya Bodi, faini, ada na tozo zinazotakiwa kulipwa.

4.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, mnamo tarehe 22 na 23 Agosti, 2018, Kamati ilifanya Mkutano na Wadau kwa lengo la kupokea Maoni yao (*Public hearing*) ili kuisaidia

Kamati katika Uchambuzi wa Muswada huu. Wadau hao walialikwa njia mbalimbali ikiwemo kuwaandikia barua rasmi ya wito wa kufika mbela ya Kamati kwa ajili ya kutoa maoni yao (**Rejea Kiambatisho 1**), kutoa taarifa kwa umma na kutoa nafasi kwa mtu ye yeyote mwenye kuhitaji kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yake, mitando ya kijamii, pamoja na taarifa kupitia tovuti ya Bunge (www.parliament.go.tz).

Mheshimiwa Spika, Njia zote hizi ziliwezesha kutoa taarifa kwa umma na wadau mahususi kwa ajili ya kutoa maoni kuhusu muswada huu wa Sheria. Wadau mbalimbali walifika katika Mkutano huo ambaao ni pamoja na Chama cha WanaSheria Tanganyika (Tanganyika Law Society (TLS), TWaweza, HAKI ELIMU, Chama cha kutetea Haki za Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), Tanzania Education Network (TENMET) pamoja na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ambaao walishindwa kufika siku iliyopangwa ya **tarehe 23 Agosti, 2018** na kwa ridhaa yako Mheshimiwa Spika Kamati ilikutana na Chama Cha Walimu Tanzania siku ya **tarehe 24 Agosti, 2018**, ili pia kuweza kupata maoni yao kuhusu Muswada wa Sheria ili kuisaidia Kamati katika uchambuzi wake. Ni imani ya Kamati kwamba ulitoa nafasi hiyo nyingne ya wadau hasa CWT kutoa maoni yao kwa kuwa ultambua umuhimu wa wadau hao katika taaluma ya ualimu.

Aidha, kuna mdau ambaye alishindwa kufika mbele ya Kamati na badala yake alitoa maoni yake kwa maandishi. Mdau huyo ni Stallion Attorneys ambapo maoni hayo yamesaidia pia Kamati kuboresha Muswada huu na kuiwezesha Kamati kuuchambua Muswada na kutoa maoni na ushauri unaowasilishwa leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupokea maoni ya wadau pamoja na majadiliano na wajumbe wa Kamati kuliibuka hoja mbalimbali ambazo Kamati na Serikali kwa pamoja tulikubaliana kuwa hoja hizo zina uzito wake na zingehitaji muda wa kuzifanya kazi hivyo Kamati illazimika kuongeza siku za kufanya kazi na hivyo kuuchambua Muswada huo mpaka **siku ya Jumatatu ya tarehe 27 Agosti, 2018**.

Mheshimiwa Spika, Hoja zilizoibuliwa ni pamoja na kuonekana kugongana kwa baadhi ya majukumu yaliyoainishwa katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu ya mwaka 2012 pamoja na majukumu yaliyoainishwa katika Muswada wa Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018 ambayo ni Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kulingana na umuhimu wa Sheria hii ya kusimamia Taaluma ya Walimu hapa nchini, mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa kuzingatia Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za bunge, Toleo la Januari, 2016 ikisaidiana na wadau waliota maoni yake ya kuboresha Muswada ambayo kwa pamoja Kamati na Serikali waliona kuna umuhimu wa kuyafanya kazi, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilikubaliana na Kamati kwamba marekebisho yote yatawasillishwa na Serikali kwenye Jedwall la marekebisho (*Schedule of Ammendments*) kama ambavyo Kamati imependekeza.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu Muswada huu, naomba nikushukuru tena wewe kwa kuisaidia Kamati kutekeleza jukumu la uchambuzi wa Muswada huu. Vilevile ninaipongeza sana Serikali kwa kuwa wasikivu, waelewa na hata kuweza kuahirisha majukumu yao mengine kwa siku siku ambayo haikupangwa Kamati kuwa nao na kuweza kufika mbele ya Kamati ili kupokea Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa ajili ya kuyafanya kazi.

Ni imani yangu kubwa na Kamati nzima kwamba, tumeisaidia Serikali na wananchi wa Tanzania katika kuiboresha Sheria hii ambayo ipo katika mchakato wa kutungwa kwa ajili ya manufaa ya kuilinda taaluma ya Ualimu, Walimu wote wa Tanzania na watoto wetu wanaofundishwa na watakaofundishwa na walimu hawa ambao tumewawekea ulinzi mzuri kuhusu taaluma yao ya ualimu.

5.0 MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo kwa lengo la kuboresha Muswada huu:-

5.1 MAONI KUHUSU VIFUNGU

- a) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini makosa ya uchapaji na sarufi (*spelling and grammatical errors*) na inashauri **Marekebisho yafanyike kwenye maeneo yote yenye makosa hayo ili kuweka maana stahiki katika vifungu hivyo vilivyoonekana kuwa na makosa ya kiuchapishaji.**
- b) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza **Kifungu cha 3** kuhusu *Interpretation* kuongeza maana ya maneno "*Continuous Professional Development*" kwakuwa neno hilo limetumika katika Muswada na halijatolewa maana yake. Aidha neno "**student**" nalo lifafanuliwe vyema ili kuweka maana halisi ya neno hilo kwakuwa lilivyo sasa linashindwa kuwasilisha aina nydingine ya wanafunzi.
- c) **Mheshimiwa Spika**, Katika maana ya neno "*Tertiary education Institution*" imetolewa maana yake kwamba ni taasisi ya elimu zaidi ya sekondari na haijaonesha ukomo wake kwa maana ya inaishia wapi kwa maana vyuo vikuu vimejumuishwa au la. Kamati inashauri kwamba neno hilo litolewe maana yake na lioneokane katika orodha ya maneno yaliyotafsiriwa ili kuondoa mkanganyiko huo.
- d) **Mheshimiwa Spika**, Katika **Kifungu cha 5(1)(b) (iv)** kinachohusu "*Composition of Board*" ambayo imeeleza kwamba Bodi hiyo ya Taaluma ya Walimu Tanzania itakuwa na wajumbe nane (8) ambao watateuliwa na Waziri mwenye dhamana. Kamati inapendekeza kwamba, katika wajumbe hao Sheria iainishe mjumbe mmoja atokane na wadau binafsi wa masuala ya elimu ambao kwa umoja wao watampendekeza mtu mmoja wa kuwakilisha katika Bodi hiyo kulingana na vigezo vinavyohitajika kuwa mjumbe wa

Bodi. Kwa kufanya hivyo, Bodi hiyo itakuwa imetoa uwiano wa wajumbe wa Bodi wa kuwa na uwakilishi wa Serikali lakini pia wadau wa elimu kutoka Sekta binafsi.

Aidha, katika Kifungu hicho pia, Kamati inapendekeza Sheria iainishe sifa za wajumbe watakaoeuliwa kuwa wajumbe wa Bodi ya Taaluma ya Ualimu. Mfano, Sheria iweke masharti ya ili mtu aweze kuteuliwe kuwa mjumbe wa Bodi anapaswa awe na kiwango cha shahada ya kwanza na sifa nyingine zinaweza zikaainishwa katika Kanuni za Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri pia kuweka ukomo wa kufanya kazi kwa Bodi moja kabla ya kuteua wajumbe wapya wa Bodi hiyo. Hii ni kutokana na kwamba katika Muswada hakuna mahali palipolezea ukomo halisi wa Bodi moja kufanya kazi yake, hivyo Kamati inapendekeza kuwa muda wa maisha ya Bodi moja iwe ni miaka mitatu (3) ili kuwapa wajumbe wengi wapya kufanya kazi katika Bodi hiyo kwa ajili ya kusimamia taaluma ya Ualimu.

e) **Mheshimiwa Spika**, katika **Kifungu cha 6(1)(d)** kuhusu "*Functions of the Board*" Kamati inashauri kufuta neno "*Control*" katika Kifungu hiki ili kuleta maana zaidi katika jukumu linaloainishwa na Kifungu hicho kwakuwa madhumuni ya kuundwa kwa Bodi hii ni kusimamia (**Regulate**) Taaluma ya Ualimu nchini na siyo kudhibiti (**Control**) taaluma hiyo.

f) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11** kinachohusu "*Deputy Registrar*" Naibu Msajili hakijaainisha ukomo wa muda wa kufanya kazi kwa Naibu Msajili wa Bodi ya taaluma ya Walimu. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Sheria iweke ukomo wa madaraka ya Naibu Msajili kama ambavyo imeweka kwa Msajili Mkuu wa Bodi katika **Kifungu cha 10(2)** kinachoainisha ukomo wa Bodi kuwa ni baada ya kipindi cha miaka mitano na atateuliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano kulingana na utendaji wake.

g) **Mheshimiwa Spika**, Katika **Kifungu cha 14 (1)(a)** kinachohusu "*Appointment of supervisory officers*" Kifungu

kinaeleza kuwa maafisa usimamizi hao watatokana na maafisa wakongwe kwa maana ya "*senior professional teachers*". Kamati inashauri kwamba maafisa hao watokane na walimu wenyewe usoefu mkubwa kwa maana ya kwamba isomeke "*Experienced professional teachers*" na watambulike kama "*Assistant Registrars*" badala ya "*supervisors*". Kwa kufanya hivi itarahisisha Sheria kutambua uwepo wa wasaidizi wa Msajili Mkuu wa Bodi ya Walimu badala ya kuonekana kama ni wasimamizi na kuleta mkanganyiko wa kimantiki katika utendaji wa ofisi ya Msajili wa Bodi hiyo.

h) **Mheshimiwa Spika**, Katika Kifungu cha 17 kinachohusu "*Register*" kinachoainisha taarifa zitakazo nakiliwa katika daftari la usajili katika Kifungu **2(g)** kilichoandikwa "*registration number or category of registration*" Kamati inashauri kutenganisha taarifa hizi kwa kuwa zote ni taarifa muhimu kuwepo katika rejesta hiyo kwa maana ya namba ya usajili na ngazi ya usajili ambao mwalimu husika amesajiliwa kama ni usajili wa muda au wa kudumu. Kwa kufanya hivi kutaiwezesha Bodi kutambua sifa za mwalimu husika kwa namba ya usajili, ngazi ya usajili na taarifa nyingine ambazo zimeainishwa katika Kifungu hiki cha 17.

i) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18** kinachohusu "*Qualification for registration*" katika Kifungu cha **18(1) (b)**, kinachotaka kuonesha mtu yuko sawa na sahihi kufanya kazi ya ualimu. Sifa hii kufahamika kwake ni kwa mujibu wa vipimo vya daktari ndiye anaweza kuonesha kama mtu huyo yuko timamu kufanya kazi ya ualimu. Ni ushauri wa Kamati kuwa, Kifungu hicho kifutwe kwakuwa kimeweka sifa ambazo haziwezi kubainika kwa macho wakati wa usajili ili mwalimu huyo aweze kupata usajili wa Bodi.

j) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21** kuhusu "*Criteria for registration*" Kamati inapendekeza **Kifungu 21(1)(a)** kinachoeleza tabia njema ya mwalimu anayeomba usajili wa awali katika rejista. Utekelezaji wa Kifungu hiki ni mgumu kwakuwa tabia ya mtu itatambulika baada ya mwalimu kuwa amekwisha ingia katika kutumika taaluma yake. Ni

maoni ya Kamati kwamba Kifungu hicho kifutwe na kitumike wakati wa kuhuisha leseni yake ya kufundishia.

Aidha katika **Kifungu 21(1)(b)** kufuta maneno kuanzia “.....and atleast one year of full time teaching to the satisfaction of the Board” ambacho kinaweka sharti la mwali mu anayesajiliwa kwa mara ya kwanza awe amefanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja, wakati huohuo Sheria inabainisha makosa kwa mwali mu atakayefundisha bila kusajiliwa na Bodi. Kamati inashauri kufuta sharti hilo kwa mtu anayesajiliwa kwa mara ya kwanza asiwekewe sharti la kuwa na mwaka mmoja wa kufanya kazi kama sharti la kusajiliwa. Kwa kufanya hivyo kutatoa fursa ya Walimu wote waliomaliza ualimu waweze kutambulika na Bodi na nchi kufahamu ni kwa kiwango gani ina hazina ya watu wenye taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu 21 (1)(c) na (d) vifutwe kwakuwa katika **Kifungu cha 21(1)(c)** kinaweka masharti ya kuweka kiwango cha mwali mu alichochangia katika kupata elimu yake. Pendeleko hili ni kuto kana na utekelezaji wake kuwa ni mgumu na utawazuia walimu wengi kupata stahiki ya kutambuliwa kama mwali mu.

Kifungu cha 21 (2), (3) na 4 vinavyoainisha vigezo vya usajili, ni ushauri wa Kamati kuwa, vigezo vitakavyotumika katika usajili viwe ni vile vinavyohusiana na taaluma ya ualimu (*Academic qualifications*) tu na siyo tabia ya mtu husika. Aidha, Kamati inatoa ushauri kwamba, Waziri akishirikiana na Bodi ya Taaluma ya Walimu waandae miongozo mbalimbali ya kuweza kupata taarifa kuhusu mienendo ya Walimu pamoja na tathmini ya lazima katika maeneo ya kufanya usajili wa walimu hasa wakati wa kuhuisha leseni kwa kuwa usajili unafanyika mara moja.

k) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 23** kinachoainisha *“Renewal of registration”* Kamati inapendekeza kufuta **Kifungu cha 23 (1)** na **23(2)** kwakuwa sifa zilizowekwa ni kwa ajili ya kuhuisha usajili. Ni maoni ya Kamati kwamba mwali mu atasajiliwa mara moja tu na kinachopaswa kuhuishwa na

leseni ya ufundishaji na siyo usajili, hivyo basi vifungu hivyo havina mantiki katika Sheria hii na kwa kufanya hivyo Kifungu hiki kitapangwa upya.

- l) **Mheshimiwa Spika, Kifungu 24** kinachohusu "*Payment of annual registration fee*" kinachobainisha ada za usajili wa mwalimu kuweza kulipa kila mwaka. Kamati inashauri ada hiso ziainishwe katika kanuni za Sheria hii.
- m) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27** kinachohusu "*Criteria for provisional registration*" kinachotoa masharti ya usajili wa muda kwa mwalimu, Kamati inashauri **Kifungu 27(4)** kufutwa kwa kuwa hakipo wazi katika masharti ya sifa ya kupewa usajili huo wa muda.
- n) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 29** kinachohusu "*Prohibition of teaching by unauthorized teacher*" kinachobainisha katazo la kufundisha kwa mwalimu ambaye hana usajili wa Bodi, Kamati inashauri katika **Kifungu 29(1)** kufuta neno "*be employed as*" na kuweka neno "*employ*" ili kujumuisha waajiri katika zui la kuajiri mwalimu ambaye hajapata usajili na kupata leseni. Aidha, **Kifungu 29(2)** Kamati inashauri kiongezewe masharti ya adhabu ambayo itatolewa kwa mtu ambaye atakwenda kinyume na sharti hili.
- o) **Mheshimiwa Spika, Katika Kifungu cha 30** kinachohusu "*Practicing licence for teacher*" utoaji wa leseni za kufundishia, Kamati inashauri kiongezwe Kifungu cha 30(3) kitakachoweka masharti ya muda wa leseni ya kufundishia ya awali kuwa ni miaka mitatu (3).
- p) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 31** kinachohusu "*Renewal of practicing licence for teachers*" kinachoweka sharti la uhuishaji wa leseni ya kufundishia kwa mwalimu ambaye leseni imekwisha muda wake. Kamati inashauri kifutwe kwakuwa masharti yaliyowekwa yanafanana na masharti ya **Kifungu Cha 23** cha Sheria hii ambacho kinaainisha uhuishaji wa usajili ambapo Kamati imeshauri

masharti hayo yawe ya uhuishaji wa leseni na siyo usajili kwa kuwa usajili utafanyika mara moja na uhuishaji ni wa leseni za ufundishaji.

Aidha, katika Kifungu cha kutoa masharti ya uhuishaji wa leseni kiongeze masharti ya kuwa mwalimu awe amelipa ada zake, awe na cheti cha usajili pamoja na taarifa za kuwa amejiendeleza kitaaluma kwa kipindi cha matumizi ya leseni yake ya awali ya kufundishia ambayo inapendekezwa kuwa ya miaka mitano baada ya leseni ya awali ya miaka mitatu kuisha muda wake.

q) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 35** kinachohusu *"Removal of name from Register"* kinachoelezea sababu zitakazopelekea Bodi kufuta jina la mwalimu katika rejista ya Walimu. Kamati inashauri kwamba katika **Kifungu cha 35(e)** kufutwa kwakuwa mtu akifariki amefariki haina mbadala wake. Kwa mantiki hiyo Kamati inashauri kufuta **Kifungu cha 35(f)**.

r) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 45** kinachohusu *"Disobedience of summons and refusal to give evidence"* Kamati inashauri Serikali kwenda kukiangalia tena upya ili kuweka masharti ya Sheria hii kuweza kufanyiwa kazi. Kwakuwa masharti yake hayaedani na makosa yaliyoainishwa.

s) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha cha 50 kinachohusu "Appeal" Kifungu cha 50(2)** kinachoelezea masharti ya mwalimu ambaye hataridhishwa na uamuzi wa Waziri kupewa siku 30 za kukata rufaa Mahakama ya Rufaa. Ni maoni ya Kamati kwamba muda huo ni mchache ikizingatiwa miundombinu na maeneo mengi ya Walimu wanakofanya kazi inaweza kuleta changamoto kubwa ya Walimu hao kukosa haki yao ya msingi ya kuweza kukata rufaa. Ni maoni ya Kamati kwamba, Kifungu hicho kiainishe muda wa kukata rufaa kuwa ni **siku tisini (90)** yaani **miezi mitatu (3)** badala ya **siku thelathini 30 tu**. Kwa kufanya hivyo upande wa mlalamikaji atakuwa ametendewa haki ya kuweza kukata rufaa pale panapohitajika. Aidha, katika

Kifungu hicho kibainishe muda wa **siku arobaini na tano (45)** kwa Waziri mwenye dhamana kuweza kutoa majibu ya mwalimu aliyekata rufaa kwa kutoridhishwa na maamuzi ya Bodi.

t) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 52** kinachohusu "***Power to Borrow***" kinachoainisha Bodi kupewa mamlaka au uwezo wa kukopa fedha kama mkopo wa riba, ni maoni ya Kamati kwamba, Bodi imepewa mamlaka makubwa ya kukopa fedha hizo kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kamati inashauri kwamba, ili kutoa nafasi ya uwajibikaji na kulinda dhamana ya Bodi, basi mikopo hiyo lazima ipate idhini ya Waziri mwenye dhamana ya Elimu. Kwa kufanya hivyo pia, kutaongeza uwazi wa matumizi ya fedha zinazokopwa pamoja na ufuataji wa Sheria za kukopa kama ambavyo taasisi nyingine za Serikali zinafuata.

u) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 59** kinachohusu "***Offence for illegal practice***" kimeainisha makosa ya mwalimu anayefundisha bila kusajiliwa kwamba atakuwa anatenda makosa na adhabu yake imetajwa katika Kifungu hicho. Ni maoni ya Kamati kuwa, lionezwe neno "**or licence**" baada ya neno "**registered**" ili kuweka masharti ya mwalimu anayefundisha bila leseni kupata adhabu hiyo sawasawa na mwalimu anayefundisha bila ya kusajiliwa. Kwa kufanya hivyo Bodi itakuwa inaendelea kusimamia vyema taaluma ya ualimu hapa nchini kwa kuhakikisha walimu wote wanaofundisha wanafuata masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria hii.

v) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 60** kinachohusu "***Prohibition for unauthorized teacher***" kinachotoa katazo la mwalimu kufundisha bila ya kibali cha Bodi, ni maoni ya Kamati kuwa Kifungu hiki kinakaribia kuwa na ufanano wa maudhui na **Kifungu cha 29** kinachohusu "***Prohibition of teaching by unauthorized teacher***". Kamati inashauri kwamba, Serikali ikifanyie marekebisho Kifungu hiki ili kiwe Kifungu kimoja kinachotoa katazo pamoja na adhabu yake kwa mtu atakayekwenda kinyume na katazo hili.

- w) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 63** kuhusu "*Offences for a teacher who fails to obey summons*" kinachoainisha adhabu kwa mwalimu aliyeshindwa kutii wito wa kufika mbele ya Bodi na kutoa ushahidi na makosa mengine anayoweza kutenda mbele ya Bodi. Ni maoni ya Kamati kuwa, makosa hayo yaliyoainishwa na adhabu iliyowekwa kwa mwalimu atakayeshindwa kufuata masharti hayo ni vitu viwili ambavyo havina uwiano kwa maana ya kwamba adhabu ni kubwa ikilinganishwa na aina ya makosa tajwa. Kamati inashauri kufanya marekebisho ili kuweka uwiano katи ya makosa yaliyoainishwa na adhabu itakayotolewa ikibidi kupunguza adhabu husika kwa kuzingatia mazingira ya Walimu ambao watakuwa katika Bodi hiyo.
- x) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 64** kinachohusu "*General Offence and penalty*" kinaainisha adhabu itakayotolewa kwa mtu atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria hii na adhabu ya kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tatu au kifungo cha miaka mitano au vyote kwa pamoja. Ni maoni ya Kamati kwamba adhabu ya fedha haijaonesha ukomo kwakuwa imetamka kiasi si chini ya shilingi milioni tatu inaacha mwanya wa kulipa faini ya fedha zaidi ya iliyotajwa. Kamati inashauri kwamba Kifungu hiki kirekebishwe na kuainisha ukomo wa faini hiyo ili kuondoa utata na wakosaji wengine watakaonekana wanapendelewa au kuonewa kwa mujibu wa Sheria hii.
- y) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 68** kinachoainisha "*Codes of ethics*" ni maoni ya Kamati kuwa haiba ya mwalimu inategemeana na mazingira ya mwalimu anakofanya kazi au mwajiri wake ambapo kwa kuweka sharti hili Bodi itakuwa imejipa jukumu kubwa ambalo utekelezaji wake utakuwa ni changamoto. Kamati inashauri kuwa haiba hizi za mwalimu ziainishwe katika Kanuni baada ya Waziri kushauriana na wataaluma wa elimu kuhusu aina ya vigezo au aina ya haiba ziwekwe katika kanuni hizo badala ya kuoneshwa katika Sheria hii.
- z) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 70** kinachohusu "*Replacement certificates*" kianachoainisha utoaji wa cheti

kingine cha usajili baada ya kubainika na kuthibitika kwamba cheti cha usajili wa awali kimepotea. Ni maoni ya Kamati kuwa kwa mujibu ya neno "*replacement*" haiteti mantiki sahihi ya maana ya kupata cheti kingine cha usajili au leseni nyingine ya kufundishia. Kamati inashauri kubadili neno "*replacement*" na kuweka neno "*another*" ili kuonesha kwamba kutakuwa na utoaji wa nakala nyingine ya cheti au leseni ya kufundishia baada ya Bodi kujiridhisha nakala ya awali kupotea kwa utaratibu maalumu.

aa) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 72 kinachohusu "Regulations"** kwa maana ya Kanuni mbalimbali zitakazotungwa ili kusaidia utekelezaji wa Sheria hii, ni maoni ya Kamati kuwa iongezwe sharti la kuweka au kuipa Bodi jukumu la kuwaendeleza wanachama wake au walimu kitaaluma kama ambavyo ilivyo kwa Bodi nyingine kama za uhasibu, Bodi ya wakandarasi. Kwakufanya hivyo, kutawapa fursa walimu ya kuijendeleza kitaaluma kwakuwa katika **Kifungu Cha 31** moja ya kigezo cha kuhuisha leseni ya kufundishia ni pamoja na sifa ya kuijendeleza kitaaluma kwa kipindi cha matumizi ya leseni ya ufundishaji. Aidha, Walimu wataendelea kuipa hadhi taaluma yao na kuendelea kuonekana kuwa ni taaluma rasmi na inayotambulika hapa nchini.

bb) **Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 74 kinachohusu "Transitional provisional"** Ni maoni ya Kamati kuwa katika **Kifungu cha 74(2)** kinachoainisha muda wa kipindi cha mpito cha kuhakikisha kila mwalimu mwenye taaluma ya ualimu awe amejisajiliwa katika Bodi ndani ya **miezi 12** ambao ni mwaka mmoja tu. Ni maoni ya Kamati kuwa, muda huu ni mfupi sana kulingana na wingi wa wanataaluma ya ualimu pamoa na changamoto nyingine zinazowakabili.

Kamati inashauri Sheria itoe muda wa **miaka miwili (2)** ili kuwapa nafasi wanataaluma ya ualimu kujisajili lakini hata wale wanaokaribia kustaafu basi wasipate usumbufu wa kujisajili kwa muda mfupi. Kwa kufanya hivyo kutakuwa kumepatikana nafasi nzuri ya Walimu kujisajili kwa uhuru zaidi.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada huu wa Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Joyce Lazaro Ndalichako (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. William Tate Ole Nasha (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Ndg. Leonard Akwilapo, Naibu Katibu Mkuu Ndg. James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Ave Maria Semakafu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati na kuwasilisha vyema Muswada huu mbele ya Kamati pamoja na kutoa ufanuzi wa kina pale palipohitaji kufanya hivyo. Namshukuru pia MwanaSheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wake kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutoa mwongozo wa kitaalamu wa kiSheria wakati wote wa uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru tena Wadau wote waliofika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Aidha, nawashukuru pia Wadau ambao walishindwa kufika mbele ya Kamati kutokana na sababu mbalimbali lakini waliweza kutuma maoni kuhusu Muswada kwa Maandishi. Napenda kuwaeleza kuwa maoni yao yamesaidia kuboresha Muswada huu wa Sheria hii muhimu kwa Maslahi mapana ya Taaluma ya Ualimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipo mshukuru Makamu mwenyekiti wangu wa Kamati Mhe. Juma Selement Nkamia (Mb) na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri yenye umahiri katika uchambuzi wa Muswada huu. Wajumbe wamefanya kazi nzuri ya kuhakikisha uchambuzi wa Muswada unakuwa wenye tija kwa maslahi ya Taifa zima. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu

ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa majina kama ifuatavyo:-

1.Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb,	Mwenyekiti
2.Mhe. Juma S. Nkamia, Mb	M/ Mwenyekiti
3.Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb	Mjumbe
4.Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb	Mjumbe
5.Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb	Mjumbe
6.Mhe. Grace Victor Tendega, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Peter Ambrose Paciece Lijualikali, Mb	Mjumbe
8.Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Deogratius Francis Ngalawa, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
14. Mhe. John Peter Kadutu, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Maulid Said Mtulia, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Seleman Said Bungara, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
24. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb	Mjumbe
25. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe
26. Mhe. Khalifa M. Issa, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein na Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati Ndg. Dickson Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. Aidha, namshukuru Kaimu Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndg. Pius T. Mboya pamoja na wasaidizi

wake Ndg. Leorcard Kapongwa na Ndg. Rehema Kipera kwa Uchambuzi wa kisheria walioufanya kuisadia Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

Peter Joseph Serukamba, Mb
MWENYEKITI
5 Septemba, 2018

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa tupokee taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Susan Lyimo, hebu cheka kidogo basi. (*Kicheko*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani hapa Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Bodi ya Taaluma ya Walimu wa Mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama Waziri Kivuli wa Elimu, naomba pia nitumie fursa hii na kuwatataka kila la heri katika mitihani yao wanafunzi wote wa darasa la saba, zaidi ya laki tisa wanaokwenda kufanya mitihani yao katika mazingira magumu ya kukosa vitabu na vilevile kukosa Walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa katika Bunge hili wakati nachangia masuala mbalimbali kuhusu elimu, nimekuwa nikisisitiza mara kadhaa kwamba, hakuna elimu bila Mwalimu. Msisitizo huo haukulenga kuwa na idadi ya kutosha ya Walimu peke yake, bali ulilenga pia kuwa na Walimu walioendelezwa kitaaluma na kubobe katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, msisitizo huo ulilenga kuwa na Walimu wanaopata maslahi na stahiki zao kwa wakati ili wawe na motisha wa kufanya kazi kwa ufanisi. Mambo yote hayo kuhusu Walimu yakifanyiwa kazi vizuri kwa vyovoyote vile lazima viwango nya ubora wa elimu vitaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Serikali kuufahamu ukweli huo, bado kada ya ualimu imekuwa ikichukuliwa kama kada dhaifu na isiyopewa kipaumbele na Serikali. Uthibitisho wa jambo hili ni kuwepo kwa malalamiko na madai ya Walimu ya muda mrefu ambayo yamekuwa hayashughulikiwi ipasavyo na sasa madai hayo yamekuwa ni kama wimbo wa kawaida tu ambao ukiimbwa hakuna anayeshtuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaeleza mara nyingi miaka ya nyuma kwamba athari za Mwalimu mwenye kinyongo kutokana na kutopewa stahili zake ipasavyo ni mbaya sana kwa kuwa zinasambaa kwa vizazi vingine (*multiplier effect*) na zitaathiri sekta nyingi za uzalishaji. Walimu wakifanya mgomo baridi na kutofundisha ipasavyo hatuwezi kuona athari zake sasa; na pengine ndiyo maana Serikali inakuwa na ugumu wa kushtuka na kushughulikia kwa haraka madai yao lakini athari zake ni za muda mrefu na zinaweza kuonekana hata baada ya miaka kumi au ishirini mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mshangao wa Profesa Casmir Rubagumya, aliyekuwa Mkuu wa Chuo cha *Humanities and Social Sciences* (*Humanitia* na *Sayansi za Jamii*) katika Chuo Kikuu cha Dodoma kuhusu kuperomoka kwa elimu hasa elimu ya juu yamkini unatokana na makosa yaliyofanyika siku za nyuma za kutoshughulikia masuala ya Walimu katika ngazi za chini ambapo athari zake zinajitokeza wazi sasa kwa kushuka kwa ubora wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Rubagumya anathibitisha kwamba kiwango cha ubora wa elimu ya wanafunzi wanaojiunga na chuo kikuu unapungua kila

mwaka; na kila mwaka wanapokea wanafunzi dhaifu kuliko mwaka uliopita. Alishangazwa kwamba wanafunzi wanaojinga na elimu ya juu hawana uwezo wa kuzungumza Kiswahili au Kiingereza fasaha. Anaendelea kusema kwamba tatizo halikuwa tu kwenye lugha, bali pia uwezo mdogo wa kufikiri vizuri katika lugha zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, profesa huyu alibaini pia kwamba wanafunzi wa elimu ya juu walikuwa pia hawana uelewa wa mambo ya kawaida kuhusu Tanzania. Alishangazwa na kitendo cha mwanafunzi wa mwaka wa pili wa Chuo Kikuu cha Dodoma kushindwa kufahamu jina la Makamu wa Rais wa Tanzania, jambo ambalo hata mwanafunzi wa darasa la pili angetazamiwa kufahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Rubagumya anasema kwamba matatizo ya kielimu aliyoyagundua *UDOM*, aliyagundua pia kwa vyuo vingine vikuu vingine alivyokuwa anafanya kama mtahini wa nje (*external examiner*). Kwa maneno yake mwenyewe, anasema wanafunzi wa vyuo vikuu sasa hivi wanaonekana kutengeneza kizazi tofauti kisichopenda kabisa kujishughulisha na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi duni wa kada ya ualimu nchini; kumekuwa na usimamizi duni wa kada ya ualimu hususan maendeleo ya Walimu, jambo ambalo linayumbisha Sekta ya Slimu. Usimamizi huo duni unatokana na kukosekana kwa chombo kimoja chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala ya elimu yakiwemo maendeleo ya Walimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayohusu elimu na hususan madai ya Walimu yamekuwa yakishindwa kutatuliwa kikamilifu kutoptana na kuwepo kwa taasisi kadhaa zinazoshughulika na masuala ya Walimu, jambo ambalo linaleta mkanganyiko juu ya nani hasa mwenye mamlaka juu ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba zangu za miaka ya nyuma nilieleza kuwa ili kuondoa mkanganyiko uliopo kutokana na kuwepo kwa taasisi mbalimbali za kusimamia elimu yaani Wizara ya Elimu, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa wakati huo na sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; ni kuanzisha chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza ianzishwe Mamlaka ya Udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı Tanzania (*Tanzania Education and Training Regulatory Authority – TETRA*) ili masuala yote ya udhibiti wa utoaji wa elimu nchini pamoja na kushughulikia masuala ya elimu yatatuliwe na chombo kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa ushauri huo, Serikali ilianzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers' Service Commission*) badala ya mamlaka ya udhibiti kama ilivyopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani mapema kabisa wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Tume hiyo, ilisema kwamba tume hii ilianzishwa kukidhi maslahi ya kisasa yaliyolenga kupata kura za Walimu katika Uchaguzi Mkuu wa 2015, kwa ahadi kwamba matatizo ya Walimu yangekuwa historia kwa kuanzishwa kwa tume hiyo. Leo ni takriban miaka mitatu tangu Uchaguzi Mkuu ufanyike na tume hiyo kuundwa, lakini matatizo ya Walimu yamebaki palepale na hata kuongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Tume ya Utumishi wa Walimu hajasaidia hata kidogo kutatua kero za Walimu. Kwanza muundo wake una matatizo; ukitoka ngazi ya Taifa ambapo ndiyo makao makuu, tume hiyo ina matawi Wilayani tu huku mkoa ukiwa umeachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, licha ya tume hii kupewa hadhi ya mwajiri lakini haifanyi kazi za mwajiri. Majukumu ya mwajiri ni pamoja na kuajiri, kulipa mishahara, kupandisha madaraja, kufukuza na kadhalika. Katika

majukumu hayo ya mwajiri, Tume ya Utumishi wa Walimu haina mamlaka ya kuajiri wala kulipa mishahara, mwenye mamlaka hayo ni Mkurugenzi wa Halmashauri (*DED*); Tume ya Utumishi wa Walimu haina mamlaka ya kupandisha madaraja ya Walimu, mwenye mamlaka hayo ni Mkurugezi wa Halmashauri pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya msingi ambayo Walimu wamekuwa wakiyalalamikia siku zote ni kuhusu kupandishwa madaraja na kupandishwa mishahara, mambo ambayo Tume ya Utumishi wa Walimu haina mamlaka nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti aidha, madai ya siku nyingi ya Walimu ni kuwa na chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala yao, lakini badala ya Serikali kukidhi hitaji hilo, inazidi kuongeza vyombo na taasisi za kushughulikia masuala ya Walimu. Ikiwa sheria hii itapita basi masuala ya Walimu yatakuwa yanashughulikiwa na taasisi sita zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu; Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Halmashauri za Wilaya; Manispaa na Majiji; Tume ya Utumishi ya Walimu; na sasa Bodi ya Kitaaluma ya Walimu Tanzania. Hii ni kwamba hakuna kada nyingine yoyote nchini zaidi ya Walimu inayoshughulikiwa na taasisi au vyombo kama Walimu yaani vyombo sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu mapendelekezo ya Muswada huu ni kwamba chimbuko na madhumuni ya kuletwa kwa Muswada huu ni utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Mawaziri katika Waraka Na. 14/2011/12 na Waraka Na. 10/2013/14 kuwa iundwe Bodi ya Taaluma ya Walimu itakayosimamia masuala ya usajili, weledi na maadili ya ualimu na Walimu katika Sekta ya Umma na Binafsi; lengo likiwa ni kutungwa kwa Sheria ya kuanzisha Bodi ya Taaluma ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli maagizo ya Baraza la Mawaziri ndiyo sababu ya msingi ya kuleta Muswada huu na siyo kwamba kulikuwa na tatizo la msingi katika taaluma za Walimu, basi kuna tatizo kubwa katika utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la kitaalam kwamba kabla ya kuanzisha sera au sheria ni lazima kuwe na tatizo la msingi katika jamii linalopelekea mahitaji ya kuanzishwa kwa sera au sheria hiyo. Sidhani kama maagizo ya Baraza la Mawaziri ndiyo *Problem Statement* inayopelekea mahitaji ya kutungwa kwa sheria hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kuhusu uhitaji wa kuanzishwa kwa sheria hii ni kwamba idadi ya Walimu imeongezeka sana na kutokana na idadi kubwa ya Walimu kumekuwepo na changamoto nyingi zinazohitaji kuwa na mfumo thabitii wa usimamizi wa ubora wa Walimu na taaluma ya ualimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa na kauli hii ya Waziri kwamba idadi ya Walimu ni kubwa sana na kwamba kutokana na idadi hiyo inabidi kuwatungia sheria ya kuwadhibiti. Kwa takwimuza Serikali hii hii, Serikali imekiri kwamba kuna upungufu mkubwa wa Walimu lakini kwa kuwa leo inataka kupitisha jambo lake na haina sababu nyingine ya msingi, imeona isingizie kwamba Walimu ni wengi hivyo wadhibitiwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za *BEST (Basic Education Statistics in Tanzania)* za mwaka 2016 na 2017, hizi ni takwimu za Serikali, idadi ya Walimu kwa shule za msingi imeshuka kutoka Walimu 191,772 mwaka 2016 hadi kufikia 179,291 mwaka 2017, ikiwa ni anguko la asilimia 6.5 na kufanya uwiano wa Mwalimu na wanafunzi kuwa 1:50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika shule za awali, idadi iliyopungua ni Walimu 1,948 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuongezeka kutoka 1:135 (Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 135) mwaka 2016 hadi kufikia mwalimu mmoja kwa wanafunzi 159 mwaka 2017 badala ya ule uwiano tunaoutegemea wa 1:25 ambao ni uwiano unaokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za sekondari kuna uhaba mkubwa wa Walimu kwa baadhi ya masomo kama ifuatavyo; Hisabati, kuna upungufu wa Walimu 7,291; Baiolojia, kuna upungufu wa Walimu 5,181; Kemia, kuna upungufu wa Walimu takribani 5,373; Fizikia, kuna upungufu wa Walimu 6,873.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Elimu Msingi za Mikoa (*BEST Regional Data, 2017*); Wallimu 7,743 wanatarajiwa kustaafu kati ya mwaka 2018 na 2019. Aidha, takriban Walimu zaidi ya 30,000 wana umri wa zaidi ya miaka 51 ya kuzaliwa; hivyo na wao wanatarajiwa kustaafu muda mfupi ujao. Kwa hiyo, hoja kwamba Walimu ni wengi si sahihi, kwa kuwa kimsingi Serikali haina sababu za msingi za kuleta Muswada huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama kweli Walimu wangkuwa wengi; idadi yao inaathiri vipi taaluma zao? Hoja ingekuwa kwamba imethibitika kuwa kuna Walimu wengi wenye vyeti feki au vya kughushi wasio na sifa za kufundisha au imebainika kwamba maadili ya Walimu yameporomoka, kungekuwa na sababu ya msingi ya kuunda chombo cha kudhibiti ubora wa taaluma zao na maadili yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine iliyotolewa ni kuzingatia Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuia ya Afrika Mashariki inayosisitiza nchi wanachama kuwianisha na kutambua sifa za kitaaluma na kitaalam (*Mutual Recognition of Academic and Professional Qualifications*) ili wenye sifa hizo waweze kufanya kazi kwa uhuru katika nchi wanachama bila vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, itifaki hiyo inakwenda sambamba na mwelekeo wa usimamizi wa taaluma mbalimbali duniani ambapo kunatakiwa kuwe na vyombo huru kisheria vya kusimamia, kudhibiti na kuendeleza taaluma husika (*Regulatory Authorities*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina mgogoro na sababu hii kwa kuwa ndiyo hoja ya msingi ambayo Kambi ilikuwa ikiisimamia miaka mingi iliopita, kwamba tuwe na chombo kimoja tu cha kudhibiti ubora wa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unavyoongeza ukubwa na matumizi ya Serikali; Muswada huu unaanzisha Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania. Hiki ni chombo kipyaa katika muundo wa Serikali na taasisi zake. Kimeongeza idadi ya taasisi za Serikali. Ni chombo kitakachokuwa na viongozi na Watendaji Wakuu na watakuwa na shughuli mbalimbali za kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ni wazi kuwa itahitajika bajeti ambayo hapo awali kabla ya kuundwa kwa chombo hicho haikuwepo. Kwa maneno mengine, kutakuwa na ongezeko la matumizi ya Serikali katika kukiendesha chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Serikali hii hii ya Awamu ya Tano iliojipambanua kwamba inabana matumizi ili kuelekeza fedha zinazopatikana kwa kubana matumizi kwenye miradi ya maendeleo. Ili kutekeleza azma hii, Serikali ilianza kudhibiti malipo hewa na kuwatumbua watumishi wa umma kutohana na sababu mbalimbali, kufuta safari za nje na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ilidhani zoezi hilo lingeenda sambamba na kupunguza ukubwa wa Serikali kwa kupunguza maeneo ya kiutawala

kama vile wilaya na mikoa na taasisi za Serikali zenyе majukumu yanayokaribia kufanana ili kuipa dhana ya kubana matumizi uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, cha ajabu imeanzishwa taasisi mpya kama hii Bodi ya Kitaaluma ya Walimu ambayo majukumu yake kwa kiwango kikubwa yanafanana na Tume ya Utumishi wa Umma isipokuwa tu hapa wanaongeza walimu kutoka shule binafsi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ilidhani ingekuwa busara kuifanyia marekebisho Sheria ile ya Tume ya Utumishi wa Umma (*Tanzania Teacher's Commission*) ili kuipa Tume ya Utumishi wa Walimu mamlaka ya kudhibiti ubora wa taaluma za Walimu badala ya kuanzisha chombo kipyä kinachoongeza ukubwa na kuongeza matumizi ya Serikali. Haya pia yalikuwa ndiyo maoni ya Chama cha Walimu na pia ya Walimu binafsi pamoja na Chama cha Kutetea Haki za Walimu Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si jambo la kubishaniwa kwamba mishahara ya Walimu ni midogo ndiyo maana malalamiko kuhusu kupandishwa madaraja na mishahara yamekuwa endelevu. Pamoja na mishahara yao kuwa midogo wana makato mengi ya fedha kutoka kwenye mishahara hiyo hiyo midogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani kodi ya mapato (*pay as you earn*) ambapo wanakatwa asilimia tisa ya mshahara, makato ya marejesho ya mkopo wa elimu ya juu kwa wale ambao wamepitia vyuo vikuu na kukatwa mikopo, wanakatwa asilimia 15 ya mshahara. Licha ya makato hayo bado wana changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutopewa posho za kufundishia, posho za makazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendelezo la Muswada wa sheria hii pia itawakata tena ada ya cheti cha usajili kwenye Bodi kila mwaka au itakavyopangwa kutohuna na kanuni na ada ya leseni ya kufundishia. Hii ni kuwafanya walimu waendelee kuwa duni kiuchumi, lakini pia kuwavunja moyo na kuwaondolea morali wa kufundisha. Muswada huu umelenga kuwadhibiti Walimu badala ya kuwaendeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Muswada huu umetilia mkazo sana kwenye kuwadhibiti na kuwaadhibu walimu pindi wanapokosea katika kutekeleza majukumu yao. Muswada haujazungumzia namna ya kuwapa walimu ushauri nasaha pindi wanapokuwa na msongo wa mawazo au matatizo yanayoweza kupelekea kushuka kwa weledi wao. Muswada umejaa orodha ndefu ya makatazo, makosa na adhabu kwa mwalimu anayetenda kosa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina maana kwamba walimu wasichukuliwe hatua za kinidhamu wanapofanya makosa, isipokuwa tunataka kuona pia mkakati wa kuwarekebisha walimu wafanye kazi yao kwa kuzingatia maadili yao kwa mfumo rafiki na siyo huu wa kipolisi na kimahakama unaopendekezwa na sheria hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, himitisho, kama nilivyosema hapo awali hakuna elimu bila mwalimu. Kwa sababu hii ni lazima kuwajengea walimu mazingira rafiki ya kufanya kazi kwa kuwaendeleza kitaaluma na kuwapa motisha kwa masilahi na stahili nytingine ili waweze kuwa na ufanisi katika kazi zao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuwa na chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala ya walimu ikiwa ni pamoja na kudhibiti ubora wa taaluma zao, lakini pia kushughulikia masilahi yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono maoni ya baadhi ya wadau wa elimu kwamba kuendelea kuongeza idadi ya sheria za kuwadhibiti, kuwaadhibu, kuwakandamiza na kuwapa walimu maisha ya utumishi yaliyojaa fadhaa (*stress*) au

msongo wa mawazo hakutaongeza ufanisi wa walimu bali kutaendelea kuwavunja moyo na kudidimiza hari yao ya kufanya kazi. Hii ni kwa sababu sheria hizi zinatambua wajibu wa walimu lakini hazitambui nafasi ya mwajiri kutoa kwa hiari yake haki na masilahi bora kwa walimu katika utumishi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu nilioubaini katika Muswada huu, nimewasilisha Jedwali la Marekebisho ili kurekebisha baadhi ya vifungu kwa hatua ya sasa, tukiendelea na msimamo wa kuitaka Serikali kupunguza utitiri wa vyombo na taasisi zinazoshughulikia masuala ya walimu na kubaki na chombo kimoja tu kwa ajili hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha. Nakushukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa taarifa yenu. Naomba utulivu.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA
NA UFUNDI MHESHIMIWA SUSAN ANSELIM JEROME LYIMO
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA BODI YA
TAALUMA YA WALIMU TANZANIA, 2018 (THE TANZANIA
TEACHERS' PROFESSIONAL BOARD ACT, 2018) KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Bodi ya Taaluma ya Walimu ya mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa katika bunge hili wakati nikichangia masuala mbalimbali kuhusu elimu, nimekuwa nikisisitiza mara kadhaa kwamba, hakuna elimu bila mwalimu. Msisitizo huo haukulenga kuwa na idadi ya kutosha ya walimu peke yake, bali ulilenga pia kuwa na walimu walioendelezwa kitaaluma na kuboea katika fani mbalimbali. Aidha, msisitizo huo ulilenga kuwa na walimu wanaopata maslahi na stahiki zao kwa wakati ili wawe na motisha wa kufanya kazi kwa ufanisi. Mambo yote hayo kuhusu walimu yakifanyiwa kazi vizuri kwa vyovyyote vile lazima viwango vya ubora wa elimu vitaongezeka.

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kuufahamu ukweli huo, bado kada ya ualimu imekuwa ikichukuliwa kama kada dhaifu na isiyopewa kipaumbele na Serikali. Na uthibitisho wa jambo hili ni kuwepo kwa malalamiko na madai ya walimu ya muda mrefu ambayo yamekuwa hayashughulikiwi ipasavyo na sasa madai hayo yamekuwa ni kama wimbo wa kawaida tu ambao ukiimbwa hakuna anayeshtuka.

Mheshimiwa Spika, nilishaeleza mara nyngi miaka ya nyuma kwamba athari za mwalimu mwenye kinyongo kutokana na kutopewa stahili zake ipasavyo ni mbaya sana kwa kuwa zinasambaa kwa vizazi vingi (multiplier effect) na zinaathiri sekta nyngi za uzalishaji. Walimu wakifanya mgomo baridi na kutofundisha ipasavyo hatuwezi kuona athari zake sasa; na pengine ndio maana Serikali inakuwa na ugumu wa kushtuka na kushughulikia kwa haraka madai yao lakini athari zake ni za muda mrefu na zinaweza kuonekana hata baada ya miaka kumi au ishirini mbele.

Mheshimiwa Spika, mshangao wa Profesa Casmir Rubagumya, aliyekuwa Mkuu wa Chuo cha Humanitia na Sayansi za Jamii katika Chuo Kikuu cha Dodoma kuhusu kuporomoka kwa elimu hasa elimu ya juu yamkini unatokana na makosa yaliyofanyika siku za nyuma za kutoshughulikia masuala ya walimu katika ngazi za chini ambapo athari zake zinajitokeza wazi sasa kwa kushuka kwa ubora wa elimu ya juu. Profesa Rubagumya anathibitisha kwamba kiwango cha ubora wa elimu ya wanafunzi wanaojiunga na chuo

kikuu unapungua kila mwaka; na kila mwaka wanapokea wanafunzi dhaifu kuliko mwaka uliopita. Alishangazwa kwamba; wanafunzi wanaojunga na elimu ya juu hawana uwezo wa kuzungumza Kiswahili au Kiingereza fasaha. Anaeleza kwamba tatizo halikuwa tu kwenye lugha, bali pia uwezo mdogo wa kufikiri vizuri katika lugha zote mbili.

Mheshimiwa Spika, Profesa alibaini pia kwamba wanafunzi wa elimu ya juu walikuwa pia hawana uelewa wa mambo ya kawaida kuhusu Tanzania. Alishangazwa na kitendo cha mwanafunzi wa mwaka wa pili chuo kikuu kushindwa kufahamu jina la Makamu wa Rais wa Tanzania; jambo ambalo hata mwanafunzi wa darasa la pili angetazamiwa kufahamu.

Mheshimiwa Spika, Profesa Rubagumya anasema matatizo ya kielimu aliyoagundua UDOM, aliyagundua pia kwa vyuo vingine vikuu alipokuwa kama mtahini wa nje (external examiner) katika vyuo hivyo. Kwa maneno yake mwenyewe, anasema wanafunzi wa vyuo vikuu sasa hivi wanaonekana kutengeneza kizazi tofauti kisichopenda kabisa kujishughulisha na elimu.

2. USIMAMIZI DUNI WA KADA YA UALIMU NCHINI

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na usimamizi duni wa kada ya ualimu hususan maendeleo ya walimu jambo ambalo linayumbisha sekta ya elimu. Usimamizi huo duni unatokana na kukosekana kwa chombo kimoja chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala ya elimu yakiwemo maendeleo ya walimu nchini. Matatizo yanayohusu elimu na hususan madai ya walimu yamekuwa yakishindwa kutatuliwa kikamilifu kutokana na kuwepo kwa taasisi kadhaa zinazoshughulika na masuala ya walimu jambo ambalo linaleta mkanganyiko juu ya nani hasa mwenye mamlaka juu ya walimu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba zangu za miaka ya nyuma nilieleza kuwa ili kuondoa mkanganyiko uliopo kutokana na kuwepo kwa taasisi mbali mbali za kusimamia

elimu – yaani Wizara ya Elimu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kwa wakati huo na sasa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma; ni kuanzisha chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala hayo. Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza ianzishwe Mamlaka ya Udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı (Tanzania Education and Training Regularity Authority – TETRA) ili masuala yote ya udhibiti wa utoaji wa elimu pamoja na kushughulikia masuala ya walimu yaratibиwe na chombo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa ushauri huo, Serikali ilianzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (Teachers' Service Commission) badala ya mamlaka ya udhibiti kama ilivyopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani mapema kabisa wakati wa kujadili muswada wa sheria ya kuanzisha tume hiyo, ilisema kwamba Tume hii ilianzishwa kukidhi maslahi ya kisiasa yaliyolenga kupata kura za walimu katika Uchaguzi Mkuu wa 2015, kwa ahadi kwamba, matatizo ya walimu yangekuwa historia kwa kuanzishwa kwa tume hiyo. Leo ni takriban mitatu tangu Uchaguzi Mkuu ufanyike, lakini matatizo ya walimu yamebakı pale pale na katika maeneo mengine yameongezeka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Tume ya Utumishi wa Walimu haijasaidia hata kidogo kutatua kero za walimu. Kwanza muundo wake una matatizo. Ukitoka ngazi ya Taifa (Makao Makuu) tume hiyo ina matawi Wilayani tu. Hakuna matawi ngazi ya Mkoa. Matokeo yake, ngazi ya Taifa inazidiwa na kazi kwa kuwa hakuna ngazi ya mkoa ambayo ingeweza kuchambua matatizo ya walimu katika mkoa husika na kuwasilisha taifani.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, licha ya tume hii kupewa hadhi ya mwajiri lakini haifanyi kazi za mwajiri. Majukumu ya mwajiri ni pamoja na kuajiri, kulipa mishahara, kupandisha madaraja, kufukuza n.k. Katika majukumu hayo ya mwajiri; Tume ya Utumishi wa Walimu haina mamlaka ya kuajiri wala kulipa mishahara – mwenye mamlaka hayo ni

Mkurugenzi wa Halmashauri (DED); Tume ya Utumishi wa Walimu haina mamlaka ya kupandisha madaraja ya walimu – mwenye mamlaka hayo ni Mkurugezi wa Halmashauri pia.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya msingi ambayo walimu wamekuwa wakiyalalamikia siku zote ni kuhusu kupandishwa madaraja na kupandishwa mishahara mambo ambayo tume ya utumishi wa walimu haina mamlaka nayo. Aidha, madai ya siku nyingi ya walimu ni kuwa na chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala yao; lakini badala ya Serikali kukidhi hitaji hilo, inazidi kuongeza vyombo na taasisi za kushughulikia masuala ya walimu. Ikiwa sheria hii itapita basi masuala ya walimu yatakuwa yanashughulikiwa na taasisi sita zifuatazo:- Wizara ya Elimu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji, Tume ya Utumishi ya Walimu, na Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania.

3. UCHAMBUZI WA MUSWADA WA SHERIA YA BODI YA KITAALAM YA WALIMU

3.1. Chimbuko na Sababu za Kuletwa kwa Muswada

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundu kuhusu mapendelekezo ya Muswada ni kwamba chimbuko na madhumuni ya kuletwa kwa muswada huu ni utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Mawaziri katika waraka Na. 14/ 2011-12 na waraka Na. 10/2013-14 kuwa iundwe Bodi ya Taaluma ya Walimu itakayosimamia masuala ya usajili, weledi na maadili ya ualimu na walimu katika sekta ya umma na binafsi; lengo likiwa ni kutungwa kwa sheria ya kuanzisha Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama kweli maagizo ya Baraza la Mawaziri ndiyo sababu ya msingi ya kuleta muswada huu na sio kwamba kulikuwa na tatizo la msingi katika taaluma za walimu, basi kuna tatizo kubwa katika utendaji wa Serikali hii. Ni suala la kitaalam kwamba kabla ya kuanzisha sera au

sheria ni lazima kuwe na tatizo la msingi katika jamii linalopelekea mahitaji ya kuanzishwa kwa sera au sheria hiyo. Sidhani kama maagizo ya Baraza la Mawaziri ndiyo ‘Problem Statement’ inayopelekea mahitaji ya kutungwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine iliyotolewa na Waziri kuhusu uhitaji wa kuanzishwa kwa sheria hii ni kwamba idadi ya walimu imeongezeka sana, na kutokana na idadi kubwa ya walimu kumekuwepo na changamoto nyingi zinazohitaji kuwa na mfumo thabiti wa usimamizi wa ubora wa walimu na taaluma ya ualimu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwanza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa na kauli hii ya Waziri kwamba **idadi ya walimu ni kubwa** na kwamba kutokana na idadi hiyo inabidi kuwatungia sheria ya kuwadhibiti. Kwa takwimu za Serikali hii, Serikali imekiria kwamba kuna upungufu wa walimu lakini kwa kuwa leo inataka kupitisha jambo lake na haina sababu za msingi, imeona isingizie kwamba walimu ni wengi hivyo wadhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za BEST za mwaka 2016 na 2017; (hizi ni takwimu za Serikali!) idadi ya walimu kwa shule za msingi imeshuka kutoka walimu 191,772 mwaka 2016 hadi kufikia 179,291 mwaka 2017 ikiwa ni anguko la asilimia 6.5 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuwa 1:50. Aidha, katika shule za awali, idadi iliopungua ni walimu 1948 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuongezeka kutoka 1:135 mwaka 2016 hadi kufikia 1:159 mwaka 2017 badala ya 1:25 ambao ni uwiano unaokubalika.

Mheshimiwa Spika, katika shule za Sekondari kuna uhaba mkubwa wa walimu kwa baadhi ya masomo kama ifuatavyo:

- i. Hisabati – kuna upungufu wa walimu 7,291
- ii. Baiolojia – kuna upungufu wa walimu 5,181
- iii. Kemia – kuna upungufu wa walimu 5,373

iv. Fizikia – kuna upungufu wa walimu 6,873 (Hii ni kwa mujibu wa takwimu za BEST, 2016)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Elimu Msingi za Mikoa (BEST Regional Data, 2017); walimu 7,743 wanatarajiwa kustaafu katika mwaka 2018 na 2019. Aidha, takriban walimu zaidi ya 30,000 wana umri wa zaidi ya miaka 51 ya kuzaliwa; hivyo na wao wanatarajiwa kustaafu muda mfupi ujao. Kwa hiyo hoja kwamba walimu ni wengi si sahihi, kwa kuwa kimsingi haina sababu za msingi za kuleta muswada huu.

Mheshimiwa Spika, hata kama kweli walimu wangekuwa wengi; idadi yao inaathiri vipi taaluma zao? Hoja ingekuwa kwamba imethibitika kuna walimu wengi wenye vyeti nya kughushi wasio na sifa za kufundisha au imebainika kwamba maadili ya walimu yameporomoka, kungekuwa na sababu ya msingi ya kuunda chombo cha kuthibiti ubora wa taaluma zao na maadili yao.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine iliyotolewa ni kuzingatia Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuia ya Afrika Mashariki inayositisiza nchi wanachama kuwianisha na kutambua sifa za kitaaluma na kitaalamu (Mutual Recognition of Academic and Professional Qualifications) ili wenye sifa hizo waweze kufanya kazi kwa uhuru katika nchi wanachama bila vikwazo. Aidha, itifaki hiyo inakwenda sambamba na mwelekeo wa usimamizi wa taaluma mbalimbali duniani ambapo kunatakiwa kuwe na vyombo huru kisheria nya kusimamia, kuthibiti na kuendeleza taaluma husika (Regulatory Authorities).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina mgogoro na sababu hii kwa kuwa ndiyo hoja ya msingi ambayo Kambi ilikuwa ikiisimamia miaka mingi iliyopita kwamba tuwe na chombo kimoja cha kudhibiti ubora wa elimu.

3.2. Muswada unavyoongeza Ukubwa na Matumizi ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaanzisha Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania. Hiki ni chombo kipyä katika muundo wa Serikali na taasisi zake. Kimeongeza idadi ya taasisi za Serikali. Ni chombo kitakachokuwa na viongozi na watendaji na shughuli mbalimbali za kufanya. Ni wazi kuwa itahitajika bajeti ambayo hapo awali kabla ya kuundwa kwa chombo hicho haikuwepo. Kwa maneno mengine, kutakuwa na ongezeko la matumizi ya Serikali katika kukiendesha chombo hicho.

Mheshimiwa Spika, ni Serikali hii hii ya awamu ya tano iliyojipambanua kwamba inabana matumizi ili kuelekeza fedha zilizopatikana kwa kubana matumizi kwenye miradi ya maendeleo. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali illanza kudhibiti malipo hewa na kuwatumbua watumishi wa umma kutokana na sababu mbalimbali; kufuta safari za nje nk. Kambi Rasmi ya Upinzani ilidhani zoezi hilo lingeenda sambamba na kupunguza ukubwa wa Serikali kwa kupunguza maeneo ya kiutawala kama vile wilaya na mikoa na taasisi za Serikali zenyé majukumu yanayokaribia kufanana ili kuipa dhana ya kubana matumizi uhalisia. Lakini cha ajabu imeanzishwa taasisi mpya kama hii Bodi ya Kitaaluma ya Walimu ambayo majukumu yake kwa kiwango kikubwa yanafanana na Tume ya Utumishi wa Walimu. Kambi Rasmi ya Upinzani ilidhani ingekuwa busara kuifanyia marekebisho ile sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu ya 2015 ili kuipa Tume ya Utumishi wa Walimu mamlaka ya kudhibiti ubora wa taaluma za walimu badala ya kuanzisha chombo kipyä kinachoongeza ukubwa Serikali na hivyo kuongeza matumizi ya Serikali.

3.3. Muswada unavyoongeza Mzigo wa Michango kwa Walimu

Mheshimiwa Spika, si jambo la kubishaniwa kwamba mishahara ya walimu ni midogo; ndiyo maana malalamiko yao kuhusu kupandishwa madaraja na mishahara yamekuwa

endelevu. Pamoja na mishahara yao kuwa midogo wana makato mengi ya fedha kutoka kuwenye mshahara huohuo mdogo. Mathalani kodi ya mapato (pay as you earn) ambapo wanakatwa asilimia 9 ya mshahara, makato ya marejesho ya mkopo wa elimu ya juu wanakatwa asilimia 15 ya mshahara. Licha ya makato hayo bado wana changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutopewa posho ya kufundishia, posho ya makazi nk.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la muswada wa sheria hii kuwakata tena ada ya cheti cha usajili kwenye Bodi kila mwaka na ada ya leseni ya kufundishia kila mwaka ni kuwfafanya walimu waendelee kuwa duni kiuchumi lakini pia ni kuwavunja moyo na kuwaondolea morali wa kufundisha.

3.4. Muswada umelenga Kuwadhibiti Walimu badala ya kuwaendeleza

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla muswada umetilia mkazo sana kwenye kuwadhibiti na kuwaadhibu walimu pindi wanapokosea katika kutekeleza majukumu yao. Muswada haujazungumzia namna ya kuwapa walimu ushauri nasaha pindi wanapokuwa na msongo wa mawazo au matatizo yanayoweza kupelekeea kushuka kwa weledi wao. Muswada umejaa orodha ndefu ya makatazo, makosa na adhabu kwa mwalimu atakayetenda kosa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina maana kwamba walimu wasichukuliwe hatua za kinidhamu wanapofanya makosa; isipokuwa tunataka kuona pia na mkakati wa kuwarekebisha walimu wafanye kazi yao kwa kuzingatia maadili yao kwa mfumo rafiki na sio huu wa kipolisi na kimahakama unapendekezwa na sheria hii.

4. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, hakuna elimu bila mwalimu. Kwa sababu hiyo, ni lazima kuwajenjea walimu mazingira rafiki ya kufanya kazi kwa kuwaendeleza

kitaaluma na kuwapa motisha wa maslahi na stahili nyingine ili waweze kuwa na ufanisi katika kazi yao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuwa na chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala ya walimu ikiwa ni pamoja na kuthibiti ubora wa taaluma zao lakini pia kushughulikia maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono maoni ya baadhi ya wadau wa elimu kwamba kuendelea kuongeza idadi ya sheria za kuwadhibiti, kuwaadhibu, kuwakandamiza na kuwapa walimu maisha ya utumishi yaliyojaa fadhaa (stress) hakutaongeza ufanisi wa walimu bali kutaendelea kuwavunja moyo na kudidimiza ari yao ya kufanya kazi. Hii ni kwa sababu sheria hizi zinatambua wajibu wa walimu lakini hazitambui nafasi ya mwajiri kutoa kwa hiari haki na maslahi bora ya walimu katika utumishi wao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapungufu niliyoyabaini katika Muswada huu; nimewasilisha jedwali la marekebisho ili kurekebisha baadhi ya vifungu kwa hatua ya sasa lakini tukiendelea na msimamo wa kuitaka Serikali kupunguza utitiri wa vyombo na taasisi zinazoshughulikia masuala ya walimu na kubaki na chombo kimoja kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Susan Anselm Jerome Lyimo (Mb)
**WAZIRI KIVULI NA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI
YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU,
SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
5 Septemba, 2018

MWENYEKITI: Hoja hii sasa naitoa kwenu muiamue kwa hatua ya kwanza ya kuiboresha kwa michango. Tuna hizi taarifa mbili; ya Kamati na hii ya upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Sasa nianze na orodha ya wachangiaji hapa. Nianze na Mheshimiwa Anatropia Theonest, atafuatiwa na Mheshimiwa Othman Omar Haji na Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae. Niseme wazi, naendeleza ya jana, uchangiaji ni dakika kumi.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Nampongeza Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuwasilisha vyema, hitaji la walimu siyo utitiri wa taasisi za kudhibiti bali chombo cha kuwasaidia. Walimu kama taasisi wamekuwa na malalamiko siku yingi. Kada ya walimu imeonekana ni kada illyodharaulika na kusaulika. Kama haitoshi wale wanaofeli katika hatua mbalimbali wamekuwa wakisokomezwa kwenye ualimu. Sasa tunataka tuone, je, hii taasisi italeta mabadiliko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada uliyowasilishwa na Serikali, nimepitia vipengele tofauti tofauti, nikianza na *composition* ya Bodi, muundo wa Bodi unaopendekezwa katika kifungu cha 5 kwa kiwango kikubwa naona unampa Waziri mamlaka mengi sana ya kuteua. Ukitoka Muswada, unaona maeneo mengi sana Waziri anateua. Anaanza kumteua Mwenyekiti wa Bodi, anatoka anawateua wajumbe nane wanaopatikana katika kifungu cha 5(1)(b) katika maeneo tofauti tofauti, anatoka hapo, anakuja kuteua wasaidizi au wasimamizi wa walimu katika Wilaya na Mikoa, hiyo ni kifungu cha 14, wote huo ni uteuzi wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona hapa kinachofanyika ni mawazo ya Waziri atakayekuwa anamwona anafaa, tutaenda kuwa na *composition* ya Bodi ya maoni ya Waziri. Badala yake napendekeza kama ikionekana inafaa, watu wenye vigezo wajitokeze *senior professional teachers wagombee* hizo nafasi *among the*

contenders ndiyo Waziri aweze kuteua mmojawapo. Sababu kubwa ya kuteua sidhani kama ni bahati mbaya, ni kwa ajili kuteua watu wenyewe mrengo fulani fulani wanaoutaka watu fulani. Hilo ni pendekezo langu la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, uteuzi mwingine ni *appointment of the Registrar* ambaye ndiye atakuwa *CEO* wa Bodi na *Deputy Registrar*, wote huo ni uteuzi wa Waziri. Huu ni upungufu mkubwa sana kumchukulia Waziri kama Mungu. Hiyo ndiyo tunayoiona leo ya Mheshimiwa Jiwe ambaye anaweza kumteua kila mtu kuanzia juu mpaka chini. Naona tusiendeleze haya mambo ya kumruhusu mtu mmoja atutengenezee anachohisi anaweza kufanya. Badala yake tuwaache walimu wenyewe uwezo waweze kujitokeza na wateuliwe kushika nafasi katika Bodi yao kwa maana wao ndiyo wana maono ya namna ya kuendesha chombo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Muswada sijaona uhusiano wa hii Bodi ya Walimu na Chama cha Walimu kilichokuwepo na badala yake kuna *representative* kutoka kwenye *professional*, anasema kuna mwakilishi mmoja kutoka kwenye Chama cha Walimu ambaye naye ni mmoja wa watu watakaoeuliwa na Waziri. Nadhani hiyo tuiangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nitapenda kuongelea ni ada za usajili. Wote tunatambua kwamba walimu wanalipwa kiwango kidogo cha fedha. Kwa hiyo, tuangalie hata ada ambazo tunaziweka kama sifa mojawapo ya kuwapa usajili ziwe katika *minimal stage* au ikiwezekana hata isiwepo ili mradi ana vigezo vingine vya msingi siyo lazima alipe, *otherwise* mtuambie kuanzishwa kwa Bodi husika kunaenda sambamba na kuongeza kipato au mishahara ya walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nitapenda nilizungumzie kutoka kwenye huu Muswada linapatikana katika *section 23*. Masharti yanayoongezeka kwa mwalimu ku-*renew license* au *certificate*. Naenda *page* ya 12 ambapo namwona mwalimu ameshasajiliwa, amepewa leseni lakini katika ku-*renew* leseni unamwona

anahitajika *a-submit performance appraisal*, *a-submit* tena kuonyesha amejiendeleza kwa kiwango gani na fedha ya usajili. Hapa nachokiona ni likwazo kingine cha pili, hii inamaanisha mwalimu anasajiliwa mara mbili. Kwa nini wakati wakati wa *ku-renew* leseni isiwe ni kupewa tu leseni badala ya kuwa na masharti mengine mapya ambayo naona mnajaribu kuyatengeneza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho nimekipitia ni cha 28 kuhusu mtu ambaye siyo Mtanzania kusajiliwa na Bodi. Tuna-*assume* kwamba nchi nyingine zinazotuzunguka zitakuwa na chombo cha *ku-certify* walimu. Nadhani ni upungufu, ni lazima kama tunatengeneza Bodi, basi iwe hata na *minimum qualification* ya kutazama wale watu wanaokuja kufundisha hapa nchini badala ya kutegemea kwamba waje na *recommendation* kutoka kwenye taasisi za nchini kwao ambazo zimewa-*recommend*. Nashauri tutengeneze mfumo wa kuwatambua wale walimu na kuwaweka kwenye *system* waweze kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni *code of ethics* or *code of conduct*, nadhani hata Kamati wameisemea. *This is general*, sitegemei Bodi ikae na kusema hii ni sahihi au hii siyo sahihi. Sitegemei kama wao wana kitu kinaitwa *criteria of truth* au namna ya kuwa-*Judge* walimu na badala yake uwepo mjadala wa Kitaifa wa ipi miiko sahihi kwa mwalimu? *Otherwise* viwe vitu ambavyo ni *common* sana, lakini kutaka kuwawekea kwamba tuna *wa-Judge* kwamba mwalimu akifanya hivi ni tofauti na maadili, akifanya vile ni kinyume na maadili, tunaweza kuwaonea sana walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine ukienda, *dressing code* ya stahili hii inakubalika lakini kwenye maeneo mengine *dressing code* ya stahili hii haikubaliki. Kwa maana hiyo, kuwepo na mjadala wa Kitaifa ambapo hata walimu nao waridhie kwamba tuna *abide* kwamba hii ni sahihi na hii siyo sahihi. Vinginevyo tutawaonea kama ambavyo tumekuwa tukifanya katika wakati tofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nimekipitia, nashauri kwamba kama kumekuwepo na tuhuma dhidi ya mwalimu, baadaye amekata rufaa kwa Waziri ambapo Kamati imependekeza siku tisini nami naafiki siku hizo tisini badala ya siku thelasini ambazo zinaonekana ni chache, rufaa imeenda tena *High Court* na mwalimu ameshinda rufaa yake, kuwepo na *remedies* ambazo mwalimu atawezu kupatiwa. Kama ameshinda kesi yake na ameweza kuwa *installed*, sasa Bodi husika itoe tamko rasi kuonesha kwamba walikosea na badala yake wamwondolee zile tuhuma mwalimu aweze kuwa *cleared* kuendelea na kazi badala ya kuonekana ana makandokando ambayo amekatia rufaa na ameshinda. Kwa hiyo, kwenye marekebisho nitakuja na kipengele cha kupendekeza *remedies* ambazo mwalimu au mtuhumiwa anapaswa kupewa kama akishinda rufaa yake dhidi ya *charges so and so.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache kwa jinsi nilivyopitia Muswada, naomba niishie hapo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Umejielekeza kikamilifu kwenye hoja iliyo mbele yetu, tunakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Othman Haji.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie Muswada huu uliopo mbele yetu. Kabla sijaendelea nami naipongeza hotuba ya Upinzani ambayo imeshiba ushauri. Namshauri Mheshimiwa Waziri auchukue ushauri huo kwa sababu ni mzuri kweli kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi mimi nitajikita katika suala hili la leseni kwa walimu, ambalo nahisi kidogo ni geni. Kwa kule Zanzibar kwetu siyo geni, walimu wana leseni, lakini sijui kutakuwa na tofauti gani kwa leseni zinazotumika Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani alivyosema, tasni yetu ya elimu ina uchache wa walimu. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kusema kwamba kuna ongezeko la walimu lakini lazima tujue kwamba kuna matataizo ya walimu. Ukienda kwenye shule huko utakuta wengine wanakamatiza tu, kuna masomo hayana walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuweka kipengele hiki cha leseni maana yake umeweka kizuizi cha wengine wasiingie katika kada hii ya ualimu. Ni jambo nzuri, lakini tukumbuke kwamba kuna baadhi ya masomo katika shule zetu, sio walimu tu wenyetaaluma ya ualimu wanaofundisha. Mfano kuna masomo ya hisabati na fizikia, kuna walimu tunawategemea kama wa *engineers*. Ukienda kwenye shule za binafsi hawa walimu wanapatikana kwa wingi lakini hawajapitia ualimu. Je, tunapoweka kikwazo hiki huu mchango wa hawa watu utapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu nilimsikia Mheshimiwa Waziri akisema kwamba asilimia 90 ya wanafunzi wetu wanaohitimu masomo yao, wanafeli somo la hisabati. Kwa hiyo, hiyo asilimia 10 inayopatikana Waziri ajue kwamba na hawa watu wengine wa nje wana mchango wao. Kwa hiyo, pamoja na mambo mengine kipengele hiki cha kuweka leseni kinakwenda kuzuia walimu wengine ambao watataka kusaidia hii taasisi wasipate nafasi hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine ni malipo ya ada ya leseni. Kama tunavyojua walimu wetu ni dhaifu kimapato. Katika wafanyakazi ambao wanawalipwa kima kidogo kabisa cha malipo ni walimu. Walimu hawana hata mahali pa kukaa. Walimu katika ya mishahara yao wanalipa *income tax* na kuna malipo mengine, ikiwa wataongezewa mzigo mwingine wa malipo itakuwa ni janga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri, ikiwa ni malipo ya leseni kwa walimu iwe ni mara moja. Yaani pale wanapokwenda kukata leseni, iwe ni mpaka kustaafu kwake. Vinginevyo ikiwa kila mwaka wanalipa haya malipo ni kwamba mnafanya walimu ni chanzo cha mapato ya

Serikali kitu ambacho hakikubaliki. Kwa hiyo, nashauri malipo ya leseni yaondolewe au yawe mara moja tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka hapo, naenda kwenye ukomo wa hii leseni. Sifa ya ualimu ni ujuzi na ujuzi hauzeeki. Walimu wengi wanapostaafu wengine hutaka waendeleze ujuzi wao katika shule nyngine za binafsi. Sasa nilitaka kujua vipi huyu mtu ambaye amefika ukomo wa kustaaafu, ataruhusiwa kufundisha katika shule au ni mpaka akate leseni nyngine? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hilo hilo la leseni, sasa nizungumzie hawa walimu wa kigeni. Katika shule zetu, hususan *private*, utakuta kuna walimu wa kutoka Uganda, Kenya, Sudan wapo mpaka Waturuki wapo, sasa hawa watakuwa na sifa zao zinazowaleta hapa. Kipengele hicho sijakifahamu mpaka sasa hivi, nataka Mheshimiwa Waziri atueleze, vipi wakiwa hapa watachukua zile zile sifa zao walizokuja nazo au tutawapa leseni kama tunavyowapa hawa walimu wa Kitanzania? Nashauri walimu watakaoingia hapa pamoja na sifa zao na wao tuwalazimishe wawe na leseni za Kitanzania kama wanavyofanya walimu wa hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi langu ni hilo la leseni, naomba kuunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Magembe na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, lakini naomba nitoe shukurani zangu za dhati na furaha kubwa sana niliyonayo leo. Leo tunaandika historia kama Bunge, tunaenda kutambua hadhi ya mwalimu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo hakika Marehemu Mheshimiwa Bilago angekuwepo angeanza na maneno yafuatayo. Siku zote aliniambia ukimaliza Uenyekiti hujatupa *Teachers Professional Board* utakuwa hujawatendea haki walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusiwafanye walimu ni watu hohe hahe, tusiwafanye walimu ni jambo tu la kupita. Bunge hili limetunga Sheria ya Bodi ya Wahandisi, Bodi ya Wanasheria, Bodi ya Wakandarasi, hata juzi tu tumetunga Bodi ya Wasaidizi wa Madaktari. Ni kosa kubwa sana Waheshimiwa Wabunge kuukata Muswada huu. Tunaweza tukausahihisha Muswada huu lakini tusichanganye taaluma ya ualimu na maslahi ya malimu, hivi ni vitu tofauti sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Prof. Ndalichako kwa kuleta jambo hili. Ni jambo ambalo vyama vyote na wote waliokuja mbele ya Kamati yetu walikuwa wanalitaka miaka yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeshuhudia watoto wetu wanafundishwa na walimu ambao sio walimu na ukikosea kwenye kufundisha watoto huu ndiyo msingi wa kuwa na elimu bora. Ndiyo maana leo tumeona walimu kwenye shule za *private* wanafanya vituko lakini hakuna cha kuwafanya. Mikono ya Waziri wa Elimu imefungwa, hawezি kushughulika na mwalimu aliye kwenye *private school*. Mwalimu aliyeajiriwa kwenye Shule ya Sekondari ya Serukamba anaafuata masharti yangu mimi. Hiki tunachofanya leo Waheshimiwa Wabunge, tunataka tutambue hadhi ya walimu, *profession* ya ualimu lakini tuwawekee makatazo. Ukipanya makatazo hayo, tutakunyang'anya cheti cha kufundisha. Ndicho kilichofanya na Muswada huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali yako matatizo ya walimu; mishahara midogo, hawapati stahiki zao, hiyo ndiyo shughuli ya *TSC*. *Tanzania Service Commission* ina shughuli moja kuhakikisha inahangaika na maslahi ya walimu walioajiriwa Serikalini lakini Bodi hii inakuja kutambua nani ni mwalimu. Ukihamaliza ualimu, tumepeendekeza wasianze na *provisional registration*, waende moja kwa moja

wasajiliwe kwa sababu ukishawasajili utakapokuja kwenye leseni ndiyo tumeweka masharti sasa utuambie umefundisha mwaka mmoja. Kama umefundisha mwaka mmoja, tutakuwa tumeangalia tabia yako, tumefuatilia unavyoji-conduct, then tunakupa leseni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, sasa tutawapa walimu ajira. Sasa hivi walimu hawatategemea kuajiriwa na Serikali peke yake, kwa sababu walimu wote waliosajiliwa, walimu wenye leseni tunakwenda kuwapa hadhi kama Taifa. Akishakuwa na leseni yake anaweza akaenda Afrika Mashariki akafundisha. Tumeona juzi Rwanda ilitaka walimu wa Kiswahili Watanzania hawakuajiriwa, unajua sababu? Hawana leseni ya kufundishia. Hao wote mnaosema wanajasjiliwa na *TSC* ni walimu wanaoajiriwa na Serikali, ndiyo wamefanya *register* kule, wamefanya iwatambue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengine hapa tusiyachanganye matatizo ya mfumo na Bodi. Kwenye Bodi ya Injinia siyo Injinia wote wanafanya kazi *TANROADS*, *TAMISEMI* au Bunge, mainjinia wote kokote waliko wanatambuliwa kama mainjinia na wana Bodi yao. Hatuwezi kukaa hapa Waheshimiwa Wabunge tupinge Bodi hii ya Walimu, hapana, tutakuwa hatuwatendei haki walimu. Yako mambo hata kwenye Kamati tumesema, tuangalie kwenye leseni, *fee* yao isiwe kubwa sana kwa sababu walimu ni wengi, *fee* ipungue, lakini lazima tuisimamie maadili ya ualimu, taaluma ya ualimu lazima tuisimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakumbuka juzi kwenye mitandao, tumesema hapa, mwalimu mmoja anatembea na watoto wa kike wamemlalia hapa, imezagaa lakini hakuna cha kumfanya. Tungekuwa na Bodi hii, leo tungeshamnyang'anya leseni, yule asingekuwa mwalimu. Nawaomba sana wenzangu, Bodi hii ni jambo kubwa, tumefanya mageuzi makubwa kwa kada ya ualimu Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iende mbali zaidi, Mheshimiwa Waziri Prof. Ndalichako tuanze *ku-define*

nani anakuwa mwalimu sasa? Haiwezekani aliyepata *Division Three* au *Division Four* ndiyo aende kufundisha watoto wetu, tubadilishe. Umefika wakati kwamba ukifaulu, ukipata *Division One*, kazi yako ya kwanza mwalimu, ziko nchi zimefanya. Kwa kufanya hivyo, tutaanza sasa kuupa hadhi kubwa zaidi ualimu lakini pia tutapata walimu ambao watafanya kazi nzuri zaidi, lakini *as it is now* walimu wapo, vyuo viro sasa tuanze kwenda mbele zaidi; tumeshaandaa Bodi na baada ya Bodi tuanze sasa kuhangaika na kuweka watu gani wanakuwa walimu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu wanasema kuna kazi za *TSC*. *TSC* ina kazi zake, inahangaika na walimu walioajiriwa na Serikali, ikahangaike kuhakikisha walimu sasa wanapata stahiki zao, mishahara na vyeo. Hii ndiyo kazi ya *Tanzania Service Commission*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, tunakoenda, nimeona hapa kwenye Bodi, naomba Mheshimiwa Waziri akalete *amendment*, Mwenyekiti iteuliwe na Rais, kwa sababu Bodi zote zinateuliwa na Rais. Kwa kufanya hivyo, tutaendelea kuipa hadhi Bodi hii kwa sababu ukisema wewe uteue Mwenyekiti wa Bodi na wajumbe, nadhani siyo sahihi. Utaratibu wa Bodi zote, Mwenyekiti anateuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema, ukiangalia pale kwenye *registration*...

TAARIFA

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Sheria inasema, *registration* lazima uwe umefanya kazi mwaka mmoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ndogo.

MWENYEKITI: Taarifa tena!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati hii ya Huduma za Jamii kwamba hayo mapendekezo ambayo anashauri Waziri akayalete, tayari yameshaletwa na Waziri Kivuli wa Elimu, Mheshimiwa Susan Lyimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Peter Serukamba hili hakuliona, ndiyo maana hata kwenye hotuba yake halipo. Anachotakiwa kufanya ni ku-appreciate kwa sababu maoni haya ya mabadiliko yako tayari mezani kwake, aseme anayaunga mkono na amshawishi Mheshimiwa Waziri ayaunge mkono. Sasa sitarajii Mheshimiwa Jenista alivyoona... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana, Mheshimiwa Halima ni Mbunge wa muda mrefu lakini haelewi utaratibu. Ripoti hii ya Kamati ni ya Wajumbe wote. Ripoti hii ya Kamati tulioiandika Mheshimiwa Susan ni sehemu yake ...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Lakini Mheshimiwa Susan mwenyewe ameleta *amendment*.

MBUNGE FULANI: Si mlikataa?

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Nami hapa naongea kama Peter siyo kama Mwenyekiti. Unajua watu wanahangaika kupata *kick* hapa, ndiyo tatizo letu hapa. (*Kicheko/Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa yake, kwa sababu najua anakotaka kunipeleka, siwezi kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Nasubiri mmalize kusema ili niendelee.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba kuunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Almas Maige wajiandae.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango mdogo katika Muswada huu ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jambo hili la kutaka kuanzisha Bodi ya Taaluma ya Ualimu limeshughulikiwa kwa muda mrefu. Kwa kweli napenda nimpongeze sana kwa dhati kabisa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Prof. Ndalichako kufanikiwa kulileta jambo hili hapa Bungeni kwa sababu linahitajika sana. Hongera sana Mheshimiwa Prof. Ndalichako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru Mawaziri wa Elimu ambao walihudumu katika Wizara hii tangu mwaka 2006. Namshukuru hasa Mheshimiwa Mama Margaret Sitta ambaye alilanzisha jambo hili kwa nguvu mpya kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kupanuka kwa elimu haraka haraka katika miaka hii 20 iliyopita au miaka hata 30 hivi iliyopita, kumekuwa na walimu wa aina nyingi sana ambao wameingia kufundisha katika shule zetu. Mwanzoni tulikuwa na *Universal Primary Education* au ile ilikuwa inaitwa *UPE* na tukawa tunafundisha walimu wakati mwingine waliitwa hata Voda fasta. Kuanzia mwaka 2006 tulikuwa na upanuzi mkubwa katika shule za sekondari katika kila kata. Kwa hiyo, tukawa tumepanua sana idadi ya mahitaji ya ualimu katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho hicho kumekuwa na upanuzi mkubwa sana katika elimu ya juu na hasa katika vitivo vinavyofundisha walimu kwa ajili ya sekondari na shule za msingi. Kwa sababu hiyo, hii Bodi ni muhimu sana katika hatua hii ili kuweza kuhakiki walimu mbalimbali ambao wako darasani wanafundisha watoto wetu. Lengo kubwa hasa ni kuhakikisha kwamba uhakiki huu unatuletea ubora katika elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 - 2015 kulikuwa na uajiri wa walimu uliotoka walimu 7,000 katika shule za msingi mpaka karibu kufikia walimu 30,000. Haiwezekani kwamba wote hawa walikuwa ni wazuri na wenye sifa za kutosha. Kwa hiyo, wakati huu ni muafaka kuwa na Bodi hii itakayoweza kuwahakiki na kuweza kuhakikisha kwamba walimu wanaofundisha wana sifa stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nichomekee hapa hapa kwamba katika mikoa mingine wakati walimu walikuwa wanaongezeka sana kwenye shule za msingi na sekondari iko mikoa ambayo ikuwa haipatiwi walimu kwa sababu awali ilikuwa na walimu wengi kupita mikoa mingine. Moja ya mikoa hiyo ni Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya yangu ya Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya kiasili, walimu wanakuja, wanazeeka, wanastaifu, wanaondoka, wengine wanakufa na wengine wanahama, Walimu waliokuwa wameajiriwa katika Wilaya yangu mwaka

2001 wamepitiwa na mkumbo huo na hivi sasa kuna upungufu wa walimu 390. Wastani wa idadi ya walimu katika shule zetu za msingi ni walimu wawili au watatu. Nami naamini katika Wilaya nyingine kama Same na hata Hai na nyingine mkoani pale, ziko namna hiyo hiyo. Nawaomba wakati huu Wizara ya Elimu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI waende wapitie ikama, kwa sababu nafasi hizi zilizoko zina mishahara, watusaidie kuajiri walimu mapema iwezekanavyo, kwa sababu shule watoto wanakaa bure, hawafundishwi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nasema haya, nimeisoma hii sheria vizuri, nashauri kwamba walimu wale wanaofundisha kwenye vyuo vya ualimu, lakini pia walimu wale ambaao wanafundisha vitivo vya walimu watakaokuja kufundisha kwenye shule za msingi na sekondari na wenyewe walazimike kusajiliwa kwa sheria hii. Kwa kufanya hivyo itasaidia kuhakikisha kwamba kweli wale wanaofundisha walimu wanawafundisha kwa kuwa na sifa stahiki katika kufanya kazi hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la nidhamu na maadili. Walimu wetu ambaao wanafundisha huko na hawa ni wachache sana, lakini hawana maadili yanayotegemewa kwa mwalimu anayefundisha kwa kujenga malezi bora katika shule. Ndiyo maana katika hizi siku za karibuni kumekuwa na walimu ambaao wanapiga watoto mpaka wanakuwa; kuna walimu ambaao wanakuwa na mahusiano ya kimapenzi na watoto; na kuna walimu ambaao kwa hulka hawawezi kutekeleza wajibu wao. Katika haya ni muhimu sana Bodi katika Kamati zake ambazo zimependekezwa ziwe kali sana katika kuhakikisha kwamba kila mwalimu aliyesajiliwa na Msajili wa Walimu au Mrajisi awe na sifa stahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni kitu cha kupendeza kwamba Bodi hii sasa ikishamfukuza mwalimu anayefundisha kwenye shule za Serikali, mwalimu huyo hawezи kwenda kuajiriwa kwenye shule za binafsi. Hii itahakikisha

kwamba mtu ambaye sio mwalimu hawezi kufundisha kwenye *public school*/na *private school*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wazazi watakuwa na mahali ambapo wanaweza kwenda wakalalamika kama wanadhani kwamba watoto wao hawatendewi haki. Hili jambo ni muhimu sana. Nami nawashauri sana, pamoja na tofauti zetu za kiitikadi, tuiunge mkono Serikali kwa nguvu zote, Bodi hii ianzishwe na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa. Malizia basi, uunge mkono hoja.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga sana mkono Serikali katika kuleta Bodi hii na msisitizo wangu ni kwamba wote tuiunge mkono na ianze kazi mara moja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Hongoli.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kutakia heri wanafunzi wote wanaofanya mtihani wa *primary school* na niwatakie heri *specifically* wanafunzi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega. Matumaini yangu ni kwamba mwaka huu watafanya vizuri kama walivyofanya mwaka 2017 kuwa Halmashauri ya saba Kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa dhati kabisa na Mheshimiwa Waziri. Sekta ya elimu inahitaji *transformation* na *transformation* tunazofanya ni hatua kwa hatua. Uanzishwaji wa *Teacher's*

Professional Board limekuwa ni wazo na ni jambo ambalo limekuwa kwenye mjadala kwa muda mrefu. Bodi hii kwa muundo wetu wa kiutawala katika nchi, anayesimamia utawala na uendeshaji wa walimu ni Waziri wa TAMISEMI lakini anayesimamia sera, ni Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa *Teacher's Professional Board* unampatia Waziri wa Elimu mkono wa kuweza kuangalia walimu walioko katika shule zetu za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Hii itatupatia fursa na kumpa Wizara ya Elimu mtu anayesimamia sera mkono wa kuweza kuwasimamia walimu na kuhakikisha kile ambacho anakitazama yeze kama *vision* kinafikiwa. Hili ni jambo muhimu sana ambalo sisi kama Wabunge tunatakiwa kuiunga mkono Serikali kwa dhati kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na *conflict*, nami nimesoma kwa kina hotuba ya Dada yangu Mheshimiwa Susan. Ukitazama ameonyesha *a lot of gaps* ya *Teacher's Service Commission* na Muswada ulioko mbele yetu ni *Teacher's Professional Board*. Kumekuwa na maoni na hoja kwamba uwepo ya Bodi ya Kitaaluma hii ni kuongeza mzigo wa gharama katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kujiuliza, kama tunataka kupunguza gharama na kama tunataka *streamline* sekta ya elimu, tujadili mfumo wa *D by D*. Kwa sababu mfumo wetu wa *D by D* umemfanya mwalimu kuwa chini ya Mkurugenzi, kusimamiwa na Halmashauri na TAMISEMI, ndio maana kuna *Teacher Service Commission* anayeangalia maslahi ya walimu. Kwa hiyo, kama Sheria ya *Teacher's Service Commission* ina upungufu, huo ni mijalada ambao tunatakiwa tuulete, tutazame upungufu uliopo tuweze kuirekebisha sheria hiyo na hilo ni jukumu la Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeipitia sheria hii, jambo pekee ambalo naiomba Serikali, kwenye *functions* za Bodi hii mojawapo ni kufanya *training*. Naomba Mheshimiwa Waziri anapoenda kutengeneza *regulations*, hizi *training* za

kila mwaka ambazo mwalimu anapata, ziweze kuwa accounted na kupata *score marks* ambazo zitamsaidia mwalimu at the end of the year anapoangalia maslahi yake mwisho wa mwaka yaweze kuwa considered katika mapato yake ya mwaka. Kwa sababu mwalimu kama kapata taaluma ambazo zimetolewa na Bodi yenyewe kwa utaratibu maalum uliowekwa kwa mujibu wa regulation, kama ilivyo NBAA, score marks hizo ziwe na positive impact katika maslahi ya mwalimu ili iwe incentive kwa mwalimu kuweza kujiedeleza. Hili ni jambo la muhimu sana likaangaliwe katika regulation. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anachangia ndugu yangu Mheshimiwa Serukamba ali-rise a very important point juu ya suala la appointment ya Mwenyekiti wa Bodi. Mwenyekiti wa Bodi kutokana na sheria anateuliwa na Waziri. Nami naomba kwenye composition, sekta yetu ya elimu ina composition ya aina mbili, ina upande mmoja unaoendeshwa na private sector na upande mwingine unaendeshwa na Serikali. Kwa hiyo, nafikiri Serikali itazame composition ya ile Bodi; nimeona kwenye amendment ya Mheshimiwa Susan Lyimo naye kaweka, kwamba tuangalie ni namna gani tunaweza kuwaingiza watu wanaosimamia private sector katika Bodi ya profession wawe na uwezo wa kuwa na representation. Ni muhimu tuangalie namna gani composition hii tunaweza ku-add into that. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mwenyekiti, Mheshimiwa Serukamba alisema kwamba Mwenyekiti wa Bodi ateuliwe na Mheshimiwa Rais kama zilivyo Bodi nyingine. Nimeangalia amendmentya dada yangu Mheshimiwa Susan, pendekemo lake hajasema kwamba ateuliwe na Rais, alibadilisha tu Chairman to chairperson, hakukuwa na issue ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachotaka nishauri ni kwamba private sector inasaidia sekta ya elimu. Tuangalie namna gani tunaweza kuwaingiza katika composition ya ile Bodi, namna gani uwakilishi wa sekta binafsi uliowekeza katika elimu unaweza kuwemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu sana, *Professional Board* ya Walimu, naiomba Serikali, kutokana na *structure* na kazi yake, ni muhimu mno ikapata *resource* kwa nia njema, kwa sababu jambo hili litakuwa na *positive impact* kwenye suala la elimu katika nchi yetu lakini isiwe ni njia ya kuingiza chanzo cha mapato hasa hizi *fee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *annual fee* ambazo mwalimu atatakiwa kulipa *for registration*, nashauri na naomba *humbly* na Mheshimiwa Waziri namwomba sana, atakapoenda ku-*form regulations* iendane na hali halisi ya kipato cha walimu ili isiwe kiwango ambacho kitawa-*discourage* walimu kukata hizi leseni. Ni muhimu sana kwa sababu walimu wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu lakini kipato chao ni kidogo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kuipongeza Serikali kwa dhati kabisa kwa kuja na Muswada huu. Hii ni hatua muhimu sana ya kuleta *reform* katika sekta yetu ya elimu na nimpongeza Mheshimiwa Waziri kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bashe kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Joram Hongoli na muda ukiruhusu Mheshimiwa Allan Kiula, ajiandae.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia kuwaombea wanafunzi wote wa darasa la saba ambao wameanza kufanya mitihani yao leo. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili waweze kumaliza mitihani vizuri na hatimaye waweze kufaulu vizuri na kwenda sekondari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kuleta Muswada huu muhimu sana kwa walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ambao ni walimu tulipo humu ndani tumekuwa tukiulilia kwa muda mrefu tangu tulipoanza Bunge hili kwamba tunaomba tuwe na Bodi ambayo itasimamia masuala ya walimu (*Teacher's Professional Board*). Hatimaye leo tunafurahi kwamba Mheshimiwa Waziri ameileta na naipongeza Kamati kwa kuijadili na kuja na mapendekezo mazuri sana ambayo yapo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Walimu ni muhimu sana na huu Mswada ni wa muhimu sana kwa walimu kwa sababu kumekuwa na makundi ya walimu. Kama wenzangu walivyosema, ni kwamba kuna walimu wale ambao wanafanya kazi kwenye shule zisizo za Serikali na wale ambao wanafanya kazi kwenye shule za Serikali. Wale wanaofanya kazi kwenye shule zisizo za Serikali walikuwa wanaonekana kama *weak* hivi au hawakutambulika kwa sababu wenzao wa Serikali wanapewa *cheque number* na wanatambulika, lakini hawa waliopo kwenye shule za watu binafsi, wamekuwa wakifanya lakini bila kutambulika na wakati mwingine wanashindwa kupata stahili kwenye baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, sasa kuititia hii Bodi sasa walimu hawa watatambulika kama walivyo wenzao kuititia usajili. Kwa hiyo, napongeza sana hili na litatusaidia sana kuhakikisha kwamba walimu wetu wote kuwa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wenzangu wameeleza vizuri kwamba uwepo wa Bodi hii ya Walimu itakayosimamia mambo taaluma za walimu, itatusaidia sana kuwaondoa wale walimu ambao hawana vyeti, wale walimu ambao wamekuwa wana matatizo sehemu nyingine, wakipata matatizo kwa mfano Serikalini, wamekuwa wakimbilia kwenye shule za watu binafsi, kwa sababu kule hawawezi kurudi kwa sababu ya yale matatizo. Kwa hiyo, sasa kumbe kuititia huu usajili ambao utafanyika kila mwaka, wataweza kubainishwa na hatimaye kuondolewa kabisa kwenye utumishi wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna moja ama nyingine imekuwa ni moja ya sababu inayochangia pengine

utovu wa nidhamu, lakini pia kushuka kwa maadili katika shule zetu hizi za Tanzania. Kwa sababu watoto wanaofundishwa wote wanakuwa ni Watanzania na wanaingia kulelewa na mwisho wa siku wanamaliza chuo na wanakuja kufanya kazi kama watoto wengine. Kwa hiyo, ni muhimu sana hawa walimu kwanza tujue taaluma zao vizuri, wakaguliwe, waweze kusajiliwa na kupitia huo usajili waweze kufanya kazi vizuri na hatimaye kuwalea watoto wetu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu kibaya sana kama kutomlea mwanafunzi vizuri hasa wale watoto wa chekechea. Sasa hivi kwenye vituo vyetu vyaa elimu hasa kwenye vituo vile vyaa *Day Care* na *Nursery Center*, kuna walimu wengi hawajapitia mafunzo ya ualimu wa awali lakini wanafundisha. Kuna wengine wameishia *form four*, kuna mwingine amefika *form six* anaanzisha kituo chake cha *Day Care*, mwisho wa siku huyu mtoto kwa sababu kile kituo kimesajiliwa, anapokelewa kwenye mfumo rasmi kwa maana ya shule za Serikali wakati amekosa maadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi ambacho mtoto tunamlea vizuri kujitambua lakini pia kuwa na maadili mema, tunaanza kumlea anapokuwa kwenye shule za awali pale chini ndipo malezi ya mtoto yanapoanzia, siyo huku juu. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na watu ambaa tuna uhakika kwamba hawa watu wana sifa stahiki za kuweza kuwasaidia watoto wetu waweze kupata maadili mema ya Kitanzania lakini pia waweze kufundishwa na kuandaliwa vizuri kwa ajili ya masomo ya shule ya msingi, baadaye sekondari na hatimaye vyuo vikuu. Kwa hiyo, ni muhimu sana na Bodi hii ndiyo mwarobaini wa tatizo hili la maadili kwa watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia ni kudhibiti maadili ya walimu. Tumesikia mara nyingi na Waheshimiwa wamesema hapa kwamba kuna baadhi ya walimu wanatoa adhabu zisizostahili, ni kwa sababu pengine hawajafundishwa, hawajaenda vyuoni. Kuna *clip* hapa nimeiona, mwalimu ameshika kiboko, anachapa wanafunzi

nafikiri sijui ni wa *form four* au *form five*, anawachapa viboko mgongoni na kichwani, sasa huyu sio mwalimu. Tunaojua ualimu huwezi kumchapa mtoto mgongoni wala kichwani, lakini kuna mwalimu anafanya hivyo. Kwa nini? Inawezekana huyu mwalimu sio mwalimu, hajapata maadili ya ualimu, hajapata kufundishwa namna ya kumlea mtoto na namna ya kutoa adhabu. Kwa hiyo, naamini kwamba tukidhibiti hili kupitia Bodi hii itatusaidia tuwe na walimu wazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini walimu wengine wamekuwa wakitembea na wanafunzi; anavaa *jeans* na *t-shirt* shulenii. Ukiuliza anakuuliza, kuna shida gani? Kwa hiyo, Wakuu wa Shule huko shulenii wamekuwa wakipata shida. Mkuu akimuuliza kwa nini unavaa *jeans*, *t-shirt*, nguo yenye maandishi mgongoni na kifuani, anauliza kuna tatizo gani, haelewi kwa nini anatakiwa asivae nguo hiyo kwa sababu amekosa maadili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi siku hizi kwenye vyuo vyetu wanafunzi wamekuwa wakijifunza kusomea mitihani, kujifunza namna ya kujibu mitihani, lakini wakienda kazini, mambo wanayofanya ni tofauti kabisa na namna inavyotakiwa. Naamini kwamba Bodi hii itasimamia vizuri kuhakikisha kwamba walimu wetu wanakuwa kwanza na maadili yanayotakiwa lakini pia wanayaafuata ili watoto wetu waweze kujifunza kwao. Maana mwanafunzi huwa anajifunza kwa mwalimu. Sasa mwalimu akiwa wa hovyo, basi mwanafunzi anajifunza mambo ya hovyo hovyo na mwisho wa siku tunakuwa na Taifa liliilo na mambo ya hovyo hovyo. Kwa hiyo, Bodi hii sasa itatusaidia kuhakikisha kwamba walimu wetu wanakuwa na maadili mazuri na hatimaye tutaanza kuwatengeneza Watanzania ambao wana maadili mazuri ya Kitanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye kifungu cha 74(2) kinachoeleza kwamba walimu watapata usajili, kutakuwa na *transitional provision* ambayo itatolewa lakini haielezi vizuri. Labda pengine niseme mtakapotengeneza kanuni, mjaribu kuweka hasa kwenye ile fomu, kuwe kuna maoni ya Mkuu wa Shule ama Mwalimu

Mkuu pale anapofundisha kwa sababu yule ndiye anayefanya *assessment* ya kwanza. Kwa hiyo, lazima atoe maoni kwamba huyu mwalimu aliyepo pale shulenii anafaa kuendelea kuwa mwalimu? Kuna walimu wapo huko, kwa mambo wanayoyafanya ni tofauti kabisa na mwalimu. Tusipokuwa na sehemu ambapo Mkuu wa Shule atamwangalia na kutoa maoni ya usajili wa huyu mwalimu kwamba asajiliwe au asisajiliwe kutokana na mwenendo wake akiwa pale shulenii, tutaendelea kuwa na walimu ambao hawana maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, watakapotengeneza kanuni na kwenye fomu zile kuwe kuna sehemu ambapo Mkuu wa Taasisi kwa maana ya Mkuu wa Shule au Taasisi aweze kutoa maoni yake. Kupitia maoni hayo pia, yataweza kufikishwa hata kwa Afisa Elimu Kata au Wilaya ili wakitoa *recommendation*, huyu mwalimu aweze kupewa kibali. Tukitoa tu kwa sababu amelipa, tutaendelea kupata walimu ambao hawana maadili. Mimi naamini kwamba tukifanya hivyo tutakuwa na walimu wazuri na watasaidia kiwango cha elimu kiweze kupanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Bodii hii pia itatusaidia kutambua walimu kila mahali walipo. Kwa hiyo, kwa kuwa watakuwa wanajili kila mwaka tutajua mwalimu fulani yuko wapi. Sasa hivi tuna uhaba wa masomo ya sayansi, kumbe kuna walimu wengine wako kwenye shule za binafsi wanafanya kazi huko, wanafundisha vizuri sana, kumbe tunaweza kuwachukua wale...

*(Hapa kengele illilia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Allan Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia Muswada huu ambao ni muhimu sana. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kuleta Muswada huu, nasema umekuja kwa muda muafaka. Nasema hivi kwa sababu taaluma nyingi zimeona umuhimu wa kuweka udhibiti au kutambua watu ambao wako sahihi katika taaluma hiyo. Ndiyo maana kwenye wasilisho la Mheshimiwa Waziri amejaribu ku-*cite* baadhi ya taaluma ya Uhasibu, Ufamasia, Ukunga na kadhalika kuonyesha umuhimu wa kuwepo kwa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri tu Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu aweze kufafanua kidogo tofauti kati ya Bodi na *Teacher's Service Commission*, kwa sababu hapa inaonekana upo mchanganyiko, huyu kachukua kazi za huyu na huyu kachukua kazi za mwingine. Kwa hiyo, hilo ni jambo muhimu sana. Ingawa Mwenyekiti wa Kamati alijaribu kufafanu lakini alikwenda kwa *speed* sana. Kwa hiyo, ni muhimu Waheshimiwa Wabunge tukafafanuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maudhui ya kuanzishwa kwa Bodi hii ni kulindwa kwa hadhi ya taaluma na utalaamu wa ualimu kwa kuzuia watu wasiokidhi vigezo na viwango. Ndiyo maana kwenye maeneo mengine tumekuta kuna madaktari *fake*, waandishi wa habari *fake*; sasa nafikiri huu ndiyo mwarobaini wa taaluma ya ualimu kulindwa tukizingatia kwamba taaaluma ya ualimu ni taaluma yenye heshima kubwa na ni taaluma yenye mchango mkubwa katika Taifa hili na sisi wote tumetoka mikononi mwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwenye Muswada, tukianza pale *section 5*, jambo la muhimu tunashauri kwamba uteuzi wa Kiongozi Mkuu au Mtendaji Mkuu ateuliwe na Rais, itakuwa ni jambo nzuri; Mheshimiwa

Waziri atue wajumbe wa Bodi lakini huyo Mtendaji Mkuu atue watendaji kwenye maeneo ya wilaya ambako huko mbele imeelezwa ili kuwepo na mgawanyiko, kwa sababu yule mtendaji ndio anasimamia wale watendaji kwenye ngazi ya chini. Sasa hili ni jambo zuri ambalo inabidi liangaliwe na mwasilisha Muswada aweze kuangalia kama anaweza kuleta *amendment* ikawa imekaa vizuri. Nafikiri kazi hiyo ya Rais kuteua itakuwa haina uzito wowote ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa tukienda ukurasa wa saba, *functions of the Board*, kifungu cha 6(2) kuna kitu kimeandikwa: “*In performing its functions under this Act, the Board shall collaborate with the Ministry with a view of ensuring that individuals who wish to be trained in the teaching profession, receive the requisite education and train for registration under this Act.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kwamba Wizara sasa inajivua hapa. Kwa nini Wizara isibaki na jukumu lake la kuhakikisha hilo jambo linakuwepo? Kwa hiyo, hii kazi haikutakiwa kupelekwa kwenye Bodi. Nashauri hapa pafanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *section 9, delegation of power* na penye nikapata mashaka kidogo, nikaona Bodi imeshaanza kuzidiwa kazi hata kabla hajaanza. Kwa hiyo, nafikiri suala la *delegation* kwenye kifungu kidogo cha (1) yote iwe *deleted*. Sababu pia aliposhuka chini kidogo kwenye kifungu kidogo cha (3) anasema, *Notwithstanding subsection (1), the Board shall not have power to delegate its, zile powers* zikawa zimelezwa pale. Kwa hiyo, suala la *delegation* nafikiri lote tu lingeachwa, Bodi iachiwe utaratibu wa kufanya kazi na majukumu yote Bodi iwe inawajibika kwa sababu tunapoanzisha kitu, tunataka hicho kitu kiwajibike. Tunasema tunaanzisha kitu kikubwa ili kiwajibike katika tansia hii ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *section 14(2)(a)*, kuna kitu pia nimeona kama hakijakaa sawa. Wanasesma, *conduct preliminary investigation on charges or complaints*

against teaching professionals on malpractise, lack of competence, unajua ili tupate walimu bora huu mchujo unatakiwa uanzie kwenye *admission*, kwa hiyo, anapomaliza anakuwa amehitim. Kwa hiyo, viko vitu ambavyo vitapimwa anapokwenda kufanya kazi, lakini suala la *competence* vyuo vyetu viwe vimefanya kazi ya kutosha kuona hao walimu wanaotolewa wanakuwa kweli ni walimu wameiva, ndipo twende kumpa leseni. Sasa mwalimu anatoka, mpaka unampa leseni anakwenda kupimwa kule na Bodi inaonekana kuna udhaifu huku kwenye chujio la kwanza. Kwa hiyo, chujio linatakiwa lifanyike kikamilifu. Sasa hilo na lenyewe lingeweza kuangaliwa kwa uzuri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukurasa wa 10, suala la *ku-reject an application*, nilifikiri hii Bodi inaanizishwa inakuwa ni ya klsasa kabisa, kwa sababu kutakuwa na mambo ya *IT* na kila kitu. Kama *IT* ipo, ina maana ile *application* yenyewe itakuwa *rejected* unapotuma tu maombi yale, inakataliwa moja kwa moja. Kwa hiyo, hili jambo litakuwa halipo. Kwa hiyo, eneo hilo nashauri liondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *full time teaching* na lenyewe napendekeza lifafanuliwe vizuri. Pia ukienda ukurasa wa 11, kifungu cha 21(2)(b)(iii), pale aliposema, *the Board shall take into account any behavior of the applicant if, is unfit to be a teacher*. Narudia kule ambako nilisema kwamba chujio la mwalimu linatakiwa lianzie mbali. Kwa hiyo, Bodi illtakiwa ifanye mambo mengine, siyo hii kusema *unfit to be a teacher*. Hilo ni jambo ambalo linatakiwa liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ukurasa wa 12, *section 23* linazungumziwa suala la tozo. Hizo tozo kama Waheshimiwa Wabunge wengine walivyochangia, tunapendekeza kwamba tozo isiwe chanzo cha mapato na ziangulariwe zisiwe kikwazo. Nashauri *registration* iwe bure kabisa (zero) lakini kwenye *annual fee* ndiyo iwe inalipiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema *registration* iwe bure kwa sababu watu wanapomaliza chuo wanakuwa hawana pesa na hali zao ngumu. Kwa hiyo, kama hali zao ngumu, basi iwe zero ila huko kwenye *annual fee* ndiyo iwe inafanyika. Vinginevyo, tutashindwa kusajili watu wengi kwa sababu Serikali inaa jiri walimu wachache na wengine wanaenda *private sectors* lakini wako watoto na kaka zetu mtaani na vyeti vyao wanazunguka. Sasa hivi tu hawana kazi, wakitakiwa walipe na hiyo *registration fee* itakuwa ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilliona nilzungumzie kidogo ni suala la kusimamia nidhamu. Sasa imefikia wakati kama tunatengeneza mifumo au taasisi za kusimamia nidhamu. Huyu mwalimu anakwenda kusoma, maana kama *degree* anasoma miaka mitatu, kama *diploma* anasoma miaka miwilli, sasa kule anakuwa hajawa *vetted?* Maana upekuzi unatakiwa uanzie kule, wenzetu wale kule kwenye vyuo waseme bwana wewe hufai, yaani kazi ya ualimu wewe haikufai. Kama mifumo ya huko itakuwa imekaa vizuri, hata nidhamu za walimu zitakuwa zimekaa vizuri. Kwa hiyo, Bodi itakuja kushughulika na mambo mengine tofauti na jambo la nidhamu. Vinginevyo, nidhamu huyu mwalimu awe amebadilika tu baada ya kuajiriwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Kwa leo kwa sababu ya muda ndiyo tunaishia hapo. Mchana tutaanza na Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala. Hawa watakuwa wachangiaji wetu watatu wa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na nilikuwa nimewataja Waheshimiwa watatu wa kwanza jioni hii, tuenze na Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala ajiandae.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada huu ulioko mezani leo, Muswada wa kutunga Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Kitaaluma ya Walimu. Kwanza nami namshukuru sana Waziri wa Elimu na wadau wote ambao kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana kuuleta Muswada kama ulivyo. Pia ninayo machache ya kuchangia vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ualimu ni taaluma kama ilivyo taaluma ya uhandishi, udaktari, ukandarasi, sheria na kadhalika. Kinyume cha Bodi zote ambazo zinaongoza taaluma zetu hapa nchini, ualimu unaonekana kwamba siyo chochote na haukuwa na Bodi yoyote ya kitaaluma kuweza kuuongoza na kuusimamia. Matokeo yake watu wengi ambao hawana taaluma ya ualimu wameenda kufanya kazi ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawasawa na watu fulani wajitolee kwamba wanajua udaktari waanze kutibu watu, hao waandisi bila kuzuiliwa chochote mtu ajitangaze yeye ni mhandisi aanze kujenga majengo kama hilli Bunge letu. Kazi ya kuingiliwa namna hiyo iltokea katika kazi ya ualimu tu. Kwa hiyo, kwa muda mrefu taaluma hii ya ualimu ambayo ni muhimu sana kwa kweli ndiyo mlango pekee kwa mtu yejote anayetaka elimu kinyume chake ni kuingia ule mlango wa wajinga. Leo Bunge lako linajadili Muswada muhimu sana

ambao utaunda Bodi itakayolinda elimu yetu. Mlango huu wa elimu utalindwa sasa kwa Bodi ya kitaaluma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ualimu ni taaluma, kwa hiyo matokeo ya watu kuingia katika taaluma hii na kufanya kazi, walifanya iporomoke. Matokeo yake walimu wakaanza kujitetea tu kwamba taaluma ya ualimu ni wito na wamedumu kwa njia hiyo kwamba ukiingia huku, basi ni wito usifanye mabaya. Matokeo yake ni nini? Baadaye maneno ualimu ni wito yakashindwa kubeba taaluma ya ualimu na tumeanza kuona kuperomoka kwa taaluma, walimu ambao hawakuwa walimu sasa wakaanza kufanya matendo mabaya, walimu ambao ni bandia wameanza kulala na wanafunzi wao; wameanza kuiba mitihani; wakaanza kuwasaidia wanafunzi kufanya mitihani; wakaanza kuwapiga wanafunzi bila mpangilio; na wengine wakawapiga mpaka wakawaaua. Maneno kwamba ualimu ni wito hayakuweza kuhimili kishindo cha taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunajaribu kuandaa tiba ambayo walimu waliingoja kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, Muswada huu uliopo mbele ya Bunge lako, utaleta taaluma ya ualimu kuwa sambamba na taaluma nyingine nilizozitaja hapo nyuma. Kwa kifupi, utasimamia taaluma ya ualimu na kuwa tiba ya matatizo yote ya walimu hapa nchini na hivyo kuleta jambo ambalo walimu wamekuwa wanalandai la usalama wa taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, kifungu cha 6(1)(a) mpaka (j) kimeweka majukumu ya Bodi ambayo tunaipendekeza. Bodi itafanya kazi ya kuweka viwango vyya utaalamu wa ualimu; kusajili walimu wote nchini; kutakuwa na leseni ya kufundishia walimu; itasimamia uwezeshaji na kusimamia utoaji wa mafunzo kwa walimu; itafanya kazi ya kusimamia maadili na utaalamu wa walimu; itafanya kazi ya utafiti hususan kuhusiana na utaalamu wa ualimu nini kifanyike ili kuboresha tasnia hii; itafanya kazi ya kusikiliza mashauri dhidi ya walimu waliofanya makosa na kuvuruga au kwenda kinyume na maadili na taaluma ya Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya siyo madogo. Mambo haya ndiyo walimu wamekuwa wakilia miaka yote kwamba tungefanyiwa hivi msingetulaumu kwa sababu wanaofanya makosa siyo wanataaluma ya ualimu ambao sisi tunesomea. Leo Serikali ya Awamu ya Tano imesikiliza. Najua Bodi hii au Muswada huu umekaa miaka mingi ukijadiliwa na walimu pamoja na wataalamu wa elimu na kufikia hapa tulipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo tunajaribu kutoa tiba ya matatizo ya walimu nchini. Kwa hiyo, ni lazima tunapokwenda, mambo ambayo yalikuwepo yatafutika kama mtu aliyefua nguo iliyokuwa chafu na kuwa safi. Bodi hii imeliliwa na walimu kwa sababu walitaka kuthaminiwa, kuheshimiwa na kutambuliwa kitaaluma. Kwa hiyo, kutungwa kwa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Kitaalam ya Walimu ni jambo muhimu sana kwa faida ya maendeleo ya elimu nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuchangia hivyo. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maige kwa mchango wako. Mheshimiwa Richard Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kamala na Mheshimiwa Edward Mwalongo, ajiandae.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza, nianze kuipongeza Serikali kwa hatua ambayo wameifanya ya kutambua taaluma hii kwamba inabidi ikae kwenye hali ya *professional*/na tukijua idadi kubwa ya watu ambao wameajiriwa kwenye upande wa ualimu ndio wanaoongoza nchini Tanzania na ndiyo msingi wa maendeleo wa Taifa letu kupata wataalam wa maeneo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kwenye vifungu kwa haraka haraka nikianza na kifungu cha 5 kuhusiana na Bodi. Kama wengine ambavyo wamechangia kwamba Waziri ndiye ambaye atamteua Mwenyekiti wa Bodi, nafikiri

tutengeneze *consistency*, other Professional Boardies Rais ndiye anayeteua, halafu pia tuongeze suala la *qualification* kwamba Mtanzania angalau awe na shahada mbili halafu amekuwa *senior for a minimum of ten years.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchanganyiko wa wale *members nane, subclause (3)*, wale wawakilishi kutoka kwenye vyama wawe wawili badala ya mmoja. Halafu ile *subclause (4)*, pale kwenye *two members appointed by the Minister* awe mmoja. Kwa hiyo, kwenye marekebisho upande wa kifungu cha 5, napendekeza yawe namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoka hapo tunaenda kifungu cha 6(2) na (3) jinsi gani Bodii ambavyo itaweza kushirikiana na Wizara hasa katika utunzi wa mitihani ambayo itakuwa zaidi ya *ki-professional*. Tutahitaji kwenye kanuni zitengenezwe ili ziwe zina-guide vizuri kullko leo hii kiongozi huyo anakuja na maoni binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo tunaenda kifungu cha 8 kwamba Bodii inaweza ikateua *members wachache* kama *sub-committee*. Sasa napendekeza hapa iongezwe iwe *at least three members* kwa sababu haijatajwa idadi, kwamba kwa *sub-committee* wanaweza wakateuliwa watu wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kifungu cha 10 kwenye suala la Msajili. Suala la Msajili iongezeke sifa, maana hapa hazijatajwa kwamba Msajili atakuwa na sifa za aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kifungu cha 11 kwa *Deputy Registrar* napo sifa hazijatajwa. Nashauri pia na yenye sifa angalau zitajwe hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 14 kwamba Waziri anaweza akateua wale ma-*supervisor* katika ngazi ya mkoa na wilaya, sasa tunaona hapa ile *chain of command*

tunai-break. Mtu wa wilaya na mkoa ambaye ni *supervisor* anateuliwa na Waziri, kwa nini asiteuliwe na *Chief Executive Officer* ambaye ni *Registrar?* Ihawezekana mtu ambaye ana-hire na ku-fire kwenye *management, controlling* inakuwa ni rahisi. Kwa hiyo, hapa ibadilishwe, badala ya *appointment of supervisory officers* kuwa Waziri awe *Registrar.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21(1)(b) kwamba ili mtu asajiliwe awe na uzoefu wa mwaka mmoja. Napendekeza hii iondoke kama ambavyo na wengine wamependekeza kwa sababu mtu unaweza ukamsajili bila hata kuwa na uzoefu kwa sababu ndiyo amepata kazi. Sasa tukiweka uzoefu wa mwaka mmoja halafu ndiyo asajiliwe, tutaondoka kwenye sifa za wao kusajiliwa. Kwa hiyo, napendekeza hii ya uzoefu iondoke, hata kwenye Bodi hizi nyingine hawaangalii sana uzoefu, wanakusajili unakuwa kama *graduand* halafu baadaye unaendelea ku-practice katika hiyo *professional.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21(4) kinazungumzia suala la mitihani ya Bodi. Kutokana na wingi wa walimu ambao wanahitim, itakuwa ni ngumu sana ku-monitor na kwa sababu kuna *collaboration* kati Bodi na Wizara, basi tuondoe hii mitihani ya Bodi tuweke tu moja kwa moja kule kwa katika vyuo vyetu ambavyo watakuwa wanahitim. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 24 kimezungumzia kuhusu *payment of annual registration fees.* Kwa sababu walimu kwanza mishahara yao siyo mikubwa na mtu ndiyo anaanza kazi, ananunua kitanda na analipa kodi. Kwa hiyo, tunapendekeza kwamba kwenye *regulations* zile *annual fee* ziwe katika kiwango ambacho wataweza kukikidhi au ku-afford waweze kulipa na isiwe kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 28 ambacho kiko sambamba na kifungu cha 34 kinazungumzia *temporary registration* ya *foreigners.* Mngejaribu kuangalia kwa mfano mtu anapata *working permit* ya miaka mitatu au miaka

minne au mitano, iendane angalau na *license* ambayo anapewa. Kwa hiyo, hilo pia liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 67 kwenye *reciprocal recognition*, kama mtu anatambulika na Bodi ya nje ya nchi yawezekana kule wana *terms labda ya five years au ten years*, sasa na hapa napo haikutaja moja kwa moja na sisi huku *license* zetu ni baada ya miaka miwili mtu ana-renew. Kwa hiyo, tuwe na *consistency*, tumpe *license* kulingana na Bodi ya nchi anayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 72 kwenye suala la Waziri kutunga kanuni, tuongeze pale katika kutunga kanuni sifa za wale *supervisors* ngazi ya mkoa na wilaya. Sifa zao zitajwe kule ili atakapoteuliwa tuwe na vigezo ambavyo vitaweza kufuatwa, ambao ndiyo mtiririko mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, niende kwenye *consequential amendment*. Tukiangalia, tuna Sheria ya *Teacher's Service Commission*, kazi zake zimetajwa pale, lakini nikiangalia baadhi ya kazi kidogo zina mwingiliano kwa asilimia fulani. Kwa mfano, *section 5(g)* inasema kwamba, *supervise teachers in-service training programmes*. Mtu tayari yuko kazini, kwa hiyo, *TSC* ndiyo wana-supervise hizo *in-service training programmes*. Kama zile za muda mfupi kwa nini zisiende kwenye *Professional Board*? Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri ni bora akaangalia suala hili. Hii inaenda sambamba na *section 5(i)*. Kwa hiyo, zile *training* ambazo zinazidi miezi sita, zibaki *TSC* na za chini ya miezi sita ziwe kwenye upande wa *Professional Board*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huo. Nafikiri na masuala mengine tutayaleta kwenye *schedule of amendment*. Naomba niunge mkono hoja na niipongeze Ofisi ya AG, nimeona kwenye *financial reporting* safari hii wamezingatia ule muda wa kupeleka ripoti kwa *CAG* na kwa Waziri tofauti na *Bills* ambazo ziliikuwa zinapita huko nyuma, kwa hiyo, hongereni sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako mzuri, umechambua Muswada. Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala, Mheshimiwa Mwalongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Malapo.

MHE. BALAZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa naomba nianze kwa kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa jinsi ambavyo alishiriki tarehe 19 kule Misenyi katika kuhitimisha kampeni kubwa dhidi ya UKIMWI pamoja na mimba za utotonii. Mheshimiwa Waziri uliyemtuma akuwakilishe, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Eva Maria, alifanya kazi nzuri, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Muswada huu, nimesoma ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho, *The Tanzania Teachers Professional Board*. Ukiangalia jina la Muswada unaona kwamba hili ni jambo kubwa lakini unapoenda sasa kwenye Muswada wenyewe kifungu hadi kifungu, unakuta umejikita zaidi katika kuangalia maadili ya mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu hapa ni kwamba, tumejaribu kumechukua neno *professional*/likawa sawasawa na *ethical*. Huu Muswada ungekuwa mzuri sana kama tungeuita *The Tanzania Teacher's Ethical Board or whatever*, unajikita zaidi kwenye *ethical* kwa sababu *profession* ya mwalimu kama taaluma, ina mambo mengi zaidi ya kuangalia maadili. Tunaangalia huyu mwalimu alisoma chuo gani, *syllabus* alizokuwa akisoma ni zipi na anafundisha namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mambo yote ukisoma Muswada huu huyaoni. Kama huyaoni, tafsiri yake ni nini? Maana yake kuna vyombo vingine vinavyoshughulikia mambo hayo. Kwa mfano, suala la kuajiri walimu hatalikuta kwenye Muswada huu. Maana yake kuna chombo kinachoshughulikia ajira za walimu. Ukisoma Muswada huu, hutaona moja kwa moja masuala yanayohusiana na ile

taaluma yenyewe ya ualimu. Maana yake ni kwamba kuna chombo kingine kinachoshughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muswada ni mzuri tuupitishe kama ulivyo, lakini naishauri Serikali basi ijiandae kuleta Muswada mwininge utakaotusaidia kupunguza uitiri wa taasisi mbalimbali zinazosaidia sekta ya elimu. Nasema hivyo kwa sababu ukzungumza na mwalimu mmoja mmoja, walichokitaka kimsingi na maombi yao ya awali waliyowasilisha Serikalini, ilikuwa kuomba chombo kitakachosimamia masuala ya elimu yote, nadhani ndiyo yalikuwa maombi yao. Kwa sababu sisi kama Wabunge tunaongea nao hawa walimu na juzi juzi nilipata bahati walinalika, nikajifunza na mambo mengi ambayo nilikuwa siyajui. Napenda kusema, kwa sasa huu Muswada tuupitishe kwa sababu ni hatua, lakini Serikali ijiandae kushughulikia kile killio cha walimu ambacho wamekua nacho muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye kifungu cha 43 kinaanzisha *Committee of Inquiry*. Ukiangalia sasa wajumbe ambao wanaingizwa kwenye *Committee of Inquiry* unakuta kuna wajumbe wawili *registered teachers, professional* hao; mjumbe mmoja kutoka *public service*; mjumbe mmoja kutoka TAMISEMI; na mjumbe mmoja *senior lawyer*. Ukingalia wote hawa, walimu wana vyama mbalimbali vinavyowawakilisha, huoni mwakilishi wao hata mmoja. Inapokuja kwenye *principle of natural justice* utakuta kwamba hawa ambao watakuwa wanakaa kujaribu kutatua matatizo mbalimbali, wanakosa yule mwakilishi anayewakilisha vyombo vyao. Sasa hili ni jambo ambalo kama lingeangaliwa lingeweza kutusaidia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba unaposema *professional* au *skills* za mwalimu, ufundishaji, hizi ziko *dynamic* hazipo *static*. Kwa hiyo, unapoamua kuzungumzia suala la *professional* ya ualimu, lazima uwe na mfumo ambao siyo tu unatoa leseni, unatoa leseni kwa mtu ambaye unajua ameandalila namna gani na ukishampa leseni, lazima umfuatilie huyo mtu anafundisha namna gani akiingia darasani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine tulifundisha ingawa lazima nikiri kwamba mimi sikuwa mwalimu bali nilikuwa *lecturer*, *lecturer* siyo mwalimu, lakini ukiamua siku moja unaweza kuingia darasani ukaeleza jinsi ulivysoma Uingereza, Japan dakika arobaini zikaisha, lakini umefundisha. Kuna Kitengo ambacho kinaitwa Udhibiti wa Ubora. Sasa hawa wadhibiti wa ubora ambao Mheshimiwa Waziri anawafahamu, ni watu muhimu sana, nami ningefurahi kama tunasema tunaanzisha chombo cha kusimamia ubora, basi wale wanaodhibiti ubora, wanaofanya kazi nzuri sana, wangeweza kuonekana kuwa sehemu ya Muswada huu jambo ambalo hatujalifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna jambo moja ambalo ni muhimu. Ziko *center* za *TRC*. *Center* hizi ni muhimu sana kwa sababu zimekuwa zikisaidia kumfanya mwalimu awe mwalimu kweli, aendane na wakati na ajue kwamba ufundishaji unabadijika. Sasa hizi *TRC* zilizo nyingi Tanzania nzima zimesahafulika. Muswada huu ungetenda haki kama ungegusia jinsi ya kuboresha hizo *Teachers Resource Center*, (*TRC*) na kuzi-/link jinsi ambavyo zitatusaidia kuongeza ubora wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Muswada huu kama ulivyo tuupitishe, lakini tuanzishe chombo ndani ya Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo hapa, tunayo changamoto kama nchi, gharama za uendeshaji Serikali zinaongezeka kila siku, lakini kila siku tunaanzisha vyombo vya namna hii. Kama kuna chombo ambacho kinaweza kufanya kazi hiyo, niwe mkweli, hakuna sababu ya kuanzisha chombo kingine. Majukumu yote haya tunayoyapa Bodi hii tungeweza kuyapeleka *Tanzania Teacher's Service Commission* na yakafanywa vizuri kabisa bila kuanzisha chombo kingine na kuongeza gharama za uendeshaji wa Serikali. Tusipokuwa makini, siku moja tutakuta tuna vyombo vingi vinavyofanya kazi ile ile na hiyo haitatusaidia sana kupata kile tunachokitaka, lazima tutumie rasilimali kidogo kufanya mambo makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makofî)

MWENYEKTI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala kwa mchango wako. Tunaendelea Mheshimiwa Edward Mwalongo, nilimtaja pia Mheshimwa Tunza Malapo, kule kwenyewe Tunduru.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimwa Mwenyekiti, awali ya yote, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia machache kwenye Muswada ulioko mbele yetu, Muswada wa kitaaluma wa Bodi ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema, naunga mkono hoja hii na naipongeza sana Serikali kwa kuleta hoja hili. Jambo la pekee ambalo napenda kulisema sana ni upande wa taaluma ya ualimu. Tumeshuhudia katika nchi yetu tukipita miongo kadhaa ya mafungu mbaliambali ya walimu, lakini kwa bahati mbaya sana mafungu haya yote yamekosa utafiti thabiti ambaao unaweza ukasema kwamba mwali mu yule aliyekuwa anaitwa Mwalimu wa *UPE* alifundisha na alikuwa na upungufu gani? Tumekwenda baadaye tumekuwa na madaraja mbalimbali ya ualimu na sifa mbalimbali za kujiunga na vyuo vya ualimu, lakini mpaka leo hakuna anayeweza kusema kwamba kijana aliyehitimu kidato cha nne na kuwa na *division four* na akawa na *point 28* akasoma taaluma ya ualimu, akapangiwa kazi ya kufundisha na akafundisha, alikuwa na upungufu upi?
(Makofî)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuundwa kwa Bodi hii, naamini kabisa kwamba sasa taaluma ya ualimu itasimamiwa vizuri. Nimeona hapa moja ya jukumu la Bodi hii ya Ualimu ni kusimamia taaluma ya ualimu. Tumeshuhudia siku za karibuni, kauli mbalimbali zikitolewa juu ya taasisi mbalimbali zinazotoa elimu ya ualimu, kumekuwa na kuyumba kwenye taasisi zisizo za Serikali na za Serikali. Vijana wanajiunga na vyuo lakini wanakatizwa masomo kwa kuambiwa kwamba hawana sifa. Kwa kuundwa kwa Bodi

hii naamini kabisa sasa kwamba Bodi itaweka utaratibu mzuri ambao utasaidia kutoa mwelekeo na utaratibu ambao utawezesha sasa kila anayetaka kufanya kazi hii ya ualimu atakuwa anajua mapema kabisa kwamba sifa yangu ni ipi, nikasome wapi na nifanye nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona kwenye Muswada huu ni kwamba, Muswada huu kwenye majukumu ya Bodi imeeleza vifungu mbalimbali ambavyo Bodi itafanya kazi, lakini ukiingia ndani ya Muswada wenye we unaeleza zaidi kama ni Muswada wa kusimamia maadili ya ualimu. Hii mimi inanitia mashaka sana kwa maana ya kwamba lengo zima la kuwa na Muswada linamezwa na kipande kidogo tu cha maadili ya ualimu. Sasa kama tutakuwa tunaunda Bodi ambayo itajikita tu kwenye maadili tu ya ualimu, basi niungane na wenzangu kusema kwamba tutafika mahali tutakuwa tunaunda vitu vingi halafu majukumu yake yatakuwa ni yale yale yanayojirudiarudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana katika suala hili tuwe makini sana kama Wabunge kuona kwamba hivi tunavyounda hii Bodi ni kweli inaenda kutatua tatizo lillipo? Au tunaunda Bodi kwa sababu tu chombo hiki kimedaiwa na watu wengi kiwepo basi kiwepo lakini majukumu yake yote hayatakwepo. Kwa sababu maelezo mengi yaliyomo kwenye hii Bodi yanazungumzia tu nidhani ya walimu, adhabu na kukata rufaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye hiyo taaluma ya ualimu wenye we, mbali ya kwamba hilo ni lengo limewekwa kwamba itasimamia utoaji wa elimu ya walimu sioni kwa ndani inaelezwaje kwamba itatoaje hiyo elimu, ni nani atawajibika na nini? Anyway kama alivyosema Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala kwamba hii ni hatua ya kwanza, lipite hili lakini tuombe sasa, nexttuleteewe kitu kingine ambacho kitajazilizia huu upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulisema, baada ya kupitisha huu Muswada, nina

imani utapita, lakini baada ya kuupitisha, kuna kipengele ambacho Wizara inatakiwa iunde kanuni. Hapa ndipo kwenye tatizo. Tunaweza tukapitisha huu Muswada leo, sheria ikasainiwa na Mheshimiwa Rais, lakini kanuni zikachukua miaka. Kwa hiyo, ikawa kazi yote tunayoifanya hapa inakuja kuwa *implemented* labda baada ya miaka miwili au mitatu. Kwa hiyo, itakuwa maana nzima ya shughuli yote hii iliyofanyika huko nyuma inakua siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, kama kweli tumedhamiria kuweka mambo sawa kwenye suala hili la walimu wa Tanzania na kwa maana ya kwamba walimu hawa ndio wanaosimamia taaluma, basi tuhakikishe kwamba kanuni zinatungwa mapema, mara tu baada ya sheria kusainiwa ili kusudi sasa Bodii hii ianze kufanya kazi mara moja. Kwa sababu ukitunga sheria, ukaunda hiyo Bodii, lakini huna kanuni, hiyo Bodii inakuwa haiwezi kufanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena jambo lingine wakati wowote wa kutunga hizo kanuni na waangalie sana mgongano wa kimaslahi, kwa sababu tunafahamu kwamba tunaiangalia taaluma hii ya ualimu kwa maana ya kwamba wanaofundisha shulenii, lakini ukienda Baraza la Mithani utakuta kwamba asilimia 90 ya watumishi wa Baraza la Mitihani ni walimu; ukienda Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, asilimia 90 ya watumishi wa pale ni walimu. Kwa hiyo, tuone kwamba vyombo hivi vingine ambavyo navyo vinashiriki katika zoezi zima la utoaji wa elimu vinashirikishwa vipi kwenye hizi kanuni ili kuondoa mgongano wa kimaslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaweka kanuni ambazo zitaleta ukinzani kwamba Bodii ya Usajili ya Ualimu inamtaka mtumishi wa Baraza la Mitihani ambaye ni mwalimu ajisajili na amejisajili, lakini anapokuja kukutwa pengine amekiuka baadhi ya miiko ya Bodii ya Walimu analindwa na Sheria ya Baraza la Mitihani ama analindwa na Sheria ya Taasisi ya Elimu. Kwa hiyo, haya ni mambo muhimu sana kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake, niseme kwamba nimefurahishwa sana na Muswada huu na hasa kwenye kipengele cha kusimamia taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwalongo. Mheshimiwa Tunza Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Gulamali na Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo nami niongee machache kuhusu hii Bodi ya Kitaalam ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ambayo napenda Waziri mhusika aje anipe ufanuzi kuhusiana na hii Bodi. *Concern* yangu ni kwamba, sisi kama walimu tulikuwa tunatamani tupate chombo kimoja ambacho hakitakuwa na matatizo katika kushughulikia mambo yetu ili tufanye kazi kwa weledi na kwa utulivu na kwa amani katika kuleta elimu ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naomba kupata maelezo machache, kwanza naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, sisi kama nchi, je, tunatengeneza walimu amba ni wataalam kulingana na mifumo yetu ya kuandaa walimu? Kama nchi ukasema kabisa mimi leo natoa wahitimu 200 waliopata labda stashahada ya elimu ni wataalamu? Hilo ni la kwanza, naomba nije nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimekuwa katika chuo cha ualimu, nimeona mambo mengi yaliyokuwa yanaendelea pale yalikuwa yanaturusha nyuma kwa maana kila siku mitaala inabadilika, mazingira ya kufundishia hayako sawasawa na mambo kama hayo. Kwa hiyo, naomba nipate ufanuzi, sisi kama nchi tunaleta chombo hiki ambacho tunataka walimu wajisajili kama wataalam, je, *are we preparing professional teachers?* Hilo swali langu la kwanza la msingi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nalotaka kuzungumza, kama walivyosema wenzangu wengi, ukiangalia huu Muswada umejikita zaidi kuzungumzia maadili ya mwalimu ambaye anaandaliwa katika mazingira ambayo siyo rafiki, anafanya kazi katika mazingira ambayo siyo rafiki, lakini mwisho wa siku tunataka tumpe mzigo mkubwa wa kumwangalia maadili yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mmoja, jambo hili hata tulipokuwa kwenye Kamati ya *LAAC* liliitokeza na tukalizungumza. Kwa mfano, mwalimu alishakopa benki, akabakiza $\frac{1}{3}$ ya mshahara wake, walipokuja watu wa Bodi ya Mikopo wakaongeza ile asilimia wakawa wanakata asilimia 15 badala ya asilimia 8. Kilichotokea mtu anapokea mshahara Sh.100,000, unamtaka awe na maadili ya kuamka asubuhi, mfano, anakaa Banana, anafanya kazi mjini, aende mjini, kwa sababu ukizungumzia suala la maadili ni pana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki kuweka mazingira ambayo tukimhukumu, tumhukumu kweli kakosa. Kuna mazingira ambayo yanamfanya akose, siyo kwa makusudi lakini ni mazingira ambayo yametengenezwa. Kwa mfano, mtu huyo anapokea mshahara kwa mwezi Sh.100,000, wapo walimu hao baada ya Bodi kuongeza yale makato, nina uhakika na ninachokizungumza. Anakaa sehemu anakotakiwa atumie nauli, unamtegemea kila siku saa 1.00 atakuwepo ofisini? Maana umeshampa leseni kwamba huyu ni mwalimu, ana leseni hii ya kitaalam lakini mwisho wa siku hatimizi yale anayotakiwa ayatimize na kuna mtu anamkwamisha ili asiweze kuyatimiza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, huu Muswada umemzungumzia zaidi mwalimu lakini simwoni mwajiri. Nataka nipate ufanuzi kwamba endapo mwajiri atakuwa hamtendei haki mwalimu huyu, kwa sababu Tume ni kama imeshindwa kazi kuwatetea walimu. Sasa *in case* mwajiri hamtendei haki mwalimu huyu, nafasi ya Bodi ni nini kwa mwalimu huyu? Naomba nipate ufanuzi wa jambo hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nachotaka kukizungumza kwa kifupi ni hizo ada za leseni ya kuingilia na ya mwaka, tuziangalie kwa kiwango chake. Hata kama mtu anasema tusiwaone walimu kwamba ni watu maskini, hawana uwemo, sisi hatuzungumzii vyanzo vingine, tunazungumzia chanzo chake alichokisomea mshahara wake, je, unakidhi haja ya haya mambo? Kama mtu ana chanzo kingine, hiyo ni *out of our business*, huko ni kujishughulisha kwake. Tunamchukulia mwalimu ambaye anaamka asubuhi, kama mnavyojua mwalimu ana kazi nyingi, aandae *scheme of work, lesson plan, log book*, kuna vitu chungu nzima. Wakati anaviandaa hivyo vitu, ana utulivu wa *mind kwenda deliver?* Unampimaje weledi wake? Ndiyo swali la msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye hii taarifa ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa tano pale kwenye matokeo ya kuwa na Bodi ya kitaalam ya Walimu, kipengele cha 1 anasema, kuinua hadhi ya taaluma ya ualimu na walimu kwa kusajili walimu wote kulingana na viwango vyao. Kwangu nafikiri hadhi ya mwalimu haiwezi kuinuliwa na kusajiliwa. Hadhi ya mwalimu itainuliwa na kufundishwa atakayofundishwa, mambo atakayopewa na thamani yake yeze kama mwalimu. Kumsajili hakumaanishi kwamba utainua hadhi yake na wala weledi wake hauwezi kuinuliwa kwa kumsajili. Weledi wake utainuliwa kule chuoni anakopata mafunzo. Wakati huo huo weledi huu utainuliwa endapo wale wakufunzi wanaomfundisha wapo katika *mind ambazo* hazina *stress*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Hayo ndiyo mambo ya Mheshimiwa Tunza Malapo, mwalimu haswa. Tunaendelea, nilikuwa nimetaja Mheshimiwa Seif Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami kuwa miongoni mwa wachangiaji katika huu Muswada. Pili, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na Naibu Waziri wa Elimu kwa jithada kubwa wanazofanya kuleta mabadiliko katika sekta ya elimu. Pongezi nydingi sana kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, kwanza nawashukuru na kuwapongeza kwa kuleta huu Muswada. Huu Muswada ulichelewa sana kuletwa ndani ya Bunge hili kwa ajili ya kuitishwa. Muswada huu ambao tunaupitisha, tayari ulishakuwepo katika nchi mbalimbali duniani. Kwa mfano, nchi kama Ghana, Nigeria na South Africa wanao. Hata Kenya walipitisha Muswada huu mwaka 2015. Kwa hiyo, ni Muswada ambao ulikuwa unahitajika hata kabla siku ya leo, lakini nashukuru kwa sababu ya kuliona hilo, mmeuleta na inakuwa sehemu mojawapo ya kuleta mabadiliko makubwa sana katika sekta ya elimu katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mapendekezo katika Muswada huu. Muswada huu umekuja ukiwa unawalenga walimu peke yake. Nafikiria kwamba kama Muswada huu umefika, ndani yake ungewekwa walimu lakini pia na wahadhiri. Kwa nini tunasema wawekwe pia na wahadhiri? Mkiangalia majukumu yaliyopo ndani ya Muswada huu, majukumu haya haya yanawalenga pia wahadhiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahadhiri pia katika vyuo mbalimbali wana taasisi na jumuiya zao. Kwa mfano, ukienda pale *University of Dar es Salaam*, wana Jumuiya ya Wanataluma inaitwa *UDASA*. Hata ukienda *University of Dodoma* wana Jumuiya ya Wanataluma inaitwa *UDOMASA*. Kwa hiyo, unaona hizi Bodipo katika vyuo. Sasa hivi vyuo vina Bodi zao kama vyenyewe, je, iko wapi Bodi inayochukua Bodi zote za vyuo hivyo? Kwa mfano, *UDOM* hata *UDSM* na vyuo vingine, iko wapi Bodi inayosimamia hao wahadhiri wote kuangalia maslahi yao na ubora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni mengine ya hii Bodi ni kutambua viwango vya utaalam wao; kuwasajili; na kutambua wahadhiri waliopo ndani ya nchi yetu. Hili jambo linawezekana kwani ukiangalia nchi kama Marekani unaweza kutambua ndani ya nchi yao kuna wahadhiri wangapi. Marekani wana *PhD holders* 67,000 na zaidi; Ujerumani wana *PhD holders* 28,000 na zaidi; Japan hivyo hivyo; na South Africa ina *PhD holders* 2,060. Je, Tanzania tuna *PhD holders* wangapi hatujui, hata ukienda ku-search huwezi kupata, sana sana tunafanya *guessing*. Bodi hii ni muhimu sana kwanza kuwatambua wenye *PhD; masters* na *degree* kwa sababu lengo lake ni kuwatambua na kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao kwa utaalam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza ndani ya Bodi hii kukawepo na Wahadhari. Bodi iwe na *department* labda ya Wahadhiri; ya waliofundisha *form five* na *six*, *form one*mpaka *form four*lakini pia ya watu wa *primary*. Kwa kufanya hivi itasaidia kuhakikisha kwamba una-regulate elimu yetu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wazo Waziri akiliona linafaa anatakiwa alichukue na ali-edit hapa kwenye kichwa cha habari kwa sababu madhumuni haya yapo na katika nchi zote duniani unakutana nayo, ukienda kuangalia *USA, UK, India*, mfumo ni huu huu. Kwa hiyo, hapa ni kuongeza tu kipengele hicho kwa sababu leo katika kudhibiti tuna wahadhiri wanaofundisha vyuo vikuu, kuititia Bodi hii inaweza ku-monitor wahadhiri wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaweza kukutana na malalamiko ya watoto wa kike katika vyuo vyetu wakinyanyasika kijinsia na mambo mengine tofauti, hata watoto wa kiume wananyanyasika kupitia utaratibu huo huo. Kukiwepo na Bodi, wanafunzi hawa wanaweza kuwasilisha malalamiko yao katika Bodi na ikawalinda kwa kufuatilia mienendo yao. Ukiwasilisha malalamiko chuongi, chuo kinaangalia umuhimu wa mwalimu katika chuo chenyewe kwa sababu kikimuondoa kitaathirika kama chuo kwa hiyo kinabidi kilinde maslahi ya mwalimu au mhadhiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimucombe sana Mheshimiwa Waziri, lazima Bodi hii iwa-*include* na wahadhiri kwa sababu hata wahadhiri wanallilia Bodi yao. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri sana hii Bodi ikawaingiza na hawa wahadhiri, itasaidia sana ku-*regulate* elimu katika nchi yetu. Katika mchango wangu nilitaka kugusia suala la kuwaingiza hawa wahadhiri katika Bodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa sababu ukishakuwa na Bodii taweza ku-*monitor* hata ubora wa elimu kwa sababu tuna *PhD holders* wengi *fake* na tuna *fake masters* nydingi sana zinaingia ndani ya nchi yetu. Kukiwa na Bodi lazima hawa waliochukua *PhD* nje ya nchi lazima waje wasajiliwe ndani ya nchi yetu ili tuwatambue ni nani na nani na wamesoma watu na kwa *qualification* gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kuna wahadhiri ambao wanatafuta kazi ya kufundisha hawawezi kupata vyuo. Anakuja hapa mhadhiri ana elimu yake lakini hapati chuo lakini kukiwa na Bodi atakuwa *registered* pale kwa hiyo chuo ambacho kitakuwa na uhaba wa mhadhiri fulani, kuititia Bodi hii itaweza kusaidia upatikanaji lakini pia kutambua uhaba wa hizo *qualification*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Kenya kuna *standard*, hata kwa Bodi hii kuwe na *standard* ya kumtambua huyu mwalimu ambaye tunataka kumpa ualimu. Kwa mfano, Kenya ili uweze kuwa mwalimu lazima ufanyiwe *interview* na upate alama 'C' na sisi kuititia Bodi hii tuna-*graduate* wengi sana, kila mmoja anasomea ualimu na akishamaliza kusoma tayari naye kawa mwalimu. Kuititia Bodi itaweza kuwafanya *interview* au kuwapa mtihani ambao utawasaidia kuchuja walimu, siyo kila anayesomea ualimu naye ni mwalimu. Ni sawa na wanaosomea uhasibu, unasoma uhasibu lakini unaenda kufanya mtihani wa Bodi ya Uhasibu uki-*qualify* unaenda kufanya kazi ya uhasibu. Kwa hiyo, hata hii Bodi naamini itaenda kufanya kazi hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza sana wahadhiri waingizwe katika Bodi hii. Hii itasaidia ku-*monitor*

elimu yetu kuanzia chuo kikuu mpaka shule ya msingi na chekechea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huo katika kuhakikisha kwamba tunaboresha elimu yetu. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Gulamali kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwanza kwa kumshukuru Mungu kwa kutupa uhai tuwepo hapa kuzungumzia suala la walimu na hii Bodii ya Kitaaluma ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu ni mtu muhimu sana katika maisha. Naamini kwamba ukitoka kwa mama mtu mwingine ambaye anakulea zaidi katika maisha ni mwalimu. Uwe ni mwanaume au mwanamke, mwalimu ni mtu ambaye anaheshimika na ndiye ametufanya hivi tulivyo hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya ukiwauliza watu au wazazi mtoto wako unataka awe nani? Watakuambia zile kazi ambazo zinaingiza fedha nyingi. Ukumuuliza *engineer* atakuambia nataka mwanangu awe *engineer*, ukumuuliza daktari atakuambia nataka mwanangu awe daktari, ukumuuliza mfanyabiashara atakuambia nataka mwanangu awe Mkurugenzi na awe *CEO*. Ukumuuliza mwalimu, kwa vile anajua dhana halisi ya mwalimu atasema, natamani mwanangu awe mwalimu lakini hii fani siyo nzuri kifedha. Mwalimu anayeifahamu kazi yake, mwalimu aliyefundishwa somo la malezi, angetamani mwanae awe mwalimu kwa sababu hata katika wanawake bora nasikia ni walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa kwenye Muswada na niende kwenye Sehemu ya *Tatu* inayozungumzia kuhusu *registration*. Kuna vipengele vingi vimeainishwa pale lakini naomba kusema kwamba kutokana na shule nyingi zilizopo nchini, shule za Serikali, shule za *private* na shule ambazo ni za kujitegemea tu tuseme, kwa kuwa na hii Bodi itasaidia sasa hata wale amba wanakuja kutoka nje kuanzisha shule zao wajue wanapata walimu amba wanakidhi vigezo na Serikali yenyewe ijue inapata walimu amba wanakidhi vigezo. Kwa hiyo basi, kuwa na hii Bodi itasaidia ku-*register* walimu kutokana na *qualification*, aina zao za ualimu na ngazi zao na hata atakapokwenda kusoma naamini atakachoongezea kitamsaidia yeye kuongeza hata kipato chake atakachokuja kulipwa baada ya kusoma mafunzo anayotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na aliyesema awali kwamba hii Bodi isishughulikie tu walimu wa shule za *primary* na *secondary* bali iende hata kwa walimu wa vyuo. Tunaelewa kwamba ili mwalimu wa chuo abakie pale chuoni kuwa *Assistant Lecturer* lazima awe ame-*perform* vizuri. Atakuwa amefaulu vizuri sana lakini atakuwa bado hana yale madili ya kiuallimu na ndiyo maana yake wakishakuwa *Assistant Lecturers* ili ukawe *lecturer* lazima upitie kozi mbalimbali. Kwa hiyo, napendekeza kwamba walimu wa vyuo nao wafikiriwe kuingia katika Bodi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia taaluma tu kwa mwalimu haitoshi na hapa katika Muswada wote haikuzungumziwa namna ambavyo mwalimu anaweza akatulia sasa akajifua, akaboresha ile taaluma yake. Hapa nina maana kwamba unakuta mwalimu yuko vizuri kitaaluma, lakini ana shida fulani fulani kutoka kwenye familia na anapoamka ili akafundishe mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nazungumzia katika zile Maslow *Hierarchy of Needs*, tuseme mojawapo *shelter*. Unakuta mwalimu ameamka kwenye nyumba duni sana anakwenda kufundisha wanafunzi amba wengi wao wameamka kwenye nyumba bora, unadhani mwalimu huyu

atatalia kweli ajiendeshe kitaaluma wakati ameweeka mkono kwenye tama anafikiria akirudi nyumbani anaingiaje pale. Mwanafunzi anamsaidia mwalimu vitabu akifika pale hakuna hata mahali mwalimu anaviweka vile vitabu vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Muswada huu ukipita ifikiriwe tena njia nyingine ya kuboresha maslahi ya walimu na kuwafanya wawe na *settled minds*. Nyumba za walimu ziboreshw, mafao ya walimu yafikiriwe, mwalimu apewe mshahara ambao unalingana na kazi anayofanya. Mwalimu anaamka alfajiri kabla ya mtu ye yeyote kuwahi shule, kengele igongwe, apange watoto aingie darasani. Mwalimu atarudi wa mwisho, akipitia *lessons* lakini mwalimu huyo huyo ni ye ye anafua watu kama hawa waliokaa hapa ndani, wote mmepitia kwa walimu lakini kipato chake ni kidogo kuliko wengine. Naomba sana Wizara ya Elimu iangalie hilo ili walimu waishi kwa raha, watembee vifua mbele na wakifikiria kugawa akili na uwezo wao ili tuweze kuwa na Taifa zuri ambalo linaweza kufikiri kimaendeleo zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na madai ya walimu muda mrefu na hapa naichomeka hiyo pia wakati tunapowafikiria kuwatengenezea Bodii lakini tuitengeneze hii Bodii wakati madai yao yameshatekelezwa, wamelipwa mishahara yao, wana amani na nchi yao, wanaweza sasa kwenda kufanya vizuri. Tuna bahati kipindi tunachozungumzia sasa Kiongozi wetu aliyeo madarakani Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alikuwa Mwalimu na pia mkewe Janeth ni Mwalimu, kwa hiyo, huu Muswada umekuja wakati muafaka kabisa, wakati ambapo watu waliopitia dhiki hizo wako katika madaraka na watawafikiria wenzao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu, pia naomba walimu wafikiriwe katika *incentives*, waongezewa au wawe wanapewa *hardship allowance*. Naamini kabisa mwalimu akipewa vitu vyta kumpa motisha, hata wengine wanaokuja nyuma wasiopenda kazi ya ualimu wataikimbilia na Bodii kama hii itakuwa na maana, hakuna sababu kuizungumzia

Bodi ambayo inaenda kuzungumzia watu ambao bado wana malalamiko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda tena pale kwenye madhumuni ya Muswada huu ile Sehemu ya Tano inaweka masharti kuhusu malalamiko ya walimu. Malalamiko haya yamekuwepo miaka yote, siyo malalamiko ya kubuniwa na kwa vile sasa yanaenda kufika mwisho kwa kuwa na hii Bodi tunataraji basi tukiunga mkono wote Muswada huu ukapita basi kuanzia mwaka 2020 hivi wala hatutafika huko malalamiko ya walimu yatakuwa hayapo tena katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ile Sehemu ya Saba inayozungumzia makosa na adhabu, makosa mbalimbali yaliyozungumziwa hapa yakiwepo ya kufundisha bila kusajiliwa na mengineyo, naomba nipayendekeze kwamba siku za nyuma walimu hao walikuwa wanafundisha wakiwa na ma-*inspector* wanawapitia shulenii mara kwa mara, wanafunzi na walimu walijua ma-*inspector* wanakuja. Kwa hiyo, naomba katika kuboresha japo halitaingia kwenye huu Muswada, lakini ifikiriwe pia walimu hao wawe na watu wa kuwazungukia mara kwa mara, badala ya kuwafikisha kwenye adhabu wawe wameshajirekebisha kabla hilo jambo halijafikia wakati wa kupeana adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na mengi zaidi ya hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri tu. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nyingine siku ya leo kuweza kuchangia katika Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote najiuliza hivi huwa tunatunga sheria ili nini? Naamini tunatunga sheria ili kutibu jambo fulani na tunatunga sheria tukiamini kwamba

walengwa wanakubaliana na mambo mengi kwa sababu ndiyo yanayokwenda kuwa-*affect*. Katika hili walengwa wakuu ni walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na tumechambua Muswada huu kwa kina, tumekuwa na wadau mbalimbali na wadau hawa wengi hawakukubaliana kabisa na Muswada huu. Sababu kubwa ni ile ambayo Waheshimiwa wengi wanaiongelea nalo ni suala la chombo kimoja cha kuwasimamia walimu lakini tumeendelea kuwafanya walimu hawa kama kuku wa kienyeji yaani wana vyombo vingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee walichokisema. Walimu wamekuwa na vyombo vingi kiasi kwamba wanajifananisha na wafungwa. Kwa mfano, wanasema, hata wafungwa wa mauaji hulindwa gerezani na askari wa aina moja tu ambaye ni Askari Magereza. Hatujawahi kuona vikosi vyote vya majeshi vikipelekwa gerezani kuwalinda wafungwa. Hata kwenye hitimisho lao wanasema kwamba wanaomba sana hili jambo au huu Muswada ungesubiri. Ukienda kwenye maoni ya Chama cha Walimu nao wanasema hivyo hivyo, hiki ni chama cha kuteteta haki za walimu na wanadai wao ndiyo walimu walioko madarasani. Nadhani tuna kila sababu, sawa tutapitisha kwa wingi wetu lakini kimsingi bado huu Muswada ulikuwa haujaiva kwa sababu una makosa mengi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa mfano, kumekuwa na hoja kwamba hii Bodi ya Kitaaluma ukiangalia kuna taaluma nyingine nazo zinasimamiwa na Bodi na mifano inakuwa kwa mfano *Doctor's Board, Engineers Board*, lakini tuwaulize, hivi hizo Bodi mnazozi-refer zenyewe zina Tume? Hazina! Kwa nini ni walimu tu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia hoja ya kwamba walimu wanasihamiwa na vyombo zaidi ya vitano na leo tunaongeza cha sita ni kweli na nadhani siyo sawasawa. Ukiangalia huu Muswada mzima kama ambavyo

wengine wamesema *seriously* ni kuwadhibiti walimu. Ukiangalia toka mwanzo mpaka mwisho hata hii hotuba ya Waziri hivyo hivyo, ni kuwadhibiti zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TSC* sawa najua ile ni Kamisheni ya Utumishi na hii ni kwa *public*. Tukasema kulikuwa kuna shida gani hawa walimu ambao sasa wanakuwa *included* na wale wa *private school* kwa nini nao wasiingizwe huko tukafanya maboresho. Hivi ni rahisi kuwa na sheria mpya au ni rahisi kufanya *amendment* sheria ambayo tunayo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata Chama cha Walimu Tanzania wanasema hivyo hivyo kwamba wanakubaliana na *TSC* iboreshweli tu wawaingize kwa sababu *TSC* iko mpaka kwenye Wilaya. Yalikuwa ni mawazo ambayo nadhani yangeungwa mkono lakini Serikali ikishaamua jambo lake inakuwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Muswada nasema ulikuwa haujaiva, kwa sababu tumejitalidi kwenye Kamati kuufanya maboresho, vilevile tulikuwa na Wizara kama kawaida, Ofisi ya *AG* lakini ukiangalia suala hili la Mwenyekiti wa Bodi ateuliwe na Rais lilitzungumzwa na wadau wameweka mapendekezo na sisi tukauliza. Wameleta majibu yao, haya hapa wakasema hata kwenye Bodi nyingine Wenyevitii na wajumbe wanateuliwa na Waziri. Kwa hiyo, masuala kama haya yanatia aibu na ndiyo sababu nilimuuliza *AG* hii ni sawasawa na akanijibu akasema siyo sawa. Sasa unajiuliza kama *AG Office* ilikuwa kwenye Kamati hili hawakuliona na wamekuja wakatuambia ni sawa? Kwa hiyo, nadhani kuna tatizo. (*Makofii*)

Mheshimia Mwenyekiti, sasa niende kwenye Muswada, hiyo ilikuwa ni *preamble*. Katika Muswada huu naanza na *section 5*. Pamoja na kwamba nitakuwa na *amendments* zangu kesho lakini niseme tu kwamba hii *composition* ya Bodi haijaka vizuri kabisa, nimelisema ndani ya Kamati na nalisema ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaongeza kitu kipyä kabisa kwa sababu tunaingiza *private sector* kwenye Bodii na *private sector* tunaweza kusema ni *about 20 percent* ya walimu wote. *If that is the case, ni lazima kuwe na representationya private sector. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia na AG atusaidie, kile kifungu cha 5(1)(iv), mimi najua *members* wa Bodii wanafanana kwa maana ya kwamba haendi pale kama sekretarieti au mtumishi. Ukitosha Kifungu cha 5(1)(iv) kinasema, *two members appointed by the Minister from amongst persons with requisite qualifications to assist the Board in the discharging of its functions.* Sasa najiuliza hii ni kazi ya member wa Bodii au ni ya sekretarieti? *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kwa sababu kuna kifungu cha 12 ambacho kinazungumzia sekretarieti, hawa watu waende kule. Hapa tunahitaji *members* ambao wanakutana mara chache na hawa hawawezi kuwa na *function* ya kumsaidia *Registrar*. Hawa wanakuja kwa ajili ya maamuzi au mambo maalum. Kwa hiyo, hicho kifungu kiondoke lakini kiwe *replaced* na walimu wawili kutoka kwenye *private sector.* *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema na narudia kusema, kama alivyosema Mheshimiwa Anatropia asubuhi, utaona Waziri ana jukumu kubwa kweli la *ku-appoint, appoint, appoint.* Mimi nadhani kwa sababu hapa Tanzania tuna vyombo vikubwa ambavyo ni *umbrella* vya walimu, kuna Chama cha Walimu Tanzania au *Tanzania Teachers Union - TTU*, vilevile kwenye upande wa *private* tuna *TAPIE*, tuna cha CHAKAMWATA ambacho mimi nilikuwa sikijui vizuri, kwa hiyo, kuna kila sababu ya hizi *organisation* zi-nominate watu wake halafu waingie kwenye Bodii na siyo Waziri kwa sababu hakutakuwa na hiki kitu tunaita *carrot and stick*. Kwa hiyo, nadhani kuna hiyo haja ya kuona kwamba hizi *organisations* kubwa namna hii zi-nominate watu wake waingie kwenye Bodii. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *section 7* anasema kwamba kazi ya Bodi ni pamoa na ku-suspend, lakini hawa walimu tayari wameajiriwa. Sasa nilikuwa naomba kujua kwa mfano wale wa Serikalini (*public*), je, Wizara ya Utumishi itakuwa *consulted?* Nani ana *mandate?* Ndiyo mambo kama haya tunasema inabidi yaangaliwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mwalimu kwa mfano amekosea amelewa, kama amelewa ameshindwa kufundisha maana yake taaluma imeathirika, lakini vilevile kiutumishi amefanya makosa. Naomba majibu kutoka Serikalini, huyu mwalimu atachukuliwa hatua na Bodi, *TSC* au Wizara ya Utumishi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ndiyo mambo ambayo tunaona kwamba kulikuwa kuna kila sababu ya kusubiri ili tu-*harmonise* halafu tuone tunaendaje mbele. Hakuna sababu ya kutunga sheria ambayo kimsingi haitaweza kufanya kazi kwa sababu *TSC* atasema mimi hili ndio jukumu langu, amelewa kwa hiyo, ni suala la kiutumishi, huyu wa Bodi atasema ameathiri taaluma wanafunzi hawajafundishwa vizuri. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo naona yanakinzana sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye suala hilohilo la Waziri kuteuwa, ukienda hiyo *section 14*, wale watu wawili wa mkoani ambao anawaita *supervisory officer*, ambao nadhani pia wawe ni *Assistant Registrar* kwa sababu wanaenda kufanya kazi hiyo, hawaendi ku-*supervise* chochote. Nadhani kazi hii ni *competitive* kwa nchi nzima. Mimi nilikuwa nadhani iwekwe kwenye gazeti watu wa-*apply* halafu Bodi ndiyo itasimamia wakati wanafanya hiyo kama ni *interview, whatever, then* wale watakaopatikana ndiyo waletwe Waziri awapeleke huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hili la *criteria* za *registration* walau Serikali imekubali, sijaona *ammendments* zao kwa hiyo sjui, lakini ukiangalia zile *criteria* za *registration* mambo yalikuwa mazito kwelikweli, nadhani kesho nitaona. Maana *ammendment* yangu imeletwa lakini ya Serikali

sijaiona isije ikawa na-repeat na sijajua ni kwa sababu gani hazijaletwa? Sijajua kama wanavizia waone kwanza zetu halafu ndiyo waende wakabadili? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu *renewal* ya leseni. Tulikuwa tunahoji kuhusu *license, license* ndiyo inapaswa kuwa *renewed* na sio *registration.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muswada ukiangalia ile *Part IV* kwa kweli Mheshimiwa AG naomba usome *section 41(3)(b)* utuambie hiyo sentensi ina maana gani? *If the employer of a person is identifiable from the details of the compliant, the employer.* Ndiyo sababu nasema haya mambo yanatia kidogo kashkash, kwa hiyo, nadhani kuna kila sababu ya kwenda kupitia na kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba hawa watu wanapokuwa *registered* wanakuwa *gazzeted*, lakini wakifanya makosa wakiwa *de-registered* mnataka wapelekwe kwenye magazeti yote nchi nzima tena ambayo yana *circulation* ya haraka. Hii nia ni ovu, mnataka kuwadhalilisha walimu. Kwa nini na katika hilo msiwaweke kwenye gazeti, mnataka kuwaweka kwenye *local news paper* ili kila mtu aseme aah, mwalimu yule alifanya vile amefukuzwa. Kwa hiyo, nadhani hiyo siyo sawasawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba sisi CHADEMA kumbe tulikuwa *far ahead* kwa Serikali kwa sababu kwenye *policy* yetu hii hapa, kwenye masuala ya taaluma ya walimu tuna sera yetu na tunasema kwamba, CHADEMA itaaniszha Sera ya Maendeleo ya Walimu ambayo lengo lake litakuwa ni kuweka miongozo ya vigezo vya chini vya mahitaji ya mafunzo kwa walimu, kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi na mitaala. Sera hiyo, itaweka utaratibu kwa ajili ya kumuendeleza mwalimu kitaaluma kila wakati ili kuboresha utendaji kazi wa mwalimu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaona ni jinsi gani sisi kwenye masuala ya walimu tumewapa walimu

kipaumbele kwamba, lazima waendelezwe. Hii ya kwenu niseme tu mnawadhibiti, mmeanzisha ile Tume mkasema mtawapandisha madaraja, mtawaongeza mshahara, *this is the third year hamjafanya hivyo*. Leo mnasema kwamba mtaimarisha utaalamu wa walimu, mtawapa mafunzo, hamna hata fedha, mtawezaje kuwaendeleza kitaaluma? Hata hizo sehemu za kuwaendeleza hakuna. (*Makofi/Vigelegele*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa uchambuzi wako Mheshimiwa Lyimo. Tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Haonga.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa chombo hiki cha kudhibiti taaluma za walimu binafsi naona siyo tatizo. Tatizo kubwa ambalo nalionna mimi ni kuwepo kwa vyombo vingi vinavyozungumzia masuala ya walimu na kusababisha mzigo kwa walimu kwa sababu, ukiangalia kila chombo kinachoanzishwa lazima mwalimu anatakiwa alipe ada, kwa hiyo, hilo ndio tatizo kubwa. Kwa hiyo, kila kinachoanzishwa lazima mwalimu ahusike, ndiyo maana Wabunge wengi wanasema kwamba, angalau tuwe na vyombo vichache ambavyo vitaangalia masuala yote kwa pamoja ili mwalimu awe amepunguziwa mzigo mkubwa. Tatizo kubwa hapa ni kwa nini kunakuwepo na vyombo vingi vya masuala ya walimu? Kwa nini tusiwe na chombo kimoja ambacho ni imara, *very strong*, cha kuweza ku-accomodate masuala yote ya walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Muswada huu ambaao uko mbele yetu kuna masuala mengi ambayo yanaingiliana sana. Ukiangalia majukumu ya Tume ya Walimu pamoja na ya Bodi hii inayoanzishwa kuna masuala kwa

mfano, Bodi inasajili na Tume inasajili; Bodi inatoa namba ya usajili, Tume na yenyewe pia inatoa namba ya usajili; Bodi inaadhibu, Tume na yenyewe inaadhibu. Sasa swalii la kujiuliza hii sheria ikipita hapa ikisainiwa tayari inakuwa ni sheria, wakati huohuo Tume inaendelea na kazi zake kama kawaida. Swalii la kujiuliza je, nani atakaye-*step down*? Nani atakayeacha kufanya shughuli zake maana Tume itakuwa inafanya shughuli zake kama kawaida wakati huohuo na Bodi imeshasajilliwa iko kisheria inaanza kufanya kazi zake? Kwa hiyo, kuna mwingiliano, Mheshimiwa Waziri atufafanulie atakapokuja ku-*wind up*, kwenye masuala haya yanayoingiliana baada ya Muswada kupita kuwa sheria haya masuala yatakuwaje kwenye utekelezaji wake? Hilo ni suala ambalo tungependa kupata ufanuzi baadaye wakati wa ku-*wind up*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo taarifa kwamba, kuna utaratibu mpya umekuja kwa ajili ya kupandisha madaraja ya ualimu. Kwa taarifa ambazo tumezipata ni kwamba, sasa hivi utaratibu utakuwa siyo kwa kufuata miaka aliyoajiriwa mtumishi, utakuwa kwa kuangalia utendaji wake, nidhamu kazini na mambo kama hayo. Sasa wakati utaratibu huu unakuja walimu wana malalamiko ya muda mrefu, ya miaka mingi, wanafanya kazi bila kupandishwa madaraja zaidi ya miaka 10. Wengine wameenda kusoma walikuwa *Diploma level*, wameingia *Degree level*, wako palepale. Wengine walikuwa *Certificate* ana *Diploma* yuko palepale. Mwingine ameenda kusoma alikuwa na *Degree* ameenda *Masters* yuko palepale. Badala ya kuwapandisha kwanza tunaleta tena utaratibu mwingine kwamba, tutakuwa tunawapima kwa kuangalia uwajibikaji, nidhamu na mambo kama hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli hili ni sahihi na tunaamua kwamba sasa utaratibu wa walimu wa kuwapa madaraja itakuwa ni hisani ya mtu anayemsimamia kazi, nina imani kabisa wapo walimu ambao hawatakaa wapandishwe madaraja kabisa kwa sababu, ni hisani ya mtu. Nayekupima kwamba unafaa kupandishwa au haufai ni mimi Sakaya, mpaka ukidhi vigezo ambavyo navitaka ni

hisani yangu. Naomba kama utaratibu huu kweli upo lazima Serikali iangalie mara mbili-mbili. Jamani walimu hawa ni fani muhimu mno, ni daraja muhimu mno, lakini mambo tunayowawekea inakatisha tamaa. Leo tusingekuwa hapa kama siyo walimu, lakini kila kitu mwalimu ni shida. Kwa hiyo, kama hilo lipo naomba Serikali itoe macho zaidi ya mawili kwenye sekta ya ualimu, walimu wapewe moyo, wawe *promoted* kwa wakati, tuweke utaratibu ambaao kila mwalimu atapanda kwa wakati wake na siyo kwa ajili ya hisani ya mtu, itakuwa ni shida kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nikienda kwenye Muswada sasa kifungu cha 29, kinasema kwamba, mtu hatafanya kazi yoyote ya ualimu au kuajiriwa mpaka awe *registered*. Swali ambalo naomba kuuliza nipatiwe majibu, wakati mwingine watoto wetu wa *form six* na *form four* wanapokuwa wamemaliza shule wanashiriki kwenda vyuoni wanakwenda kujitolea kwenye shule ambazo hatuna walimu labda wa sayansi, jografia au historia, wanatumia ule muda wao wa kupumzika nyumbani kwenda kujitolea shuleni kusaidia wadogo zao na walikuwa wanasaidia sana. Sasa naomba kujua, baada ya sheria hii kupita hawa waliokuwa wanajitolea wakati mwingine bure kabisa, wakati mwingine walimu wale wanawaangalia kutoka kwenye mifuko yao au wazazi wanawaangalia, je, huu utaratibu huu umekufa au utaendelea kuwepo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia wanafunzi ambaao wanamaliza *form four* shule shikizi kama Kaliua na maeneo mengine. Wale walikuwa wanachukua watoto ambaao wamemaliza *form four* wanasaidia kutoa elimu maeneo ambapo hakuna walimu, wazazi wamejenga shule zao wenye na kwa kweli wamesaidia maana maeneo yale ilikuwa hakuna kusoma, mtoto hasomi kabisa, lakini leo wamewasaidia watoto wale wanasona, kwa elimu yao ya *form four* wanawasaidia watoto wale na baadaye wanakua wanakwenda shule za kawaida ambazo ni shule za Serikali. Naomba kujua kwa sheria hii sasa, je, wale walimu waliokuwa wanajitolea hata kwenye zile shule shikizi za

primary ambapo ni baby class na darasa la kwanza na la pili, hawataweza kufanya kazi hii tena au itakuwaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nikienda tena kwene kifungu cha 35, kinazungumzia kuhusu Bodi kufuta usajili. Bodi inaweza kutoa jina kwene usajili, wameweka mambo mengi pale, lakini naomba nizungumzie suala lile la kwanza tu ambalo linasema kama atashindwa kulipa ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshazungumzia kwamba, kwanza walimu wana mzigo mkubwa. Kwa hiyo, naomba hiki kifungu kiangaliwe, ameshindwa kulipa ada kwa muda gani? Je, kuna sababu ya msingi imemfanya ashindwe kulipa ada? Je, alikuwa mgonjwa au anauguliwa? Naomba kifungu hiki pia kiseme kushindwa kulipa ada kwa muda kadhaa na kwa sababu ambazo hazina msingi, lakini tukisema tu kwamba, ameshindwa kulipa ada halafu ndiyo anaondolewa kwene usajili, hili ni tatizo. Haya mengine nakubaliana nayo, lakini hili la kwanza ni lazima tuweke muda, kama hiki kifungu cha 37 ambacho kimesema angalau mtu anapewa miezi 12, ilivyo hivi ni kwamba akipitiliza hata mwezi mmoja tayari anafutiwa kwa sababu, anaweza akawa na sababu. Kwa hiyo, naomba hili liwekewe *consideration* kwamba uwepo muda maalum kuhakikisha huyu mwalimu aliyeshindwa kulipa ada na ufanywe uchunguzi wa kutosha kwa nini ameshindwa kulipa ada, ameuguliwa, anaumwa au ana sababu zipi za msingi ambazo zimemfanya kushindwa kulipa ada kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kile kifungu cha 43, kinahusu Bodi ya ku-*appoint committee* ambayo itakuwa inashughulikia masuala ya hii Bodi. Ningombaa kabisa kwene sheria tuone *gender* hapa, tuone wanawake. Kati ya wale watano lazima tuseme *at least* wawili wawe wanawake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kila sheria inayopita hapa Bungeni, iwe ni bodi, iwe ni kamati, iwe ni chochote, lazima jicho la mwanamke lione kane. Kwa hiyo,

naanza kwenye kamati hii na kwenye ile Bodi inayoundwa lazima *at least* kati ya watu watano walioko hapa kwenye hii kamati itakayoundwa wawili wao wawe wanawake na iwe kwenye sheria, siyo kwenye *regulations.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kifungu cha 52 cha kuruhusu hii Bodi kuweza kukopa. Nakubaliana na Kamati kabisa kwamba haiwezekani Bodi ikaanze kukopa kwa *discretion* zao wenye, lazima kiwepo chombo kingine kinachodhibiti hata kama ni Waziri, *consultations* ziwepo na kuwepo mtu anayeruhusu, waombe kibali cha kuweza kukopa. Vinginevyo walimu watabambikiwa madeni makubwa, wataambiwa walipe kwa sababu Bodi inakwenda kukopa kwa niaba ya walimu. Kwa hiyo, kama hawajapata idhini, wakajikopea wanavyotaka tu, leo tutakuja kushangaa kwamba walimu hawa ambaao wameundiwa hiki chombo itakuwa kwao ni maumivu zaidi ya kunufaika na chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni hayo machache, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sakaya kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Haonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

MHE. PASCHAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuunga mkono mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo yametolewa hapa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuanzishwa kwa Bodi hii itakuwa ni tatizo la unyonyaji kwa walimu wetu. Leo tunasema kwamba walimu watakatwa ada ya cheti cha usajili, lakini pia watakatwa ada ya leseni ya kufundishia kila mwaka, huu naona ni unyonyaji mkubwa sana kwa walimu ambaao unaenda kufanyika kama tutaenda kukubali kuitisha suala hili bila kulifanyia marekebisho na bila Serikali kuzingatia ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo walimu wanakatwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, waliosomeshwa au walionufaika na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, leo walimu wamekopa kwenye taasisi zetu za fedha ikiwepo benki na taasisi mbalimbali, wapo walimu leo wanapokea mshahara mdogo sana, wengine wanapokea hadi Sh.50,000. Kuna mjumbe mmoja kazungumza humu ndani amesema Sh.100,000 lakini kuna wengine wanapokea Sh.50,000 na wengine hawana kitu. Sasa leo tunaenda kuwaongeza hizi ada kulipia leseni kila mwaka na kulipia ada ya cheti kila mwaka, tafsiri yake ni kwamba tunaenda kuwaongeza mzigo mkubwa sana. Nadhani kama alivyoongea Mbunge mmoja humu ndani ni vizuri hizi ada za leseni zikaondolewa ili sasa waweze kusajiliwa bure na inawezekana kabisa. Kama mnasema kwamba kwenye elimu bure mmefanikiwa sasa hili kwa nini dogo msiliweze? Unawezaje kufanya kubwa bure na hili dogo ukashindwa kufanya bure? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la mkanganyiko wa majukumu yanayomhusu mwalimu. Wamezungumza Wabunge wengi humu ndani, leo mwalimu anaajiriwa na Utumishi, mwalimu analipwa na TAMISEMI, mwalimu anaanza kupandishwa daraja na TSC, naona kwamba kinachofanyika hapa ni kuwachezea walimu wa nchi hii, ni kufanya mzaha kwa walimu wetu. Mkanganyiko huu wa majukumu tunaweza kuuondoa tukawa na chombo kimoja tu cha kuhangaikia matatizo ya walimu au mambo ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nchi kama ya Kenya nao wana TSC na siyo dhambi Watanzania kwenda kujifunza Kenya, hii Bodi ya Taaluma ya Ualimu Kenya wanayo lakini iko chini ya TSC. TSC ya Kenya inaaajiri mwalimu, inampandisha daraja mwalimu, inamlipa mwalimu, inafanya kila kitu. Tanzania tunafanya vitu vya ajabu sana na hii ni aibu kubwa sana na kwenda kujifunza kwa mtu aliyefanikiwa sio dhambi. Jambo la muhimu tujifunze Wakenya wamefanyaje na baada ya hapo naamini sasa tutakuja na Bodi nzuri yenye maslahi kwa Watanzania na ambayo mwisho

wa siku itamsaidia mwalimu badala ya kwenda kuwachanganya walimu wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Mwenyekiti wa Bodii ya Taaluma ya Ualimu anavyopatikana. Mnasema leo Waziri ateue Mwenyekiti wa Bodii, tutaenda kupata akina Kailima wengine. Tunajua Waziri ni kada wa Chama cha Mapinduzi, hata kama kesho CHADEMA itaongoza nchi hii bado huyo Waziri atakuwa ni kada wa Chama cha CHADEMA, hata kama ni CUFwataongoza nchi hii, lakini huyo bado atakuwa ni kada wa chama. Mwisho wa siku tutapata Mwenyekiti wa Bodii ambaye ni kada wa chama cha siasa, tutaenda kuzalisha akina Kailima wengine kwenye ualimu na mwisho wa siku matatizo yatakuwa makubwa zaidi ya kuyapunguza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba tutafute utaratibu mwингine ambaa ni mzuri, huyu Mwenyekiti wa Bodii tumtafute kwa njia nydingine ambayo ni bora zaidi ambayo haitakuwa kumteua, ikiwezekana wafanyishwe hata mitihani hawa watu waweze kapatikana na sifa nydingine. Tukienda kuteua, Waziri ataenda kuteua mtu ambaye ni wa chama chake, hatutapata Mwenyekiti wa Bodii hapa tutapata kada wa Chama cha Mapinduzi na mwisho wa siku hii Bodii ya Taaluma ya Walimu itakuwa ni Bodii ya CCM, haitakuwa ni Bodii ya Walimu katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma vizuri kwenye Muswada huu, Bodii ina uwezo wa kukataa kumsajili mtu na sababu za kukataa zikaambatanishwa ndani ya mwezi mmoja. Tunafahamu kwamba watumishi wa umma wanaruhusiwa kuwa kwenye vyama vyaa siasa ili mradi wasifanye siasa mahali pa kazi na muda wa kazi. Kama wanasema Bodii ina uwezo wa kukataa kumsajili mtu na sababu za kukataa kuambatanishwa tafsiri yake ni kwamba ikionekana kwamba yule mwalimu ana mtazamo au ni mwanachama wa chama kingine uwezekano mkubwa wa kumpiga chini unaweza ukajitokeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitengeneza msingi msingi mzuri wa nyumba ndipo utakapopata nyumba ambayo ni imara na bora lakini tukianza kwa msingi mbovu tutaenda kupata Bodi ambayo ni mbovu sana ambayo haijawahi kutokea katika Taifa letu. Kwa hiyo, niombe tu ni vizuri tukaa vizuri, tukatulia na tusiwe na papara ili mwisho wa siku tuweze kupata sasa Bodi nzuri na haina matatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema mamlaka ya Bodi pia ni pamoja na kutoa onyo, hoja ya kufukuzwa au kuondolewa kabisa kwenye orodha ya usajili kwa mwalimu atakayefanya kosa na kuhukumiwa kifungo cha zaidi ya miezi sita. Bado naona wapo watu wanaweza wakaa tu kwenye ile Bodi kwa sababu wapo chama fulani wakaamua tu kumshughulikia mtu mwingine kwa sababu ya mtazamo tofauti wa kisiasa. Ni vizuri mambo haya tukatengeneza vizuri ili tuweze kutengeneza chombo kizuri kwa walimu na mwisho wa siku mambo yaweze kwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza maneno hayo naomba nikazie zaidi hasa hili la ada na makato ya leseni, hapa ni vizuri ikawa bure kabisa. Mishahara kwa walimu haijawahi kuongezwa, mishahara ambayo walimu wanapokea leo ni mishahara aliyoiacha Rais wa Awamu ya Nne Kikwete, Rais wa sasa hajawahi kuongeza mishahara kwa walimu. Leo mnaongeza makato, tukisema muongeze mishahara mnasema kwamba hadi mmalize Stiegler's Gorge na *Standard Gauge* ndiyo mtaongeza mishahara kwa watumishi wa umma. Sasa Rais huyu wa wanyonge, kwa kweli ni vizuri mkaangalia mambo haya tusijetukayapeleka vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo hapa na ni Serikali ambayo imejinasibu kwamba ni sikivu, naamini kwenye hili itasikia. Kwa mtazamo wangu kama haya hayatachukuliwa maana yake Serikali itakuwa mmeweka pamba masikioni, mambo yatakuwa ni yaleyale na *businessitakuwa ni as usual*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na Mungu akubariki sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ulikuwa umeanza kuelekea kusiko. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Rehani ajiandae.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitoe pongezi kwa Wizara, Mheshimiwa Prof. Ndalichako, Naibu Mheshimiwa Olenasha pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kutuletea Muswada huu muhimu sana katika maslahi na maendeleo ya tasnia ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba kwa muda mrefu tasnia hii ya ualimu ambayo sisi wengine ndiyo imetulea imetuwa ikidharaulika, haitambuliki na haiheshimiki. Ukilinganisha na fani nyngine kama madaktari, wahandisi na wanasheria kumekuwa na tofauti kubwa. Madaktari, wahandisi na wanasheria wamekuwa na sheria zao za kutambua na kulinda taaluma yao na kwa kuititia sheria hizo tumeona fani hizi zimeweza kukua, kuendelea, kuheshimika na hatimaye kupata maslahi mazuri. Hivyo Muswada huu unakuja kutibu tatizo ambalo limewakuta walimu kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiusoma vizuri Muswada utagundua unaongelea mambo makubwa matatu. Moja, ni usajili na utambuzi kwa walimu, kwanza kuwatambua na hatimaye kuwasajili ambalo ni jambo jema kabisa. Kwa sababu hata kama unataka kumuongezea mtu maslahi na unataka kumuelimisha zaidi kwanza lazima umtambue na umsajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni maadili. Wote tumekuwa tukisema na tukilalamika kwamba maadili ya

walimu yameshuka. Sasa Muswada huu unakuja kushughulikia suala hilo la maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Muswada huu pia unaongelea maslahi. Tunaposema maslahi wengi tunakimbilia kwenye fedha lakini hata kumuendeleza mwalimu kitaaluma ni maslahi kwa sababu akiendelezwa kitaaluma ndipo ataweba kupata kipato zaidi. Ukimsajili na kumtambua ndipo atapata maslahi zaidi, zitatokea fursa walimu wa aina fulani wanahitajika ndani na nje ya nchi, kwa sababu umewasajili na umewatambua basi pia suala la maslahi linakuja vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye suala la maslahi ni vizuri pia kusisitiza kwamba tunapofanya usajili lazima Mheshimiwa Waziri na timu yake kuangalia ni kwa jinsi gani kutakuwa na kipengele cha kuweza kuongelea maslahi bayana katika sheria hii. Tunajua ni *professional instrument* lakini lazima kuliongelea hilo kwa sababu maslahi kwa walimu imekuwa ni kilio cha muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maslahi liliwahi kuongeleta na moja kati ya viongozi ambao wanaheshimika sana duniani, *Chancellor* wa Ujerumani Angela Merkel alivyoulizwa kwamba kwa nini anawalipa walimu kule Ujerumani mshahara mkubwa zaidi kuliko fani nyingine. Akasema kwamba ninyi madaktari, wanasheria na wahandisi mnataka mlipwe zaidi ya walimu waliowafundisha. Kwa hiyo, hapo nasisitiza suala zima la maslahi, tuhakikishe kwamba katika kuuboresha Muswada huu suala la maslahi liwekwe bayana. Umeongelea vizuri maslahi ya kuendeleza kitaaluma lakini tuweke pia na maslahi mengine kwa walimu hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Muswada huu vizuri na kama umesikiliza mawasilisho yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri leo pamoja na Kamati ni wazi kabisa kuna baadhi ya walimu toka wameajiriwa na wamefanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 hawajawahi kupata mafunzo yoyote ya ziada kwa sababu hawajatambuliwa. Sasa hii ni fursa kwa

walimu hao na wengine wa namna hiyo kuweza kupata mafunzo kama hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha mwalimu kuwa na leseni na ni utaratibu ambao upo kwenye nchi nyingi tu duniani ikiwemo nchi ambayo tunapenda sana sisi kuinukuu mambo yake, Marekani nao wana utaratibu wa kutoa leseni kwa walimu, ni kitendo ambacho kinaongeza hadhi ya mwalimu. Mtu kuitwa *licensed teacher* inamuongezea hadhi na heshima, anaweza akatumia leseni ile mpaka kwenda kwenye nchi nyingine za Afrika Mashariki na dunia na ikamsaidia katika kufanya mambo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hizi leseni kwa walimu zitaondoa walimu makanjanja. Tunalalamika kwamba elimu imeshuka lakini wanaofundisha hawa siyo walimu kweli ni walimu ambao wamejipachika joho la ualimu wakati siyo walimu, tunawaita walimu makanjanja, leseni zitawakimbiza. Sasa ndiyo muda huu wa kutibu matatizo ya kushuka kwa elimu yanayotokana na walimu makanjanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni hizi zitawafanya walimu hawa nao binafsi waweze kukua kitaaluma lakini ziwafanye waweze kupata soko la nje na ndani. Nitoe mfano hivi sasa lugha ya Kiswahili inakua duniani na walimu wa Kiswahili wanahitajika duniani. Je, Tanzania tuna walimu wangapi wa Kiswahili, hiyo takwimu hatuna lakini kupitia leseni hizi tutajua tuna walimu wangapi na kuwatafutia soko walimu hawa katika nchi mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwa makini kifungu cha 21 cha sheria hii ambacho kimewekwa vigezo vinavyomfanya mwalimu aweze kusajiliwa au asisajiliwe. Ukisoma kwa makini vigezo hivyo vimeweka uwazi wa hali ya juu, havijatoa tu mamlaka ya jumla, ipo bayana mno ni kwa kiasi gani mtu anaweza akasajiliwa na asisajiliwe, kiasi kwamba hata ukikataliwa kusajiliwa unajua ni kwa nini umekataliwa kwa sababu kifungu cha 21 cha Muswda huu kimejieleza vizuri sana. Ndito unaona hapa sasa nia nzuri ya

Serikali katika kuhakikisha kwamba kila mwalimu mwenye sifa hawezi kukosa kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu, maadili na miiko ya ualimu ndiyo msingi wa mafanikio na kukua kwa taaluma ya ualimu. Muswada huu unasisitiza hivyo vitu kwamba lazima kuwe na nidhamu, maadili na miiko. Hivi sasa ukimkamata mwalimu unaanza kutafuta tumshughulikie VIPI wakati chombo kama hiki hakipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu na naomba niseme kwamba ninaunga mkono Muswada huu ili tuendane sambamba na nchi nyingine za Afrika Mashariki na dunia nzima katika kukuza elimu kwa kupitia kuwasajili walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kwa mchango wako mzuri, Mheshimiwa Janet Mbene na baadaye Mheshimiwa Rehani.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa ufupi Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu ni sehemu muhimu sana ya jamii yetu na kwa kweli wanapaswa kuthaminiwa kwa kiasi kikubwa sana. Ila nina tatizo kidogo baada ya kupitia huu Muswada kutofautisha sasa majukumu ambayo yanalengwa kufanya na hii Bodi tunayotaka kuiunda na ile *Teachers Service Commission*. Naona kuna maeneo mengi ambayo yanafanana na mpaka najiuliza sasa nani atafanya nini na nani ataacha kufanya nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiria kuna haja ya kuangalia jinsi ambavyo aidha tuta-harmonize hiyo *Teachers Service Commission* tukaingiza hivi vitu ambavyo ni vipya kwenye Bodi vikaingia kule, au kama

alivyopendekeza Mheshimiwa Balozi Kamala basi tuitipishe hii lakini tukiwa na mawazo ya kuja kutengeneza *Professional Board* ambayo itazingatia tu masuala yanayohusiana na kukuza taaluma ya ualimu kwa maana jinsi ambavyo wao wenyewe watakuwa na viwango vya juu vya weledi lakini vilevile vya kufundishia na watakuwa na njia ambazo watakuwa wanafanyiwa tathmini wa kuona jinsi gani ambavyo wanatenda kazi zao kwa njia ambayo inazingatia viwango ambavyo tunavitegemea kwa ajili ya elimu ya watoto wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kuwa lazima sisi wenyewe tuwe na taasisi ambazo zinawafundisha vizuri walimu wenyewe ili na wao waje kufundisha vizuri watoto wetu. Hii naiona kuwa ni changamoto ambayo sasa hivi ndiyo inayotukabili. Suala la kuwa na viwango, taaluma ambayo inatambulika kwa walimu naona ni muhimu sana hasa kwa sasa hivi ambavyo tunajua kuna mabadiliko mengi yanayotokea duniani, kuanzia utandawazi na masuala ya mabadiliko ya teknolojia na mahitaji mengi ya Taifa letu au dunia kwa ujumla la maendeleo ambayo yanajitokeza. Hii lazima tuiangalie kwa uangalifu, wengi wamezungumza kuwa tuna taasisi nyingi zinasimamia walimu na kuna nyingi ambazo unaona kuna kazi zinaingiliana, kwa kweli tusipoangalia tutajikuta tunaongeza mzigo wa taasisi lakini tija itakuwa siyo ya kutosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana kuona Muswada huu unajikita kwenye jinsi gani tunawasaidia hawa walimu kufikia hivyo viwango. Naona tumezungumzia zaidi leseni, usajili, nidhamu na jinsi ya kuwawajibisha lakini sioni mahali ambapo tunazungumzia tunawaboresha vipi wao wenyewe ili wafikie hivyo viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua hata *Professional Boards* nyininge wana viwango vyao ili uweze kuhesabiwa kuwa wewe ni *professional*/na ukawa *registered* kwenye hiyo *board* kuna hatua ambazo unachukua. Hapa sijui tutaangalia kitu gani, tutaangalia jinsi anavyofundisha darasani, elimu yake, nidhamu, jinsi ambavyo ni mbunifu

katika kuweka mikakati ya kufundishia vizuri zaidi kwa watoto ambao labda wana matatizo maalum au tutaangalia kitu gani ili tuseme kuwa huyu sasa ndiyo anafaa kupewa leseni au usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumekuwa na mabadiliko mengi sana katika sekta yetu ya elimu. Ssijui katika kuleta Muswada huu mbele yetu tumeangalia sasa mambo yote haya, hizi *reforms* mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza na tumezi-*incorporate* katika Muswada huu ili sasa tuunde kitu ambacho kinazingatia yale mambo yote madogomadogo ambayo yamekuwa yakifanyika *overtime* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi kwangu ni lazima utambuzi wa viwango uwe ni wa kisayansi zaidi, usiwe unaotokana na Bodi labda au watu walioko kwenye Bodi. Tuwe tuna vigezo vyta kisayansi vinavyotokana na hii tasnia ya ualimu ambavyo mtu ye yote akiviona anaweza kusema huyu amekidhi au huyu hajakidhi. Isiwe ni kitu ambacho ni *subjective* kwa sababu naanza kuona hofu ya kuwa inaweza kuwa tu mtu fulani akaona hiki kwa mtazamo wake ye ye kiko hivi akaona hakifai au kinafaa kumbe sivyo. Kwa hiyo, nataka ningeionna hiyo inajitokeza, kuwa vigezo vitakuwa ni hivi, mtu atakuwa anatakiwa awe amesomea hivi na hivi na atakuwa ana ufaulu huu na huu ndiyo sasa atatambulika kuwa sasa huyu ni *professional* na huyu ndiyo anapaswa kupata leseni na *registration*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi ambayo yamezungumzwa hapa. Kuna walimu wengine tumesikia hapa walimu wa kijitolea wamemaliza *form six* na *form four* wanajitolea na tunasikia kuna wahadhili ambao hawajasomea ualimu lakini wenyewe ni wataalam wa fani zao wanawekwa kuwa walimu, hivi vyote lazima vianishwe katika huu Muswada. Je, hawa watakuwa *treated* vipi, sasa watakuwa hawafundishi tena ama vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna suala la shule za *private* sijalielewa vizuri, walimu wa shule za *private* na

wao watafanyiwa *registration* na *scrutiny* ni hii au wao wanaachwa peke yao, wako nje au ndani ya huu mfumo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia masuala ya kuunganisha masuala ya hii *professionalism* tunayoitafuta hapa na masuala mengine yote ambayo yapo katika taasisi mbalimbali ambazo zimeundwa kwa ajili ya walimu. Hii itasaidia sasa kuja na kitu ambacho kinazungumza lugha moja. Wengine wametoa mifano hapa kwamba unaweza ukakuta kwenye *TSC* kuna jambo tofauti, ukaja kwenye Bodii yanakuwa tofauti kukawa kuna mgongano halafu maamuzi yakashindikana kuitishwa au yakapitishwa yakawa yanakiuka sheria ya upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuuliza kwanza tunavyozungumzia kuwawekea walimu huu utaratibu wa kuwa na Bodii yao ya *professionalism*, tunaweza kuoneshwa wapi ambako tunawaandaa sasa wakaelewa kuwa, sasa hivi huko tunakoelekea, ili upate leseni lazima uwe umekidhi viwango hivi na hivi na tunapowawekea viwango hivyo tuna matayarisho gani ya kuwafikisha hapo? Kwa sababu walimu lazima waendelezwe, wapate fursa za kujiendeleza na kuendelezwa, wapate misaada mbalimbali katika kazi zao wakiwa kazini au nje ya utaratibu wa kazi, lakini lazima wajengewe huo uwezo wa kufikia hiyo *professionalism* au hizo *professional standards* zinazotegemewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka kuuliza kama swalii, hili suala la nidhamu ambalo naona kwa kiasi kikubwa sana ndilo lilitazamwa humu ndani, *TSC* na wenyewe wanalisimamia kipengele kwa kipengele. Sasa sijui sasa hivi suala la nidhamu na maadili ya walimu tutaliacha *TSC* au litahamia Bodii? Kama litahamia Bodii, *TSC* watakuwa wanafanya kazi gani? Kwa hiyo, nakuta kuna vitu vimeingiliana sana ambapo inanipa wasiwasi kama hii Bodii siyo *duplication* ya *TSC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mapendekezo tu kwa kiasi fulani. Nafikiri tunapozungumzia kuwa na walimu bora ambao wana viwango vinavyohitajika na kuwa tunapata

wanafunzi bora huku nyuma lazima kuwe kuna sehemu ya tatu inayozungumzia kuwawezesha hawa walimu kufikia hapo wanapotakiwa. Tuna haja sasa ya kuhakkisha kuwa *teachers training* inayotolewa kwa walimu inalingana na viwango tunavyotegemea kwenda kuviona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lazima kuwe na vigezo maalum ambavyo vinatambuliwa *globally, East Africa* au *Nationally* kuwa hiki kweli ni kiwango ambacho huyu amekifika na lazima apate leseni *otherwise* iwe hakukipata. Pia iwe rahisi walimu kufikia hivi viwango ambavyo tumeviainisha kwenye Bodii, isiwe tena ni kazi ngumu sana mwalimu kufikia huko. Kwa mfano, mwalimu anapotaka kwenda kujidendeza, je, ni rahisi kiasi gani ye ye kwenda kujidendeza kwenye fani ambayo anaitegemea kwa sababu anajua ndiyo itakayomfikisha katika kiwango? Je, walimu wanaweza kupata *scholarships*? Je, walimu wanaweza kupata *leave of absence* waende wakasome? Je, walimu wanaweza wakapata usaidizi hata kama ni mikopo kwa ajili ya kujisomesha? Hivi vyote lazima viendane na utaratibu ambaao tunataka kuunda, lazima kuwe kuna uwezeshwaji. Walimu wengi sasa hivi wanajihangaika wenyewe. Kuna mtu kazungumzia kuku wa kienyeji, sijui kama ni sahihi, lakini ninachosema mimi ni kwamba wanaachiwa wahangaike wenyewe, lakini hata wakihangaika bado wakirudi hawapati stahiki zile ambazo zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua huu Muswada hauzungumzii stahiki za walimu, lakini hivi vitu vinaendana. Mtu hawezi kuona sababu ya kuhangaike kwenda kujidendeza na kufundisha vizuri zaidi na kutengeneza mikakati maalum ya kufundishia ambayo ni ubunifu wake mwenyewe kama hakuna mahali atakapopata *recognition* ambayo ni sahihi na ambayo anastahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kusema kuwa huu Muswada unaweza kuwa ni mzuri lakini unahitaji maboresho mengi sana kadri ambavyo tumesikia uchangiaji kila upande umezungumzia. Huu Muswada sitaki kusema umewahishwa lakini naweza kusema labda haujaiva vizuri

sana. Kwa hiyo, nataka kuomba, kama inaweze kana tuuangalie vizuri zaidi kama utarudishwa kwenye Kamati, kama utarudishwa wapi ili ukabobereshwe. Kwa sababu naona una mwingiliano sana na Kamisheni nyingine za Walimu ambazo tayari tunazo, sasa hiyo inaweza kuwa ni tatizo tunavyoendelea mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbene kwa mchango na ushauri wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Rehani.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia katika Muswada huu. Nina mambo machache ya kuweza kushauri kwenye Bodii hii ya Kitaalam ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naona ili Bodii iweze kujengwa lazima ichukue majukumu ya taasisi na bodi nyingine zilizopo ndani ya Wizara ya Elimu ili iweze kujijengea sasa misingi ya kuweza kufanya kazi. Kwa sababu inasimamia elimu, lazima baadhi ya mambo yaliyokuwepo pengine NECTA, Chama cha Walimu au kwingine kokote ambayo yanahusiana na taaluma yaweze kusimamiwa na Bodii hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodii hii inatakiwa kwanza iwe na meno, kitu ambacho kwa kweli inabidi Waziri aje atueleze *structure* nzima itakuwa vipi mpaka kuweza kujenga vizuri ili iweze kuwa na meno ya kufanya kazi hii ya kitaaluma. Kwa sababu hapa pana tatizo. Isipokuwa na meno bodi hii itashindwa kutekeleza majukumu yake na kitakuwa ni chombo tu cha Serikali kama vilivyo vingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo tunaliona ni kwamba hapa Bodii hii inatakiwa isimamie na maadili ya walimu. Maadili yanakuwaje sasa? Wenzangu wameweza kuzungumza hapa ni kwamba maadili yanaendana na maslahi vilevile, yaweze kuwa sambamba ili kuweza kusimamia hayo maadili yenyewe. Kwa mfano,

tofauti iliyopo kwa walimu wa vyuo na wale walimu wanaofundisha shule za msingi na sekondari inakwaza. Kwa sababu ukimchukua mwalimu mwenye *degree* moja au *master's* akiweko chuoni anakuwa ni *Assistant Lecturer*, lakini akiwa shulenii anakuwa mwalimu tu wa kawaida na mshahara wanatofautiana. Kule pengine akianza kwenye chuo huyu mtu anaweza kuanza na Sh.1,800,000 lakini huku sekondari au shule ya msingi pamoja na *master's* yake mtu huyu anakuwa anapata na Sh.800,000 na Sh.700,000. Kwa hiyo, hapo hakujawa na *consistency* ya taaluma hasa. Kwa hiyo, Bodi hayo ndiyo mambo inayotakiwa ijikite iweze kueleza na ichanganue madaraja ya walimu ili kuweza kuonekana hayo maadili yanayotakiwa kila mmoja anatekeleza wajibu wake kwa nafasi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo llingine, Bodi hii kwa mujibu wa maelezo ya Waziri hapa nilivyoipitia inataka kuangalia hawa walimu ambao wapo tu hapa nchini na hawatambuliki. Mimi nakubaliana na usajili wa walimu kwani unatusaidia kwanza kupembua wale walimu halisi kwa *qualification* na uajiri wao ulivyokwenda sahihi kabisa Serikalini na wale makanjanja ambao wamejipandikiza tu pengine labda amefukuzwa kazi, ametafuta sehemu ya kufundisha basi amepata amejiingiza katika hiyo tasnia. Wengine tunawaajiri, anafukuzwa huku anahamia mkoa mwingine anatengeneza mazingira anaajiriwa tena, tunajua hayo yanafanyika. Hivyo, usajili utasaidia kuweza kuwatambua hawa walimu, huyu ni nani na taarifa na *qualifications* zake. Hii siyo haifanyiki hapa tu, dunia nzima ndiyo iko hivyo, lazima kuwepo na usajili wa walimu na leseni lazima zilipwe, hakuna usajili wa bure, hivyo ndivyo ukweli ulivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika usajili huu tuweze kuwajua, ambao siyo wetu waondolewe. Kama tulivyoweza kuwaondoa wale wenye vyeti feki na vitu vingine, hawa wasio na *qualifications* nao basi tuweze kuona kwamba Bodi imesimamia na wanaondoka katika hii tasnia tubaki na ile *cream ambayo tunaihitaji*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunataka kuona kwamba Bodi hii inashughulika na taaluma za walimu hasa huku chini. Kwa sababu duniani au huko kwa wenzetu, walimu *qualification* na *vetting* kubwa inafanywa kwa shule za msingi na *nursery* na ndiko kunakopatikana walimu wenye uwezo kabisa wa kujenga wale wanafunzi ambao juu wataweza kwenda kufanya vizuri. Tofauti na kwetu inavyoonekana mwalimu akishakuwa na *diploma* na *degree* hataki kufundisha chini, lakini inawezekana mwalimu huyu hajaiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wale walioiva taaluma iweze kufanya kazi kwa kuiva kwako tukupeleke utujengee *foundation* kwa wanafunzi wetu ili wakija juu tuwe tunapata urahisi kwa wanafunzi ambao wamejengeka vizuri. Hizo ndizo kazi tunazotaka tuiione Bodi hii ina meno na kusimamia hilli na isiwe inaridhia kila mtu anayekwenda, kwamba ameshakaa kule chini miezi mitatu anaomba akafundishe juu ameruhusiwa, amekwenda zake juu kwa mujibu wa taaluma yake. Kwa wenzetu Ulaya mpaka ukifika kukubaliwa kufundisha pengine *nursery* au *primary School*, umefanyiwa *vetting* ya kutosha. Naomba Bodi hii iweze kuwa na uwezo wa kupembua walimu ambao wataweza kujenga *foundation* nzuri na kujenga watoto ambao wanaweza kuja kufanya vizuri huku mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia taaluma hizi zina migawanyiko mbalimbali, baadaye Bodi hii iweze kutuvekea madaraja na taaluma mbalimbali. Kwa mfano, tuweze kuwa na Walimu wa *Arts* na madaraja yao; Walimu wa *Sayansi* na madaraja yao; Walimu wa *Hisabati* na madaraja yao; Walimu wa *Fizikia* na madaraja yao, ili sasa tuwe na *cream* ya walimu ambayo tunasema tukiwa na *package* ya walimu wa *Fizikia* ni hawa, wa *Kemia* ni hawa, wa *Baiolojia* ni hawa na masomo mengine tutaweza kuwa na mgawanyo mzuri wa hizi *resources* katika maeneo yetu na hasa yale maeneo ambayo tunahisi kwamba yana upungufu wa Walimu wa *Sayansi* au Walimu ambao wanahitajika, hasa wa *Hisabati*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Bodi hii naomba iwepo lakini vilevile naomba ikae pamoa na Mabaraza mengine ambayo yameshaundwa hapa nchini ili sasa iweze kujijengea uwezo. Wasiwasi wangu ni mmoja tu, hii Bodi itakapoundwa, hawa Wajumbe wa Bodi wanavyoweza kupatikana, niombi sana hapa siasa isitumike. Tunaunda Bodi ya Wataalam siyo Bodi ya Wanasiasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili lazima tulizungumze kwa uwazi. Tunapozungumzia taaluma, *it is a special case*, hatuhitaji siasa hapa. Kama mtu anapelekwa kwenye kuteuliwa na Rais awe *professional*. Kule kwenye Baraza la Watafiti tunasema kwamba lazima uwe *on boat*, kama haupo *on boat* hustahili. Tusichukue mtu tu ambaye ame-*retire* kwenye *u-engineer* au kwenye mambo yake mengine huko tunamleta hapa kwa sababu ana *PhD* au ana kitu gani, hapana! Tuwe na mtu ambaye yupo kwenye tasnia na anaweza kusimamia masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Rehani kwa mchango wako.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa William Olenasha Mbunge, Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanafanya katika Wizara hii ili kuboresha taaluma hii ya ualimu hapa Tanzania kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania wa mwaka 2018 (*The Tanzania Teacher's Professional Board Bill, 2018*). Muswada huu ni mzuri kwa maslahi ya walimu wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Malipo ya kupata leseni yaendane na kipato cha walimu maana walimu mishahara yao ipo chini sana na wengi wanadai stahiki zao kwa muda mrefu. Hivyo, malipo ya kupatiwa leseni yakiwa madogo yatasaidia kila mwalimu kuweza kupata leseni kwa wakati mara tu Muswada huu utakapopitishwa.

(ii) Taaluma nyingi zina utambuzi wa bodi, isipokuwa taaluma ya walimu. Hivyo basi nashauri Mwenyekiti wa Bodi badala ya kuteuliwa na Waziri wa Elimu, ateuliwe na Mheshimiwa Rais kama zilivyo bodi nyingine.

(iii) Walimu ambao si raia wa Tanzania (*expertise*) nao pia licha ya kuwa na leseni zao kutoka nchi husika, Bodi hii ya Walimu itakayoanzishwa iweze kumpa mwalimu ambaye si raia leseni na mkataba maalum ili aweze kufanya kazi yake kwa weledi. Hii itasaidia mwalimu huyo kufuata matakwa yote ya nchi na kutoa elimu yenye tija kwa watoto wetu.

(iv) Bodi ihakikishe walimu kuanzia shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu na walimu wa vyuo vikuu wote wanapatiwa leseni hizi mara baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa sheria.

(v) Walimu hao wakishapewa leseni kusiwe na masharti magumu ya kutomruhusu kwenda nchi ya jirani pindi atakapohitaji kwenda kufundisha huko.

(vi) Baada ya Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania kupitishwa na kuwa sheria, Serikali ione haja sasa ya kukaa pamoja na *Tanzania Service Commission*, ambacho ndicho chombo kinachoshughulikia maslahi ya walimu Tanzania ili kuweza kuboresha stahiki za walimu wetu. Maslahi pamoja na kuwepo kwa Bodi ya Taaluma ya Walimu itaweza kuleta tija kubwa sana kwa elimu ya Tanzania maana itaweza kuinua kiwango cha elimu na kuleta ufaulu wa hali ya juu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawatakia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Prof. Joyce L. Ndalichako pamoja na Naibu, Mheshimiwa William Tate Olenasha afya njema na umri mrefu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku ya kuwatumikia Watanzania.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania ni jambo zuri kama itafanya kazi kwa kuwasaidia walimu wa Tanzania, walimu wana mahitaji mengi sana ambayo wanahitaji kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Walimu iangalie isije ikaanza kufanya kazi za Chama cha Ualimu Tanzania (*CWT*). Majukumu ya Bodi na *CWT* yawekwe bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wana michango mingi sana kwa mfano kuchangia *CWT*; Bima ya Afya; *PAYE*; *LAPF/PPF* na sasa Bodi ya Walimu. Makato haya yanaweza sababisha mwalimu kupata mshahara mdogo sana na kufanya maisha ya mwalimu kuwa magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupima kiwango cha elimu ya mwalimu siyo kazi ya Bodi, mwalimu anapimwa na chuo alichosoma ndiyo maana wanafanya mitihani. Labda Bodi isaidie katika kuangalia haki na maslahi ya mwalimu pamoja na mazingira ya kazi ya mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuangalia tabia ya mwalimu hii inaweza saidia kama Bodi itakuwa inaratibu semina na mafunzo mbalimbali kwa walimu ili wasijisahau katika kazi zao. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Walimu ni kiungo muhimu sana kwa walimu ila Serikali ipunguze msururu wa vitengo vinavyowasimamia walimu angalau viwe viwili au vitatu tu. Maoni yangu katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Majukumu yanagongana kati ya Tume na Bodi, kwa nini zisiunganishwe ikawa chombo kimoja kuliko kuwa na utitiri wa vyombo vinavyowahudumia walimu ilhali majukumu yao yako sawa?

(ii) Leseni zisilipiwe ama kama ni lazima zilipwe basi ni kwa kuanza kujisajili tu na siyo kila baada ya kipindi fulani.

(iii) Hizi ada ni nydingi, kwa mfano, ada ya leseni na ada ya cheti cha usajili huku ni kuwakandamizi walimu kwa utiriri wa ada sasa imekuwa kama ni chanzo cha mapato.

(iv) Nidhamu ya mwalimu haiangaliwi kwa utaratibu wa tabia yake. Nidhamu utaijua pindi utakapomwajiri na sio kabla ya ajira.

(v) Vigezo viwe ni vile vyenye kuhusiana na taaluma ya ualimu.

(vi) Walimu wapewe stahiki zao zote ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na sio kulimbikiziwa madeni. Walimu wapolimbikiziwa stahiki zao watakuwa na misongo ya mawazo na hawatawajibika ipasavyo.

(vii) Napendekeza kuwe na chombo kimoja tu chenye kuwahudumia walimu ndipo maadili yatafuatwa na kuwa makini zaidi kuliko kuwa na vyombo vingi. Kwa kuwa na vyombo vingi kutasababisha maadili kuperomoka kwani kila mmoja ataongoza kwa misingi yake hivyo kutakuwa na mkanganyiko wa maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa jitihada kubwa za kuinua elimu nchini. Pia niwapongeze sana kwa kuleta Muswada huu ili kuweza kuupitia na kutoa maoni yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi hii kwa kweli itakuwa na msaada mkubwa sana kwa upande wa Walimu ambaao watakuwa na weledi mzuri kwenye shule ngazi zote, kuanzia awali mpaka vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemshauri Waziri katika haya majukumu ya bodi kwa upande mkubwa yanaonesha kumweka Mwalimu katika uadilifu na kuepuka kupatikana kwa Walimu wasiofaa, ambaao ni utaratibu mzuri sana. Pia ukiangalia kwamba itasimamia maadili ya ualimu, hii itasaidia kudhibiti Walimu ambaao wana tabia zisizofaa shulenii, mfano, kuna wimbi kubwa la wanafunzi kupigwa mpaka kufa; kwa bodi hii hili litatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine Waziri angeweka majukumu kwenye bodi ya kumsaidia Mwalimu endapo atakuwa na uhitaji fulani, kama haki zake stahiki, pia kumwekeea mazingira mazuri ili awe na ari na moyo wa kufundisha; Walimu wengi wana mazingira magumu, *especially vijijiini* mpaka inasababisha wengi wao kuacha kazi.

MHE. MOHAMMED AMOUR MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehema zote. Pia napenda kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa ya kutoa mchango wangu kwa njia hii ya maandishi. Napenda kuzungumzla mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusajili Walimu wote, kwa njia na nia nzuri ni vyema kazi ya usajili ingefanywa kwa Kanda ili kudhibiti msongamano wa Walimu, hii itapelekea kuwadhibiti Walimu na kubaki maeneo ya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa leseni za kufundishia kwa Walimu, ni jambo jema ila hajafahamika kama nia hii inaonekana kama kwamba kuna lengo nyuma bayo ambalo linakuja kuwabana baadhi ya Walimu. Kwa mfano, Walimu

watapewa leseni bure, lakini baadaye watalipia kodi leseni hizo. Kwa hiyo baada ya kuwasaidia Walimu, badala yake Walimu wanamalizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna nyingine lesseni hii inakuja kuwakandamiza Walimu kushiriki na kutumia haki yao ya msingi ya kidemokrasia na kuingia kwenye Chama cha Siasa. Wale wote watakaopenda siasa za upinzani wadhibitiwe na kutishwa hata kunyang'anywa leseni hizo. Kwa hiyo, leseni huenda zikawa zinaleta kudhoofisha demokrasi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Walimu tu? Kwa nini Watumishi wengine wa Serikali na wao hawapatiwi leseni isipokuwa kwa Walimu tu? Kuna namna nyingine hapa nje ya pazia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Elimu nchini, Naibu Waziri na Uongozi mzima wa Wizara kwa Muswada mzuri ambao kwangu mimi naona umekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi hii uanzishwaji wake utakuwa ni sababu kubwa sana katika kuimarisha kiwango cha elimu, kitu ambacho kimelalamikiwa kwa muda mrefu na Watanzania wengi. Tumeshuhudia vijana wengi wakimaliza darasa la saba, kidato cha nne, sita na hata vyuo lakini uelewa wa vijana hawa ukiwa ni mdogo au wastani. Hii imepunguza ufanisi katika maeneo mengi ya kazi sababu ya kutokuwa na Walimu wenyewe viwango vinavyokubalika. Kazi ya ualimu kwa muda marefu haikuzingatia tena weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu wa Uanzishwaji wa Bodi ya Walimu hajaelezwa wazi kama ili Mwalimu aweze kusajiliwa atafanya mitihani ya kitaaluma kama ilivyo katika Bodi zingine mfano Bodi ya

Uhasibu na Ukaguzi (*NBAA*), Bodi ya Wahandisi, Bodi ya Manunuzi na kadhalika. Naomba kupata majibu juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba, Walimu hawa watakuwa wamemaliza vyuo mbalimbali vyaa ndani na nje ya nchi, pia watakuwa wamepata vyeti kwa kuzingatia taratibu za vyuo husika lakini ili uwe mwanachama na mwenye sifa katika bodi za kitaaluma duniani kote ni lazima ufanye mitihani ya bodi husika ili uweze kutambulika, kwa sababu utakuwa umekidhi sifa zinazotakiwa, nataka kujua, je, bodi hii ni tofauti na bodi nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine, naomba kipengele cha kumtaka Mwalimu asajiliwe baada ya mwaka kisiwepo, kwa sababu tutawanyima fursa Walimu wengi ambao watakuwa wamemaliza vyuo na wana sifa za kusajiliwa, hili litazamwe upya. Ikumbukwe kwamba, tunavyo vyuo vingi vyaa ualimu nchini, vyaa Serikali na binafsi ambavyo kila siku wanahitimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria hii haijasema kama chombo kipi ambacho kitaismamia bodi hii ikizingatiwa kuwa bodi hii itakuwa na dhamana kubwa ya kubebe kundi kubwa la Walimu. Jambo hili ni muhimu kwa sababu kukosekana kwa chombo cha kutazama shughuli za utendaji wa Bodi hii ya Walimu kunaweza pia kupunguza ufanisi wa utendaji, nashauri chombo hicho kiwe ndani ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu kwa siku ya leo kwa wachangiaji ambao waliletwa na vyama vyenye uwakilishi Bungeni tumeimaliza lakini Muswada huu unaendelea hadi kesho. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge mliopata nafasi ya kuchangia kwa kusema, najua na wengine mmeendelea kuchangia na kwa maandishi pia.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, sina la ziada kwa leo, sina matangazo, kwa hiyo, niwaage kwa kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, siku ya Alhamisi, tarehe 6 Septemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12.50 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 6 Septemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*